# Jinsi ya Kuanzisha Kanisa la Kristo Mahali Ulipo

na
**J.C. Choate**

Kimechapishwa na
World Evangelism Team

**Kitabu hiki kinatolewa bure na kanisa la Kristo.**
**This book is given for free by the church of Christ.**

Nakala kwa lugha ya Kiswahili
na
Swahili Gospel Team (SGT)
©2022

Tafsiri na Mpangilio
(Translation and Layout)
**Shadrack S. Msambaza**

Mhariri
(Proof reading)
**Peter Kamatula**

# Utangulizi

Katika sehemu za ulimwengu ambapo kanisa halipo, kuna hitaji kubwa sio tu kuhubiri injili, bali pia kuelezea waongofu wapya jinsi ya kuanzisha kusanyikola Bwana“kanisa” mahali waliko. Kwa sababu hii, miaka michache iliyopita niliwasilisha masomo haya kwenye Redio ya Sri Lanka, kwa watu wa India na nchi nyingine kote Asia. Wakati huo masomo yalikuwa yamechapishwa nchini India na kutumwa kwa wasikilizaji ambao waliomba. Sasa, mahubiri haya yanachapishwa tena na yatakuwa yanatumiwa na waalimu wa World Bible School na wengine kama miongozo kwa wanafunzi kote ulimwenguni.

Mahubiri haya yalielekezwa kwa wale waliozungumza na kusoma Kiingereza kama lugha ya pili. Kwa sababu hii, masomo yalikuwa yamewekewa msingi sana na hata kurudia katika jitihada za kuwasaidia vizuri wasikilizaji na wasomaji kuelewa kile kilichokuwa kinasemwa.Uchapishaji huu pia utaenda haswa kwa watu wa mataifa mengine. Ni maombi yetu kuwa yatawasaidia waongofu wapya, na kwamba yatasababisha makusanyiko mengi mapya ya kanisa la Kristo kuanzishwa ulimwenguni kote.

J. C. Choate

# YALIYOMO

1. Mpango wa Mungu kwa Mwanadamu ............................................6

2. Unahitaji Biblia ........................................................ ............. 10

3. Unahitaji Kuokoka ........................................................... ..... 15

4. Jinsi ya kutii Injili .......................................................................19

5. Jinsi ya Kulitambua Kanisa la Bwana ........................................... 23

6. Wewe ni Muhimu kwa Bwana ..................................................... 28

7. Kwanini Kanisa Linahitajika Pale Ulipo ....................................... 32

8. Jinsi ya Kuanzisha Kanisa la Bwana ............................................. 36

9. Jinsi ya kubatiza ......................................... ................................ 40

10. Jinsi ya Kuabudu ......................................... ............................. 44

11. Jinsi ya Kuhudumia Meza ya Bwana ........................................... 48

12. Jinsi ya Kusali ...................................... ..................................... 53

13. Jinsi ya Kuimba ...................................... ................................... 57

14. Jinsi ya Kutoa ....................................... ................................... 61

15. Madarasa ya Biblia .................................... ............................... 65

16. Jinsi ya kufanya uinjilisti ................................................ ......... 69

17. Jinsi ya Kujipanga ......................................... ........................... 74

18. Mahali pa Kukutana ....................................... ............................ 79

19. Nafasi ya Mwanamke ........................................................ ....... 83

20. Jinsi ya Kuwasaidia Wahubiri ..................................................... 87

21. Jinsi ya Kuwasaidia wahitaji ....................................................... 91

22. Jinsi ya kufanya kazi pamoja .................................................. ... 95

23. Jinsi ya Kusamehe ....................................... ............................... 99

24. Jinsi ya kuwa na Usafi wa Mafundisho ....................................... 103

25. Jinsi ya Kuishi Maisha ya Kikristo ............................................. 107

26. Jinsi ya Kukabiliana na Matatizo ............................................... 111

## Somo 1

# MPANGO WA MUNGU KWA MWANADAMU

Kuanzia somo hili tutazungumzia kaulimbiu ya Jinsi ya Kuanzisha Kanisa la Kristo ulipo. Tutazungumza juu ya idadi yoyote ya vitu,kulingana na yale ambayo Biblia inafundisha,mambo ambayo yatatusaidia kuona umuhimu wa kanisa la Bwana, hitaji la kuwepo mahali tulipo, na jinsi ya kufanikisha yote haya.

Kwa hafla hii, somo letu litahusiana na Mpango wa Mungu kwa mwanadamu. Tunahitaji sio tu kujua uwepo wa Mungu,sisi ni viumbe vyake, lakini pia kwamba ana mpango juu ya yote kwa mwanadamu.

Mungu alikuwepo daima, yupo sasa, na atakuwako daima. Yeye sio wa mwili au wa kidunia, bali ni Roho, kulingana na Yohana 4:24. Yeye ni *"Mungu mmoja na Baba wa wote, aliye juu ya wote, na kwa wote, na ndani yenu nyote"* (Waefeso 4: 6). Yeye sio tu aliumba mbingu na nchi (Mwanzo 1: 1), lakini alimvika kila kitu mwadamu kwa kuwaumba mwanamume na mwanamke kwa mfano Wake mwenyewe (Mwanzo1: 26,27; 2: 7).

Mwanadamu hakuja ulimwenguni kwa bahati mbaya. Wala hakuwekwa hapa duniani kuzurura bila kusudi au mwelekeo.Maisha yake yangetumiwa kwa njia bora zaidi kuliko ile ya kutafuta raha za ulimwengu huu. Badala yake, aliwekwa hapa kwa heshima yake Muumba. Zamani, Mwandishi wa Zaburi Daudi aliandika, *"Jua kwamba BWANA, ndiye Mungu; Yeye ndiye aliyetuumba, na sio sisi wenyewe; Sisi ni watu Wake na kondoo wa malisho yake. Ingieni malangoni mwake kwa kushukuru;nyuani mwake kwa sifa.Mshukuruni, na libariki jina lake"* (Zaburi 100: 3,4).

Hata kabla ya mwanadamu kuumbwa, Mungu alikuwa na mpango juu yake. Yeye alichaguliwa mapema, au aliamua mapema kuwa waadilifu wataokolewa lakini kwamba wasio haki wangepotea. Akiwaambia Wakristo wa Efeso, Paulo aliandika, *"kama vile alivyotuchagua katika yeye kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, ili tuwe watakatifu, watu wasio na hatia mbele zake katika pendo. Kwa kuwa alitangulia kutuchagua, ili tufanywe wanawe kwa njia ya Yesu*

*Kristo, sawasawa na uradhi wa mapenzi yake. Na usifiwe utukufu wa neema yake, ambayo ametuneemesha katika huyo Mpendwa."* (Waefeso 1: 4-6). Mungu alipoamua kuwa wenye haki wataokolewa lakini waovu watapotea, Amempa kila mtu uhurukuamua ni sehemu gani atakuwa. Ikiwa mtu ataamua kuhesabiwa pamoja na wenye haki, kuokolewa katika ulimwengu huu na katika ulimwengu ujao, kwa kweli lazima ajinyenyekeze kwa Bwana kwa utiifu ili apate kuokolewa, na kuongezwa katika kanisa (Marko 16: 15,16; Matendo 2:47). Kushindwa kufanya hivyo inamaanisha mtu amechagua kuhesabiwa na kundi lingine. Ingawa mtu anazaliwa katika ulimwengu huu bila dhambi, yaani mtu huzaliwa safi na mtakatifu, kufikia umri wa kujua mema na mabaya anakuwa mwenye dhambi. hapo ndipo Mungu anamwajibisha kwa matendo yake. Kwa maana nyingine ni kukiuka sheria ya Mungu, na kwa hivyo amepotea. Dhambi ni kukiuka sheria ya Mungu, ambayo inamaanisha kuwa mtu anafanya kile ambacho ni kinyume na Mapenzi ya Mungu (1 Yohana 3: 4). Akiongea juu ya watu wa aina hii, Paulo alisema, *"kwa maana wote wamefanya dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu"* (Warumi 3:23).

Mungu alimwona mwanadamu yuko katika dhambi, na alijua kuwa dhambi huleta mauti (Warumi 6:23), kwa hivyo alimtuma Mwanawe ulimwenguni kumwokoa mwanadamu. Yohana aliandika, *"Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele. Maana Mungu hakumtuma Mwanawe ulimwenguni ili auhukumu ulimwengu, bali ulimwengu uokolewe katika yeye. "* (Yohana 3: 16,17).

Mwanadamu hangeokolewa kwa haki yake mwenyewe au kupitia dhabihu za wanyama. Waebrania 10:4 inasema, *"Maana haiwezekani damu ya mafahali na mbuzi kuondoa dhambi."* Ndiyo maana Mungu alimtuma Mwanawe mwenyewe ulimwenguni kuishi kati ya wanadamu na mwishowe kufa kwa ajili ya dhambi za ulimwengu. Tunasoma, *"Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi. Basi zaidi sana tukiisha kuhesabiwa haki katika damu yake, tutaokolewa na ghadhabu kwa yeye."* (Warumi 5: 8,9). Petro alisema kwamba Kristo alizibeba dhambi zetu katika mwili Wake mwenyewe

juu ya msalaba (1 Petro 2:24). Kristo mwenyewe alisema kwamba damu yake ilimwagwa ili tupate ondoleo la dhambi zetu (Mathayo 26:28).

Jinsi gani kifo cha mtu mmoja na umwagaji wa damu yake vingeweza kutuokoa makosa yetu? Lazima tutambue kuwa si kifo cha mtu yeyote tu, au damu ya mtu yeyote, ambavyo vingeweza kumuokoa mtu. Bali kifo cha Kristo, Mwana wa Mungu, ambaye mwenyewe hakuwa na dhambi na damu ya uhai aliyoimwaga kwa niaba yetu ni jambo tofauti. Dhabihu hiyo na hiyo damu vinaweza kuokoa na kufanya sisi tusamehewe dhambi zetu.

Swali linalofuata linalokuja akilini litakuwa, "Lakini vipi damu ya Kristo inaweza kuhusika kwa ajili ya dhambi za mtu ili ziweze kuondolewa?" Kulingana na maandiko, hili linafanyika kwa kutii amri za Bwana. Baada ya kifo cha Kristo, mazishi, na ufufuo, aliwatuma wanafunzi wake na maagizo haya: *"Akawaambia, Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri injili kwa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa."* (Marko 16: 15,16). Wakati mtu anamwamini Bwana, anatubu dhambi zake, anamkiri Kristo kuwa ndiye Mwana wa Mungu, na kubatizwa au kuzikwa majini, basi kupitia utii huo anaifikia damu ya Kristo na anasamehewa dhambi zake. Paulo alisema, *"Katika yeye huyo, kwa damu yake, tunao ukombozi wetu, msamaha ya dhambi, sawasawa na wingi wa neema yake."* (Waefeso 1: 7). Hapa anazungumzia damu ya Kristo.

Katika kitabu cha Matendo matukio kumi na moja ya wongofu yameorodheshwa. Katika kila moja, rekodi inaonesha wazi kwamba kupitia utii wao wa amri za injili waliokolewa, walitakaswa, walisamehewa, au kuokolewa na Kristo na damu yake kama walivyotii amri yake. Mbali na utii kama huo hakuna wokovu.

Wale wote waliomtii Bwana na kuokolewa wakati huo huo huletwa pamoja katika kundi la watu wanaojulikana kama kanisa au mwili wa Kristo. Na takriban watu elfu tatu waliomba kubatizwa baada ya kusikia mitume wakihubiri injili huko Yerusalemu, rekodi inaendelea kusema, *"Wakimsifu Mungu, na kuwapendeza watu wote. Bwana akalizidisha kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa."* (Matendo 2:47). Hili kanisa halikuwa kanisa lingine tu, ambalo lilikuwa la mwanadamu

au lililoanzishwa na wanadamu, bali, lilikuwa kanisa la Bwana, la kiroho tena mwili wa Kristo. Iilikuwa ni lile ambalo alikufa kwaajili yake, linalovaa jina lake, ambalo atarudi kwa ajili yake siku moja. Kanisa haliwezi kumwokoa mtu yeyote, lakini Kristo ndiye mwokozi wa kanisa (Waefeso 5:23), na kwa hivyo ni lazima mtu awe sehemu ya kanisa ili aokolewe na kwenda mbinguni (Waefeso 5: 25-27).

Kama watu waliookolewa, Wakristo, na washirika wa kanisa la Bwana, basi Mungu angependa watu wake wamwabudu yeye na kuishi maisha ya uaminifu ya Kikristo ili mbinguni kuweze kuwa nyumbani kwa milele. Huu ni mpango wa Mungu kwa mwanadamu.

Ikiwa wewe ni Mkristo na mshirika wa kanisa moja tunalolisoma katika neno la Mungu - kanisa la Kristo – tunakupongeza. Kama wewe sio, tungependa kukuhimiza ufikirie kwa uzito kuhusu mambo ambayo yamesemwa, kumtii Bwana, na kuwa Mkristo tu.

Tunapoendelea na mafundisho haya tutakuonyesha jinsi ilivyo rahisi kumtii Bwana na kuwa mshirika wa kanisa la Kristo popote ulipo. Ikiwa bado hakuna kusanyiko katika eneo lako, tutakuelekeza jinsi ya kuanzisha. Endelea kujifunza na sisi na ikiwa tunaweza kujibu maswali yako, yaliyotolewa kwa fasihi, au kukusaidia katika utii wako kwa Bwana, tafadhali wasiliana nasi. [Mawasiliano: +255 (0) 764 792 979 au +255 (0) 765 098 981].

## Somo la 2

# UNAHITAJI BIBLIA

Kanisa ni muhimu sana na tunataka kukuambia jinsi gani ya kuwa sehemu yake. Pia tutaonesha jinsi kanisa linavyoweza kuwepo mahali ulipo, ikiwa hakuna kusanyiko karibu nawe.

Kanisa tunalozungumzia sio kanisa lingine tu, kama vile madhehebu, au taasisi fulani iliyoundwa na wanadamu. Bali, sisi tunazungumza juu ya kanisa ambalo tunaweza kulisoma katika Biblia, kanisa moja ambalo ni la Kristo, yule ambaye lina jina lake. Vitu vingi vinavyohusika tutavijadili kwa kina baadaye.

Tunataka kukukumbusha kwamba Mungu alikuwa na mpango kwa ajili ya mwanadamu, akamweka hapa duniani kwa kusudi maalum, akampa kazi ya kufanya, na akaandaa makazi kwa ajili ya roho yake. Yote haya yamefunuliwa katika Biblia, ambayo wewe pia unaihitaji, ikiwa unataka kujua mapenzi ya Mungu kwako ni nini.

Natumai tayari unayo Biblia, lakini ikiwa huna, tafadhali angalia kama unaweza kuipata moja. unaweza kununuliwa katika maduka ya vitabu, nakushauri utumie toleo la **Union Version** au toleo lingine linalokubalika kimaandiko. Kuna matoleo mengi, au tafsiri zinapatikana, lakini baadhi yao ni duni.

Kwanza kabisa, unapaswa kutambua kwamba Biblia ni neno la Mungu. Ni ufunuo Wake wa mwisho, au matakwa kwa ajili ya mwanadamu. Kuna taarifa nyingi katika maandiko zinazomwelezea Mwandishi wake, uvuvio, na hitaji la kuikubali kama ujumbe wa mwisho. Paulo alisema, *"Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki; ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema."* (2 Timotheo 3: 16,17). Biblia inajulikana kama sheria kamilifu ya uhuru [hususani Agano Jipya] (Yakobo 1:25), na Kristo alisema hata mbingu na dunia vingetoweka, lakini neno lake halitapita kamwe (Mathayo 24:35). Hatupaswi kuiongeza, kuipunguza, au kuibadilisha (Ufunuo 22: 18,19;

Wagalatia 1: 6-9). Sisi tuwe watendaji wa neno (Yakobo 1:22), na siku moja tutahukumiwa kwayo (Yohana 12:48).

Lakini ikiwa una Biblia, unahitaji kujua jinsi ya kuitumia kwa usahihi (2 Timotheo 2:15). Hii inamaanisha kuwa lazima utambue kwamba kuna sehemu kuu mbili za Biblia: Agano la Kale na Agano Jipya. Agano la Kale lilianza na uumbaji na kuishia kwa nabii Malaki, akitabiri ujio wa Kristo, Mwokozi. Agano la Kale linahusu kipindi cha mababa na kipindi cha Musa. Sheria ya Musa, iliyotolewa wakati wa kipindi cha pili ilikuwa sheria ya Mungu kwa watu wake wakati huo. Lakini Kristo alikuja, alitoa sheria mpya, na kwa kufanya hivyo aliifanya ile ya kwanza kuwa kuukuu, iliondolewa ili tuweze kuwa na sheria bora. Mwandishi wa kitabu cha Waebrania, akisema juu ya Kristo na badiliko hili, alisema, *"ndipo aliposema, Tazama, nimekuja niyafanye mapenzi yako. Aondoa la kwanza, ili kusudi alisimamishe la pili. Katika mapenzi hayo mmepata utakaso, kwa kutolewa mwili wa Yesu Kristo mara moja tu."* (Waebrania 10: 9,10). Kwa hivyo sisi hatupaswi kushika Sheria ya Kale, kwa kuwa sasa tunaishi chini ya Sheria ya Kristo. Watu walioishi katika Agano la Kale hawakuweza kushika sheria ya Agano Jipya (ambalo lilikuwa bado halijaja) kama vile sisi ambao tunaishi leo tusivyopaswa kushika sheria ya Agano la Kale.

Hata hivyo Agano la Kale bado ni neno la Mungu na linatumika zaidi kwa kusudi jema. Iinatoa historia ya mwanadamu na pia linaonesha jinsi gani Mungu ameshughulika na watu wake. Linatoa mifano ya wale ambao walimtii Bwana, na walibarikiwa kwa hilo, lakini kwa upande mwingine, pia linasimulia juu ya wale ambao hawakumtii Mungu na walivyoadhibiwa kwa hilo. Zaidi ya yote, linatoa unabii mwingi juu ya kuja kwa Kristo, kufa, kuzikwa, na kufufuka kwake. Tunapogeukia Agano Jipya tunaweza kuona jinsi haya yote yalivyotimizwa. Kwa hiyo, Agano la Kale lina malengo mengi, lakini hatuwezi kulifuata kama sheria na tarajio la kuokolewa.

Agano Jipya linafunua mapenzi ya Mungu kwa mwanadamu leo. Huanza na kuzaliwa kwa Kristo, maisha, kifo, mazishi, na ufufuo, na kisha huendelea kuonesha jinsi kanisa lilivyoanzishwa, na baada ya hapo, jinsi injili ilivyochukuliwa kwenda ulimwenguni pote.

Kwa kuzingatia haya yote, mwandishi wa Waebrania alisema, *"Mungu, ambaye alisema zamani na baba zetu katika manabii kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi, mwisho wa siku hizi amesema na sisi katika Mwana, aliyemweka kuwa mrithi wa yote, tena kwa yeye aliufanya ulimwengu"* (Waebrania 1:1,2). Wakati wa kugeuka sura ya Kristo, Mungu aliagiza kutoka mbinguni na kusema, *"Huyu ni mwanangu mpendwa wangu, ninayependezwa naye; msikieni yeye"* (Mathayo17:5). Hakuna shaka basi tunajua atakayesikilizwa, huyo ni Kristo. Wala hakuna shaka yoyote juu ya agano ambalo lina sheria ya Kristo, na hilo ni Agano Jipya.

Kuna mambo kadhaa tunayohitaji kuzingatia wakati tunajifunza Neno la Mungu. Kwa hivyo lazima tukubali na kuheshimu sheria ya Mungu. Hatupaswi kuikataa, kubishana juu yake, au kuiuliza. Mungu amesema kile Alichosema na hicho kinamaliza kila jambo.

Pili, Neno la Mungu halitatugawanya. Bila shaka sisi tunajua kwamba kuna watu wengi ambao wanadai kuwa wanafuata na kufundisha Biblia, lakini wamegawanyika katika kile wanachofundisha na wanachofanya. Je! Hii inaweza kuwa inawezekana? La hasha! Bwana amesema nasi sote kupitia neno lake, na wakati sisi sote tunaamini kile alichosema, na tunatii mafundisho Yake, mapenzi hayo yanatufanya kuwa wamoja. Hiyo inamaanisha kwamba sote tutaamini kitu kimoja, wote tunapata wokovu sawa, wote tunakuwa washirika wa kanisa moja, ibada ya aina moja, na kuwa na tumaini moja. Hata Kristo aliomba kwamba sisi tuwe na umoja, wala hakutugawanya. (Yohana 17: 20-23). Soma katika Agano Jipya na utaona kwamba watu wa Bwana walikuwa wamoja. Je! Inaweza kuwa vinginevyo leo na kukubalika kwake?

Tatu, Neno la Bwana ni la mwisho. Hana ujumbe mpya kwa mwanadamu leo na wala hatatoa ufunuo mpya katika siku zijazo na miaka ijayo. Amefunua mapenzi Yake kwa mwanadamu, na Yeye alilolifanya amefunua yote. Kama angetaka kusema kitu kingine, angekuwa amesema. Kwa kuwa alitoa tu kile tulicho nacho (Biblia), basi sisi lazima tuhitimishe kuwa hana neno zaidi la kutoa. Tena, wapo wale wanaodai kuwa Mungu amezungumza nao, lakini kwa kusudi gani? Ikiwa Yeye anatoa ujumbe ule ule kama uliofunuliwa katika

Biblia, kwa nini ahitaji kuzungumza na mtu mwingine moja kwa moja? Ikiwa anatoa ufunuo mpya, je, hangekuwa akionesha upendeleo kutoa ufunuo mpya kwa mtu mmoja na sio sisi wengine? Bila shaka hao ambao wanadai kwamba Mungu amezungumza nao watasema Mungu huyo kila wakati amewapa ujumbe, lakini wakati wote hawafuati maneno yaliyoandikwa yanasema nini. Hiyo inamaanisha kwamba Mungu atakuwa akipinga neno lake mwenyewe. Je! Tunaweza kuamini hivyo? Kamwe! Kwa hivyo lazima tuhitimishe kuwa Mungu hasemi na mwanadamu leo mbali na neno lake. Ikiwa tunataka kujua mapenzi ya Mungu lazima tuiendee Biblia. Kwa mtu kudai kwamba Mungu anafanya ufunuo maalum kwake inamaanisha kuwa mtu kama huyo amedanganywa, *"Lakini ijapokuwa sisi au malaika wa mbinguni atawahubiri ninyi injili yoyote isipokuwa hiyo tuliyowahubiri, na alaaniwe."* (Wagalatia 1: 8).

Nne, siku moja tutahukumiwa na neno la Bwana.Neno gani hilo? Ni kweli inayopatikana katika Biblia. Tunachosema ni kwamba kutakuwa na sheria ambayo tutahukumiwa nayo katika siku hiyo ya hukumu. Hatutaishi kwa sheria moja na kuhukumiwa na sheria nyingine. Anachohitaji katika neno lililoandikwa, atahitaji katika hukumu *"Yeye anikataaye mimi, asiyeyakubali maneno yangu, anaye amhukumuye; neno hilo nililolinena ndilo litakalomhukumu siku ya mwisho."* (Yohana 12:48). Hataibadilisha ili tu itufae. Hii ndio sababu inatupasa tuwe waangalifu sana kufanya tu yale aliyoyaamuru. Kukataa mafundisho Yake yoyote sasa inamaanisha kwamba atatukataa siku hiyo tutakaposimama mbele zake. Ikiwa tunaamini neno, kulitii, na kuishi kulingana nalo, basi hakika tutakubalika siku hiyo.

Rafiki yangu, natumai una Biblia, lakini ikiwa huna, wacha nikuhimize ujitahidi sana kupata moja. Wewe uwe na haja ya kuisoma na kujifunza, ili kujua mapenzi ya Mungu. Soma Mathayo, Marko, Luka na Yohana ili kujenga imani moyoni mwako kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu. Soma kitabu cha Matendo ili upate kujua ni nini unahitaji kufanya ili uokolewe; Hiyo ni: kumwamini Kristo, kutubu kwako dhambi, kumkiri Kristo kama Mwana wa Mungu, na kubatizwa kwa ajili ya ondoleo la dhambi zako. Soma hapo pia juu ya uanzishwaji

wa kanisa la Bwana na jinsi ambavyo mtu anapomtii Bwana, Kristo anamwongeza katika kanisa mtu huyo anayetubu, na mtiifu.

Ili kujifunza jinsi ya kuishi maisha ya Kikristo na kuwa na tumaini la uzima wa milele, endelea kusoma katika Agano Jipya.

## Somo la 3

# UNAHITAJI KUOKOKA

Tutaendelea na mfululizo wetu wa masomo juu ya Jinsi ya Kuanzisha Kanisa la Kristo Mhali Ulipo. Ikiwa wewe ni Mkristo, na upo karibu na kusanyiko la kanisa la Bwana, tunakuhimiza kuabudu huko. Lakini ikiwa uko mbali sana, basi tunakusihi uanzishe kusanyiko mahali unapoishi.

Kwa kuzingatia mawazo haya, msisitizo wetu kwa wakati huu kuwa kwenye mada, **Unahitaji Kuokoka**.

Ikiwa tayari umeokoka, basi siongei na wewe; isipokuwa kama unadhani wewe ni Mkristo lakini kiukweli wewe sio. Kuna watu wengi kama hao. Wamefundishwa kwamba Kristo ni Mwana wa Mungu, wameamini hivyo, na kisha wanaambiwa kwamba kwa sababu ya imani yao katika Kristo wameokolewa. Wengine wameambiwa mambo mengine ambayo yanaonesha kwamba wao wamekubalika kwa Bwana. Katika somo hili tunatarajia kukuonesha kutoka kwenye Biblia yenyewe kile mtu anachopaswa kufanya ili kupata wokovu. Mara tu unapojifunza hilo, unaweza kulinganisha kile ulichofanya na mapenzi ya Bwana kuona ikiwa umeokoka au la. Ikiwa unafikiria tu wewe ni Mkristo, lakini kwa kweli wewe sio, basi nakuhimiza kuwa mwaminifu wa kutosha kwako mwenyewe na kwa Mungu kuchukua hatua juu ya ukweli ambao unajifunza, ili uweze kuokolewa.

Watu wote wamezaliwa katika ulimwengu huu bila dhambi. Kwa miaka kadhaa ya kwanza katika maisha yao hawawajibiki kwa matendo yao. Hata sheria za nchi yetu hazitawaadhibu watoto makosa yao katika kipindi hiki cha utoto cha maisha yao. Lakini wanapofikia umri wa kujua mema na mabaya, mbele za Mungu, wao huwa wenye dhambi. Dhambi hufafanuliwa kama "kukosa alama" au "Kuvunja sheria" (1 Yohana 3: 4). Mara tu mtu anapokuwa mwenye dhambi anakuwa amepotea na anahitaji kuokolewa au kusamehewa dhambi zake. Lazima ijulikane kuwa wema au haki anayojitafutia mtu haviwezi kumwokoa (Waefeso 2: 8,9). Kama ilivyotajwa tayari, hata watu wa dini wanaweza kupotea. Kristo alisema kuwa haitoshi kumwita Bwana,

jina la Bwana, kufanya matendo makuu kwa jina la Bwana, n.k., lakini badala yake ili mtu aokoke lazima afanye mapenzi ya Baba aliye mbinguni (Mathayo 7: 21-23). Mwishowe, ingawa mtu anamtii Bwana na amesamehewa dhambi zake, ili aendelee kuokolewa lazima awe mwaminifu (Ufunuo 2:10). Kwa maneno mengine, inawezekana mtu kuanguka au kurudi katika dhambi, na kwa kufanya hivyo amepotea tena katika dhambi.

Bila kukujua binafsi, siwezi kujua kama wewe ni mtoto wa Mungu au ikiwa unahitaji kuokoka, lakini nadhani tunaweza kukusaidia kuona hali yako halisi ni ipi kwa wakati huu.

Kwa mfano, ikiwa huamini kwamba Yesu Kristo ndiye Mwana wa Mungu, hujaokoka. Kristo mwenyewe alisema, *"Amwaminiye yeye hahukumiwi; asiyeamini amekwisha kuhukumiwa; kwa sababu hakuliamini jina la Mwana pekee wa Mungu."* (Yohana 3:18). Alisema pia, *"Kwa hiyo naliwaambieni ya kwamba mtakufa katika dhambi zenu; kwa sababu msiposadiki ya kuwa mimi ndiye, mtakufa katika dhambi zenu."* (Yohana 8:24). Ingawa imani haiwezi tu kuokoa, bado mtu hawezi kuwa mali ya Bwana ikiwa haamini kwamba Kristo ni Mwana wa Mungu. Hoja ni kwamba, mtu anapotaka kuwa mwumini wa Kristo, lazima kutii mapenzi ya Bwana ili kuokolewa.

Ifuatayo, mtu anaweza kuamini kwamba Kristo ni Mwana wa Mungu, lakini ikiwa hajatubu dhambi zake, ikiwa hajakiri kwa kinywa kwamba Kristo ni Mwana wa Mungu, na ikiwa mtu hajawahi kubatizwa, basi hajaokoka. Kristo alisema kwamba lazima mtu atubu la sivyo ataangamia. Hiyo ni kwamba, mtu lazima aache dhambi zake ili awe ameokoka (Luka 13: 3). Katika tukio moja Kristo alisema kwamba lazima tumkiri Yeye mbele za Baba aliye mbinguni (Mathayo 10:32), na Paulo alisema, *"Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki; na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu "* (Warumi10:10). Ndipo Kristo akasema, *"aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa"* (Marko 16:16). Sasa hii yote inamaanisha nini? Inamaanisha kwamba ikiwa mtu anataka kuokolewa kutoka dhambini, lazima aamini kwamba Kristo ni Mwana wa Mungu, lazima atubu au aache njia yake ya dhambi katika maisha, lazima amkiri Kristo kuwa ni

Mwana wa Mungu, na lazima kubatizwa au kuzikwa majini ili kupata msamaha wa dhambi zake. Kama mtu hajafanya hivi, bado amepotea.

Sio tu hayo yaliyotajwa hapo juu yaliyo kweli, lakini ikiwa mtu sio mshirika wa kanisa ambalo ni la Kristo, mtu huyo hajaokolewa. Mtu anaweza kuwa mshirika wa idadi yoyote ya makanisa, lakini bado asiwe mshirika wa haki. Kwa kweli wapo wanaotetea kwamba sio lazima kuwa mshirika wa kanisa lolote ili kwenda mbinguni. Ni kweli kwamba mtu anaweza kuokolewa na kwenda mbinguni bila kuwa mshirika wa madhehebu yoyote au kanisa lililoundwa na wanadamu, lakini mtu hawezi kuokolewa bila kuwa mshirika wa kanisa la Kristo. “Lakini je! Kanisa la Kristo sio kama madhehebu mengine tu?" Unaweza kuuliza hivyo. Jibu ni HAPANA. Kanisa sio mkombozi, Kristo anawaongeza katika kanisa wale wanaookolewa. Siku ya Pentekoste, baada ya Injili kuhubiriwa watu elfu tatu walimtii Bwana, rekodi inasema, *“Nao waliolipokea neno lake wakabatizwa; na siku ile wakaongezeka watu wapata elfu tatu”* (Matendo2:41). Tena tunasoma, *“...Bwana akalizidisha kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa.”* (Matendo 2:47).

Kutoka katika taarifa hizi tunahitimisha kuwa ikiwa mtu sio mshirika wa kanisa la Bwana hajaokolewa, kwani Kristo anawongeza kanisani wanaookolewa. Kwa maneno mengine, ikiwa mtu hajaongezwa kwenye kanisa ni kwa sababu hajaokoka. Tunasoma katika Waefeso 5:23 kwamba Kristo ndiye Mwokozi wa mwili au kanisa. Je! Kristo ana makanisa mangapi? Moja tu, kulingana na Waefeso 4: 4, naye ndiye Mwokozi wake.

Kuna ushahidi mwingine wa kuzingatia kuhusu wokovu wa mtu kama vile: ibada, kuishi Maisha ya Kikristo, kuvaa jina la Bwana, nk, lakini kwa hakika, mtu ni lazima aamini kwamba Kristo ni Mwana wa Mungu, atii amri ya Injili, na kuwa mshirika wa kanisa la Bwana ili aokolewe. Sasa nataka kukuuliza maswali yafuatayo: Je! Unaamini kuwa Kristo ni Mwana wa Mungu? Je! ulitii Injili ya Kristo? Je! Wewe ni mshirika wa kanisa la Kristo? Ikiwa unasema hapana katika moja au zaidi ya maswali haya, wewe hujaokoka. Ikiwa unaweza kusema kwa uaminifu kwamba umeokoka, basi lazima uweze kujibu NDIYO katika maswali hayo matatu.

Ikiwa wewe si mtoto wa Mungu, ninataka kukuhimiza umtii Bwana ili uweze kuokoka. Kumbuka, huwezi kujiokoa na wala huwezi kuokolewa kwa kufuata mafundisho ya wanadamu. Njia pekee unayoweza kupata wokovu ni kwa kufanya kile ambacho Bwana anataka ufanye. Hakuwezi kuwa na mbadala wa imani na utii. Na usijali kuhusu "kujiunga" na kanisa. Huwezi kujiunga na kanisa la Kristo. Mara tu unapomtii Bwana, na kuokolewa, Yeye binafsi anakuongeza kwenye kanisa Lake.

Kuhusu kutii amri za Bwana, wewe ni mshirika wa kanisa ambalo Kristo alisema atalijenga (Mathayo 16:18). Kanisa hilo zima linaundwa na makusanyiko mengi ya mahali, popote washirika wake wanapopatikana. Ikiwa kuna washirika wawili au watatu mahali ulipo, au labda zaidi, unapaswa kuwajulisha kwamba umemtii Bwana na kwamba unataka kuwa na ushirika nao. Labda tayari wanajua hili, lakini ikiwa hawajui utii wako, lazima uwajulishe. Unapokuwa mahali ambapo kanisa la Kristo halipo, itakuwa juu yako kufanya juhudi kuwafundisha walio karibu na wewe, ukiwa na matumaini kwamba wengine watamtii Mungu. Tafadhali husikubaliane na kujiunga na kikundi cha kidini ambacho tayari kipo mahali ulipo, lakini badala yake fanya bidii kuanzisha kanisa kulingana na mafundisho ya Agano Jipya.

## Somo la 4

# JINSI YA KUITII INJILI

Katika somo hili tutajifunza jinsi ya kuitii injili. Hivi unajua injili ni nini? Watu wengi hawajui. Ni jinsi gani basi wanaweza kuitii injili ikiwa hawajui injili ni nini? Hawawezi, na ndiyo maana tunatumia muda katika kujadili kuhusu injili na jinsi ya kuitii.

Kwanza, hebu tufikirie injili ni nini. Hili ni neno ambalo tunalitumia wakati wote, lakini kuna faida gani kuzungumza juu ya "injili",kama hatujui maana yake? Neno injili limefafanuliwa kama habari njema. Mtume Paulo alisema, *"Tena wahubirije, wasipopelekwa? Kama ilivyoandikwa, Ni mizuri kama nini miguu yao wahubirio habari ya mema."* ( Warumi 10:15). Kwa nini injili ni habari njema? Ni habari njema kwa sababu ni ukweli kuhusu kufa, kuzikwa, na kufufuka kwa Yesu Kristo.

Paulo aliwaandikia Wakristo wa Korintho, *"Basi, ndugu zangu, nawaarifu ile injili niliyowahubiri; ambayo ndiyo mliyoipokea, na katika hiyo mnasimama, na kwa hiyo mnaokolewa; ikiwa mnayashika sana maneno niliyowahubiri isipokuwa mliamini bure. Kwa maana naliwatolea ninyi hapo mwanzo yale niliyoyapokea mimi mwenyewe, ya kuwa Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, kama yanenavyo maandiko; na ya kuwa alizikwa; na ya kuwa alifufuka siku ya tatu, kama yanenavyo maandiko;"* (1 Wakorintho 15:1-4).

Je, kufa, kuzikwa na kufufuka kwa Kristo kungewezaje kuwa habari njema? Ni habari njema kwa sababu Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, alikufa ili tupate kuokolewa, na tuwe na tumaini la maisha ya milele. Lakini si kwamba kufa tu ndio ulikuwa mwisho wake. Tunaweza kuokolewa kutoka katika dhambi zetu kwa sababu alifufuka kutoka kaburini ili kuthibitisha kuwa alikuwa Mwana wa Mungu na kwamba alikuwa na uwezo wa kumwokoa mwanadamu. Paulo pia alisema, *"Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu tulipokuwa tungali wenye dhambi."* (Warumi 5:8). Ndipo Petro akasema, *"Yeye mwenyewe alizichukua dhamb izetu katika mwili wake juu ya mti, tukiwa wafu kwa*

*mambo ya dhambi, tuwe hai kwa mambo ya haki; na kwa kupigwa kwake mliponywa"* (1 Petro 2:24).

Kuna maandiko mengine mengi yanayozungumzia kufa, kuzikwa, na kufufuka kwa Bwana, lakini hiyo inawezaje kuniokoa mimi na wewe? Kwanza, ni lazima tuamini kwamba Kristo ni Mwana wa Mungu na kwamba Yeye alikufa, akazikwa, na kwamba alifufuka kutoka kaburini. Tusipoamini hivyo hatuwezi kuokolewa. Kristo mwenyewe alisema*,"Kwa hiyo naliwaambieni ya kwamba mtakufa katika dhambi zenu; kwa sababu msiposadiki ya kuwa mimi ndiye, mtakufa katika dhambi zenu."* (Yohana 8:24).

Lakini tunaweza kuamini ukweli huu katika maisha yetu yote na bado tukapotea, kwa sababu haitoshi kuamini tu. Hatupaswi tu kuiamini injili, bali lazima tuitii. Jinsi gani mtu anaweza kuitii injili? Tunapoendelea kusoma maandiko tunaambiwa kuwa kuna amri za injili. **Kwanza, lazima tusikie**. Hiyo ndio sababu Kristo aliwaamuru wanafunzi wake kwenda ulimwenguni pote na kuhubiri Injili kwa kila kiumbe (Marko 16:15). Paulo alisema kuwa imani huja kwa kusikia neno la Mungu (Warumi 10:17). Na bila shaka ndicho tunachofanya sasa. Tunasoma neno la Mungu, tunasikia injili ili tupate kuijua. Kisha, lazima tuiamini injili. Kristo alisema, *"Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini, atahukumiwa."* (Marko 16:16). Mwandishi wa kitabu cha Waebrania anasema kwamba pasipo imani haiwezekani kumpendeza Mungu (Waebrania 11:6).

Kisha inakuja **amri ya toba**. Hiyo ina maana kwamba ni lazima mtu aache kufanya mabaya. Kama mtu anataka kuokoka lazima awe tayari kutubu. Kristo alisema kwamba tunapaswa kutubu la sivyo tutaangamia (Luka 13:3). Paulo alitangaza kwamba Mungu ameamuru watu wote wa kila mahali watubu (Matendo 17:30). Petro aliliambia kundi kubwa la watu kwamba wanapaswa kutubu na kubatizwa kwa ajili ya ondoleo la dhambi zao (Matendo 2:38). Baada ya toba huja **ukiri**, yaani, mtu lazima akiri kwa kinywa kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu. Mungu anataka mtu aweke kumbukumbu kwamba ana amini Kristo kuwa ni Mwana wa Mungu. Ikiwa anamwonea Bwana aibu, au anakataa kumkiri, basi hawezi kuokolewa. Kristo alisema kwamba ikiwa tutamkiri mbele ya watu, atatukiri mbele za Baba aliye

mbinguni (Mathayo10:32). Paulo alisema kwamba lazima tukiri hata kupata wokovu (Warumi10:10). Filipo alimtaka mtu kutoka Kushi (Ethiopia) akiri kwamba Kristo ni Mwana wa Mungu kama alitaka kubatizwa (Matendo 8:37).

Na hatimaye, **mtu lazima abatizwe**, **au kuzikwa katika maji**, ili dhambi zake zioshwe. Kristo alisema, *"Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini, atahukumiwa."* ( Marko 16:16 ). Petro alihubiri toba na ubatizo kwa ondoleo la dhambi (Matendo 2:38). Kuna vifungu vingine vingi vya maandiko vinavyotuambia kwamba ubatizo unamweka mtu ndani ya Kristo (Warumi 6:3,4), na ndani ya kanisa (1 Wakorintho 12:13). Ni nini kinachowezesha kuzaliwa upya kama inavyotajwa katika Yohana 3:3-5?

Lakini zaidi ya yote, ubatizo unafananishwa na kifo, na mazishi, na ufufuo wa Yesu Kristo. Kristo alikufa msalabani, na mwenye dhambi huzifia dhambi zake; Kristo alizikwa kaburini, na mwenye dhambi huzikwa ndani ya maji; Kristo alifufuka, na mtu anafufuka kutoka kwenye kaburi la maji ili kuenenda katika upya wa uzima (Warumi 6:1-12). Je! Hivyo si vizuri? Kisha Paulo anaeleza, *"Kwa maana ikiwa kwa kukosa mtu mmoja mauti ilitawala kwa sababu ya yule mmoja, zaidi sana wao wapokeao wingi wa neema, na kile kipawa cha haki, watatawala katika uzima kwa yule mmoja, Yesu Kristo. Basi tena, kama kwa kosa moja watu wote walihukumiwa adhabu, kadhalika kwa tendo moja la haki watu wote walihesabiwa haki yenye uzima."* (Warumi 5:17,18). Fundisho hilo linarejelea kifo, mazishi, na ufufuo wa Kristo; utii wa injili, unamrejelea mwenye dhambi kama amezifia dhambi zake, anazikwa katika maji ya ubatizo, kisha anakuja juu kutoka katika kaburi lile la maji ambalo linaelezewa kuwa ufufuo.Kabla ya hili, mtu alikuwa mtumwa wa dhambi, lakini baada ya kukamilika matendo haya ya utii, mtu anabadika kuwa ni mtumwa wa haki.Kwa hiyo, mtu akimtii Bwana anatangaza imani yake katika kifo, mazishi, na ufufuo wa Kristo. Hilo linafanyika kwa kutii injili.

Kwa sababu mtu anaweza kutii injili, Paulo alisema kwamba Bwana atarudi siku moja kulipiza kisasi kwa wasiomjua Mungu na wasioitii injili (2 Wathesalonike 1:7-9). Petro alitangaza, *"Kwa maana wakati umefika wa hukumu kuanza katika nyumba ya Mungu; na*

*ikianza kwetu sisi, mwisho wao wasioitii injili ya Mungu utakuwaje?"* ( 1 Petro 4:17 ). Ni dhahiri kwamba ni lazima mtu kuitii injili ili aokolewe na kwenda mbinguni, kwa kuwa waandishi hawa wanasema kwamba Bwana atarudi ili alipize kisasi kwa wale wasioitii Injili, na ikiwa mwenye haki ataokolewa kwa shida, mtu anaweza kutarajia nini ikiwa hata hafanyi jitihada za kumtii Bwana?

Lakini kwa mara nyingine tena, mtu anaitii injili kwa namna gani? Maandiko yanafundisha kwamba mtu lazima ajifunze neno la Mungu ili kujua ukweli. Kuhusu **kusikia** mapenzi ya Mungu, kuja kumjua Kristo, lazima **tuamini** kwamba Yeye ni Mwana wa Mungu, na kwamba ana uwezo wa kutuokoa katika ulimwengu huu na katika ulimwengu ujao. Kisha, lazima **tutubu** au tugeuke mbali na dhambi zetu zote. Hiyo ina maana kwamba ni lazima tuache tabia zetu mbaya na kuacha kufanya mambo ambayo ni makosa. Kwa maneno mengine ni kwamba, mtu hawezi kutubu dhambi zake na kuendelea kwa makusudi kufanya mambo yanayopinga mapenzi ya Mungu. Baada ya toba, mtu lazima **akiri** kwa kinywa chake, kutoka moyoni mwake, kwamba yeye anaamini kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu. Hakika mtu hawezi kumtarajia Kristo kumuokoa kama hamwamini vya kutosha na kuikiri hiyo imani kwa wengine. Na hatimaye, lazima **abatizwe** au kuzikwa katika maji kwa ondoleo la dhambi zake. Mtu anapofanya hivi, Bwana atamwokoa na kumuongeza kwenye kanisa Lake. Je, si rahisi hivyo?

**Somo la 5**

# JINSI YA KULITAMBUA KANISA LA BWANA

Mada yetu ni **Jinsi ya Kuanzisha Kanisa la Kristo Mahali Ulipo**. Ikiwa unaishi karibu na kusanyiko la kanisa la Bwana ni vema. Lakini ikiwa unaishi katika eneo fulani ambapo kanisa halipo, linahitajika kuwepo. Au ikiwa wewe unapaswa kuhamia mahali ambapo, kanisa halipatikani litahitajika kuwepo. Unaweza kuwa mtu wa kulianzisha. Fikiri pamoja nami tunapofikiria mambo mengi ambayo yanaweza kusababisha haya.

Ili kusaidia kuelewa zaidi, tutafikiria wakati huu kuhusu jinsi ya kulitambua kanisa la Bwana. Ngoja niyaweke wazi mambo ya kanisa katika Biblia. Halipo tu lakini linaweza kutambuliwa wazi. Kuna alama za utambulisho ambazo zinalitofautisha na makundu mengine yote ya kidini. Kwa mfano, kama wewe ni mshirika wa kanisa fulani, au ukiona katika makanisa yaliyo karibu nawe, chukua hizo alama za utambulisho ambazo zinapatikana katika Biblia na ulinganishe na kanisa lako au la mtu mwingine yeyote na kuamua kama ni kanisa la Kristo au la kuiga.

Unaweza kutaka kujua ni tofauti gani inayoonekana kuhusu kanisa, kama wewe ni mshirika wa moja wapo au lingine. Unaweza kuona kwamba kanisa si muhimu, kwamba haliokoi, na kwamba mtu anaweza kwenda mbinguni bila kuwa mshirika wa kanisa lolote. Wazo linaonekana kuwa zuri na la busara, lakini sivyo. Kwa nini Bwana amejenga kanisa, hata akatoa uhai wake kwa ajili yetu, kama kanisa siyo muhimu, au ikiwa kama makanisa yote ni sawa? Kweli kanisa siyo mwokozi kwa sababu kanisa linaundwa na watu waliookoka lakini kwa kuwa Kristo ni mwokozi  wa kanisa, hiyo ina maana mtu lazima awe mshirika wa kanisa ambalo Kristo ni mwokozi wake kwa utaratibu uliowekwa ili kwenda mbinguni.

Hebu twende moja kwa moja kwenye Biblia yenyewe na tuchunguze baadhi ya hizo alama za utambulisho wa kanisa. Zitakuwa nyingi kama utakavyoona.

Manabii wa Mungu zamani za kale walinena juu ya siku ile ambayo Bwana angesimamisha ufalme wake au kanisa. Isaya alisema "*Na itakuwa katika siku za mwisho, mlima wa nyumba ya Bwana utawekwa imara juu ya milima, nao utainuliwa juu ya vilima; na mataifa yote watauendea makundi makundi. Na mataifa mengi watakwenda na kusema, Njoni, twende juu mlimani kwa Bwana, nyumbani kwa Mungu wa Yakobo, naye atatufundisha njia zake, nasi tutakwenda katika mapito yake maana katika Sayuni itatoka sheria, na neno la Bwana katika Yerusalemu.*" (Isaya 2:2,3). Yoeli alisema maneno haya; *"Hata itakuwa, baada ya hayo, ya kwamba nitamimina roho yangu juu ya wote wenye mwili; na wana wenu, waume kwa wake, watatabiri, wazee wenu wataota ndoto, na vijana wenu wataona maono; tena juu ya watumishi wenu, wanaume kwa wanawake, katika siku zile, nitamimina roho yangu."* (Yoeli 2:28,29).

Kisha Daniel akaongezea *"Na katika siku za wafalme hao Mungu wa mbinguni atausimamisha ufalme ambao hautaangamizwa milele, wala watu wengine hawataachiwa enzi yake; bali utavunja falme hizi zote vipande vipande na kuziharibu, nao utasimama milele na milele."* (Danieli 2:44).

Sasa hawa manabii wa Mungu walikuwa wanasema nini? Walikuwa wanaelezea wakati ambapo ufalme wa kiroho wa Bwana au kanisa ungeanzishwa kanisa lingejengwa Yerusalemu na kutoka hapo neno la Bwana lingeenea katika ulimwengu wote, lingekuja kwa nguvu za Roho na lisingeangamizwa kamwe, lakini lingesimama milele hili lilitimizwa Yerusalimu (Matendo 2) wakati kanisa lilipoanzishwa kwa njia ya uongozi wa Roho Mtakatifu, na kutoka hapo injili ikapelekwa duniani kote. Siku hiyo kanisa lilijengwa na limekuwepo tangu wakati huo hadi sasa na litasimama milele.

Yesu alisema kwamba atalijenga kanisa lake (Mathayo 16:18). Na alifanya hivyo kwa msaada wa mitume. Alikuwa ameahidi kutuma Msaidizi, au Roho Mtakatifu juu yao ili awaongoze katika kweli yote (Yohana 16:13). Muda mfupi kabla hajarudi kwa Baba mbinguni,

akawaambia *“Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi.”* (Matendo 1:8). Na hivyo ikawa.

Tunasoma katika Matendo 2 kwamba kanisa lilianzishwa mjini Yerusalemu. Kama ilivyoelezwa hapo awali, manabii wa Mungu walilitaja jina la mji wa Yerusalem ambapo ufalme wa Bwana, au kanisa lingeanzishwa. Lilisemekana kwamba neno la Bwana lingetoka katika mji huo. Kristo aliwaambia mitume wake, *“ Akawaambia, Ndivyo ilivyoandikwa, kwamba Kristo atateswa na kufufuka siku ya tatu; na kwamba mataifa yote watahubiriwa kwa jina lake habari ya toba na ondoleo la dhambi, kuanza tangu Yerusalemu. Nanyi ndinyi mashahidi wa mambo haya.”* (Luka 24:46-48). Baada ya Petro na mitume kufanya hivyo wakahubiri kwa umati mkubwa wa watu huko Yerusalemu, nao walitaka kujua nini walichopaswa kufanya, Petro alisema, (Matendo 2:38). Takribani watu elfu tatu walitii na Bwana aliongeza waliokolewa katika kanisa lake (Matendo 2:47).

Pia tunasoma katika Matendo 2 kwamba injili ilihubiriwa kwanza na kanisa la Bwana wetu lilianzishwa siku ya Pentekoste ya kwanza baada ya ufufuo wa Yesu Kristo. Pentekoste ilikuja siku ya kwanza ya juma na hii ilifanyika mwaka wa 33 BK.

Mitume walipokea nguvu za Roho Mtakatifu ili kuwaongoza na katika Kweli yote kwa kusudi la kuwawezesha kutenda miujija ya kusadikisha watu kwamba wao walikuwa ni mitume wa Mungu, na kunena kwa lugha ya watu waliokusanyika pale (Matendo 1:8 ; 2:1-4,9).

Kanisa liliundwa na waliookolewa, kwa kuwa kristo aliwaongeza katika kanisa (Matendo 2:41,47). Kwa hiyo lilikuwa la kiroho, mwili wa Kriso, na Kristo mwenyewe akiwa kichwa cha mwili. Akimzungumzia Kristo, Paulo alisema *“Naye ndiye kichwa cha mwili, yaani, cha kanisa; naye ni mwanzo, ni mzaliwa wa kwanza katika wafu, ili kwamba awe mtangulizi katika yote.”* (Wakolosai 1:18). Pia, soma Waefeso 1:22,23 na Waefeso 5:23.

Kanisa lilinunuliwa kwa damu ya Yesu Kristo. Paulo aliwaambia wazee wa kanisala Efeso, *“Jitunzeni nafsi zenu, na lile kundi lote nalo,*

*ambalo Roho Mtakatifu amewaweka ninyi kuwa waangalizi ndani yake, mpate kulilisha kanisa lake Mungu, alilolinunua kwa damu yake mwenyewe."* (Matendo 20:28). Kisha katika tukio lingine, aliwaambia waefeso kuhusu Kristo, "*Kwa maana mume ni kichwa cha mkewe, kama Kristo naye ni kichwa cha Kanisa; naye ni mwokozi wa mwili."* (Waefso 5:23). ikiwa Kristo alikufa kwa ajili ya kanisa, naye ni mwokokozi wake, hiyo ina maana kwamba lilikuwa na umuhimu mkubwa kwa Kristo.

Kristo anatajwa kuwa msingi wa kanisa. Baada ya Petro na mitume kumkiri kuwa ni Mwana wa Mungu, Kriso alijibu kwa kusema kwamba angelijenga kanisa lake juu ya ukweli huo au mwamba huo, mwamba akiwa yeye mwenyewe (Kristo), (Mathayo 16:18). Paulo alisema, *"Maana msingi mwingine hakuna mtu awezaye kuuweka, isipokuwa ni ule uliokwisha kuwekwa, yaani, Yesu Kristo."* (1 Wakorintho 3:11). Petro alizungumza juu ya Kristo kuwa jiwe kuu la pembeni (1 Petro 2:1-8).

Kanisa na washirika wake huvaa jina la Bwana. Wokovu hauko katika jina linguine (Matendo 4:12). Akizungumzia makusanyiko yanayounda kanisa, wanaitwa makanisa ya Kristo (Warumi 16:16). Kanisa pia linasemwa kama kanisa la Mungu (Matendo 20:28), na majina mengine ya maelezo hayo, yanayomheshimu Bwana. washirika wake wanaitwa Wakristo (Matenzo 11:26; 26:28;1 Petro 4:16).

Masharti ya kuingia yameelezwa tena na tena katika kitabu cha Matendo, tunaposoma matukio mbalimbali ya uongofu, kwa kusikia injili, watu walimwamini Mungu na Kristo, walitubu dhambi zao walimkiri Kristo kama Mwana wa Mungu, na kubatizwa kwa ajili ya ondoleo la dhambi zao (Matendo 2:38; 2:47).

Kama Wakristo, walimwabudu Bwana, wakiwa waaminifu kwake walikuwa na ahadi ya kwamba Kristo atarudi siku moja kwa ajili ya kanisa (Waefeso 5:27;1 Wathesalonike 4:15-18).

Kwa hiyo kanisa limetambulishwa waziwazi katika maandiko. Sasa jinsi gani unaweza kulipata kanisa la Bwana leo? Kwa kutumia hizi alama hizihizi utambulisho kanisa linaweza kudai kuwa ni la Bwana, lakini ikiwa halina alama hizi, sivyo. Ikiwa halipo kusanyiko la kanisa

mahali ulipo, unaweza kuanzisha moja kwa kufundisha neno la Mungu, kuwaongoa wengine, na kuendelea kutoka hapo.

## Somo la 6

# WEWE NI MUHIMU KWA BWANA

Kusudi letu katika somo hili litakuwa kujadili tena **Jinsi ya Kuanzisha Kanisa la Kristo Mahali Ulipo**, tunaamini kwamba ikiwa tunaweza kuondoa hali ya kutokuelewana inayolizunguka kanisa kila kitu kitaangukia mahali pake. Hatutaki kusisitiza juu ya kanisa, lakini wakati huo huo tunataka kuliona kama kanisa ambalo Biblia inalionesha. Vivyo hivyo, ikiwa upo katika eneo ambalo kanisa la Bwana linapatikana, na ikiwa wewe ni mshirika wa kanisa au ikiwa unapenda kuwa mshirika wake, tungependa kukuhimiza ili uwe mtu muhmu katika kuanzisha kanisa hapo ulipo.

Katika somo hili hasa tunataka kusisitiza kwamba wewe ni muhimu kwa Bwana.

Mungu alimwumba mwanadamu. Alimfanya kwa mfano wake (Mwanzo 1:26,27; 2:7). Yaani alimpa roho, nafsi, kile ambacho hakitakufa kamwe (Mathayo 16:26). Alimpenda sana hata alikuwa tayari kumtoa mwanawe afe juu ya msalaba wa kikatili ili kumwokoa mwanadamu kutokana na dhambi zake (Yohana 15;13). Hii ina maana kwamba kila mtu ni muhimu sana. Kwa hiyo kumbe wewe ni muhimu.

Angalia mtu mmoja-mmoja katika Biblia ambao ni mashuhuri sana walikuwa watu wakuu kwa sababu walimruhusu Bwana kuwatumia. Fikiria kuhusu Nuhu, Ibrahimu, Musa, Danieli, Isaya, Eliya, Elisha, Yohana Mbatizaji, kila mmoja wa mitume na wengine wengi.

Fikiria, pia, juu ya Mtume Paulo na kile alichoweza kufanya kukitimiza kwa ajili ya Bwana katika maisha yake. Alianza kama adui wa Kristo na watu wake. Mara baada ya kuongoka, ata hivyo, alifanya kazi kwa bidii zaidi, kwa ajili ya Bwana na kueneza jambo lake kuliko alivyokuwa amefanya dhidi yake fikiria safari zake za kimisionari na watu wote alioweza kuwaongoa katika Kristo. Kwa sababu ya kazi yake, na ya waongofu wake, pamoja na mitume wengine na waongofu wao, ndani ya muda osiozidi miaka thelathini injili ilienea ulimwenguni kote. Watu wachache au hata mtu mmoja anaweza kukamilisha kiasi cha wema wakati shauku, kujitolea, na nia inapokuwepo.

Angalia umuhimu uliokuwa umeambatanishwa na mtu mmoja na familia yakekatika Matendo 10. Kornelio alikuwa (kamanda wa kikosi) katika jeshi la kirumi, lakini yeye alikuwa mtu mwema. Alikuwa mtu wa kidini, pia akiomba daima na kuwapa masikini sadaka. Mungu alimtazama na kupendezwa, Mungu alimtuma Petro kwa Kornelio na familia yake kwa kusudi la kuwahubiria injili. Rekodi inasema *"Petro alipokuwa akisema maneno hayo Roho Mtakatifu akawashukia wote waliolisikia lile neno. Na wale waliotahiriwa, walioamini, wakashangaa, watu wote waliokuja pamoja na Petro, kwa sababu Mataifa nao wamemwagiwa kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa maana waliwasikia wakisema kwa lugha, na kumwadhimisha Mungu. Ndipo Petro akajibu, Ni nani awezaye kuzuia maji, hawa wasibatizwe, watu waliopokea Roho Mtakatifu vile vile kama sisi? Akaamuru wabatizwe kwa Jina lake Yesu Kristo. Ndipo wakamsihi azidi kukaa siku kadha wa kadha."* (Matendo 10:44-48). Sababu moja ya msingi katika uongofu wa Kornelio na wale wa nyumbani mwake ni kwamba walikuwa watu wa mataifa na wakawa wongofu wa kwanza wa mataifa. Fikiria maana ya uongofu huu kwa ajili ya Kristo katika siku hiyo. Wakiwa waongofu wa kwanza wa mataifa, bila shaka majina yao yalisemwa mara nyingi kuanzia wakati huo na kuendelea kama mfano wa mataifa yote waliofuata nyayo zao. Hata leo Wakeisto wengi wanatoka katika malezi ya mataifa.

Sasa hebu turudi kwenye uongofu wa mtu kutoka Kushi (Ethiopia), ingawa Filipo alikuwa akifanya kazi huko Samaria na kupata mafanikio makubwa, bado rekodi inasema, *"Malaika wa Bwana akasema na Filipo, akamwambia, Ondoka ukaende upande wa kusini hata njia ile itelemkayo kutoka Yerusalemu kwenda Gaza; nayo ni jangwa. Naye akaondoka, akaenda; mara akamwona mtu wa Kushi, towashi, mwenye mamlaka chini ya Kandake malkia wa Kushi, aliyewekwa juu ya hazina yake yote; naye alikuwa amekwenda Yerusalemu kuabudu, akawa akirejea, ameketi garini mwake akisoma chuo cha nabii Isaya. Roho akamwambia Filipo, Sogea karibu na gari hili, ukashikamane nalo. Basi Filipo akaenda mbio, akamsikia anasoma chuo cha nabii Isaya; akanena, Je! Yamekuelea haya unayosoma? Akasema, Nitawezaje kuelewa, mtu asiponiongoza? Akamsihi Filipo apande na kuketi pamoja*

*naye. Na fungu la Maandiko alilokuwa akilisoma ni hili, Aliongozwa kwenda machinjoni kama kondoo, Na kama vile mwana-kondoo alivyo kimya mbele yake amkataye manyoya, Vivyo hivyo yeye naye hafunui kinywa chake. Katika kujidhili kwake hukumu yake iliondolewa. Ni nani atakayeeleza kizazi chake? Kwa maana uzima wake umeondolewa katika nchi. Yule towashi akamjibu Filipo, akasema, Nakuomba, nabii huyu; asema maneno haya kwa habari ya nani; ni habari zake mwenyewe au za mtu mwingine? Filipo akafunua kinywa chake, naye, akianza kwa andiko lilo hilo, akamhubiri habari njema za Yesu. Wakawa wakiendelea njiani, wakafika mahali penye maji; yule towashi akasema, Tazama, maji haya; ni nini kinachonizuia nisibatizwe? Filipo akasema, Ukiamini kwa moyo wako wote, inawezekana. Akajibu, akanena, Naamini ya kwamba Yesu Kristo ndiye Mwana wa Mungu.] Akaamuru lile gari lisimame; wakatelemka wote wawili majini, Filipo na yule towashi; naye akambatiza. Kisha, walipopanda kutoka majini, Roho wa Bwana akamnyakua Filipo, yule towashi asimwone tena; basi alikwenda zake akifurahi. Lakini Filipo akaonekana katika Azoto, na alipokuwa akipita akahubiri Injili katika miji yote, hata akafika Kaisaria.''* (Matendo 8:26-39).

Masomo mengi mazuri yanaweza kutolewa kutokana na somo hili la uongofu, lakini jambo ambalo tunasisitiza kwa wakati huu ni ukweli kwamba mtu huyu alikuwa muhimu kiasi kwamba malaika wa Bwana akawaleta pamoja Filipi na mkushi ili Filipo aweze kumfundisha ukweli kwa upande wake, ili mtu huyo aweze kumtii Bwana. Sasa mkushi alikuwa nani? Alikuwa mtu wa dini sana, akiwa amesafiri mbali kutoka Kushi (Ethiopia) hadi Yerusalemu kuabudu kulingana na dini ya Kiyahudi. Hii inaonesha kwamba alikuwa mtu mnyenyekevu mwaminifu na wa kujitolea. Pia alikuwa mtu mwenye mamlaka makubwa, akiwa mweka hazina wa malkia Kandake. Sasa kwa kutii ukweli na kurudi katika nchi yake, unadhani mtu huyu mmoja alikuwa na ushawishi kiasi gani kwa viongozi na wananchi, wanafamilia wake na watu kwa ujumla? Tunapaswa kuhitimisha kwamba Mungu aliona ndani yake uwezo mkubwa wa kueneza jambo lake, na sidhani kama Mkushi huyu alimvunja moyo Bwana.

Sasa, wewe ni nani? Labda unafikiri wewe si mtu wa maana wakati unaweza kuonekana kuwa si muhimu sana ukiwa katika hali ya upweke, ikiwa utamtii Bwana na kujitoa kwake anaweza kukufanya uwe mtu muhimu unaweza kuwa kijana, mzee, mwanamke, mtu tajiri, maskini, asiye na elimu au chochote kile. Unaweza kusimamia mambo haya kama visingizio, ukisema kwamba huwezi kamwe kuwa hivyo kwa ajili ya Bwana. Utakuwa unakosea. Angalia wanaume wa kawaida na wanawake katika Biblia jinsi alivyowachukua na kuwafanya watumishi wakuu, kwa nini hasiweze kufanya vivyo hivyo kwako?

Ninachosema ni hiki: ikiwa utamtii Bwana, na kuwa mshirika wa kanisa lake, na kama utajitoa kwake, yaani ukimfanyia kazi unaweza kuwa mhubiri, mwalimu, mmisionari au mtumishi mwingine katika nafasi nyingine, hilo litakuwezesha kumfanyia mengi katika kueneza neno lake. Tunaposisitiza katika masomo haya, ikiwa uko mahali ambapo kanisa halipo, unaweza kuongoza huko kwanza kazi ndiyo, unaweza kufanya hivyo. Bwana ameahidi kuwa nawe na kubariki juhudi zako. Tafadhali fikiria juu ya haya na ombi hili ili mapenzi ya Mungu yatimizwe katika maishayako.

## Somo la 7

## KWANINI KANISA LINAHITAJIKA MAHALI ULIPO?

Mtiririko huu mzima wa masomo unahusu swalila **Jinsi ya kuanzisha Kanisa la Kristo Mahali Ulipo**. Inawezekana ili uwe tayari kuwa mshirika wa kanisa la Bwana na mshirika wa kusanyiko fulani. Katika hali hiyo, tunafurahi. Walakini, ikiwa wewe bado sio Mkristo, na ikiwa hakuna kusanyiko la kanisa mahali ulipo, naomba kwanza upitie masomo haya upate kutiwa moyo na kumtii Bwana, ili upate kuokolewa na Mungu atakuongeza katika kanisa ambalo Kristo alilijenga. Inawezekana, hata kama, ikiwa hakuna kusanyiko la kanisa linakutana mahali unapoishi. Tunataka kukupa habari nzuri unayohitaji ili kukuwezesha kuanzisha kanisa katika jumuiya yako.

Kwanza, tunataka kukuambia kwa nini kanisa linahitajika mahali ulipo. Hatuzungumzii kanisa lingine au aina fulani ya madhehebu. Kwa kweli, inawezekana kuna madhehebu kadhaa katika sehemu unayoishi, lakini hatuzungumumzii makanisa yaliyotengenezwa na wanadamu. Badala yake, tunazungumza juu ya kanisa ambalo tunaweza kulisoma katika Biblia, kanisa ambalo ni la Bwana. Ni lile ambalo Kristo alikufa kwa ajili yake, ambaye ni Mwokozi wake na lile moja ambalo yeye ni Kichwa. Pia ndilo linalovaa jina lake.

Je! Ulijua kuwa unaweza kuwa mshirika wa madhehebu fulani katika kanisa na bado ukapotea? Wale walio katika makanisa yaliyoundwa na wanadamu watakubali kwamba unaweza kuokolewa bila kuwa mshirika wa lolote kati yao. Ndiyo maana kanisa la Bwana linahitajika kuwa katika jamii yako, kwa ajili yako na kwa ajili ya wengine ambao wanaweza kutaka kumtii Bwana.

Kanisa la Kristo ni muhimu, haimaanishi kuwa lenyewe ni mwokozi, lakini ili mtu aokolewe ni lazima awe sehemu yake. Kwa kweli, mtu anapookolewa, katika mchakato huo Bwana anamwongeza kwenye mwili wa watu waliookolewa ambao anauita kanisa lake (Matemdo 2:47). Lakini sikia maneno ya Mtume Paulo aliposema, *“Kwa maana mume ni kichwa cha mkewe, kama Kristo naye ni kichwa cha Kanisa; naye ni mwokozi wa mwili.”* (Waefeso 5:23). Tafadhali zingatia kwamba, Paulo anasema kuwa Kristo ni mwokozi wa mwili

wake. Lakini mwili ni nini? Kulingana na Waefeso 1:22,23 na Wakolosai 1:18, mwili ni kanisa. Kwa hiyo, Kristo ni mwokozi wa kanisa. Lakini kuna miili mingapi? Tena, Paulo anasema kwamba kuna mwili mmoja tu (Waefeso 4:4). Lakini ikiwa mwili ni kanisa na kuna mwili mmoja tu maana yake kuna kanisa moja tu. Inaleta maana kuwa mshirika wa kanisa la Kristo, na inaleta maana kwa kanisa kuwa mahali ulipo kwa vile hilo ni Kanisa, wewe na wengine mnapaswa kuwa washirika ili kumpendeza Mungu.

Sababu nyingine kwa nini kanisa linahitajika kuwa hapo ni kutoa huduma kwako na washirika wengine wowote wa kanisa kwenye kusanyiko ambalo kwalo mtaabudu. Ikiwa hakuna kusanyiko katika eneo lenu, unaweza kuwa dhaifu kiasi cha kuanza kuabudu pamoja na kundi la dini nyingine. Lakini hili siyo suluhisho la tatizo.

Acha nieleze kwa nini huwezi kuabudu pamoja na kanisa lingine. Ikiwa wewe ni mshirika wa kanisa la Kristo, hiyo inamaanisha wewe si mshirika wa kundi fulani la madhehebu. Kanisa la Bwana ni tofauti na wao kwa kuwa ni mali ya Bwana, huvaa jina la Kristo, na ibaada yake na mafundisho yake ni tofauti. Je! Unaweza kuabudu na kanisa ambalo si la Bwana? Huwezi kuimba nao kwa sababu wanatumia vyombo vya muziki, huku watu wa Bwana wakiimba bila vyombo (akapela). Paulo alisema kwamba sisi tunapaswa kuimba na kufanya muziki miyoni mwetu (Waefeso 5:19). Huwezi kuomba nao kwa sababu wao si watu waliookoka. Bwana ameahidi kuwasikia watu wake, lakini si mwenye dhambi (Yohana 9:31). Huwezi kujifunza nao kwa sababu wao wanaongozwa na taratibu na nidhamu au sheria za wanadamu. Hutaweza kuishiriki meza ya Bawna pamoja nao kwa sababu wao hawana meza ya Bwana kila siku ya kwanza ya juma [au hata wakishiriki, si halisi] (Matendo 20:7). Wala huwezi kuchangia pesa zako kwao kwa sababu zitatumika kuunga mkono mafundisho yao ya uwongo. Na wala huwezi kushirikiana nao kwa sababu huwezi kuwatia moyo waendelee na makosa yao. Hizi ndizo sababu zinazofanya usiweze kuabudu na kanisa lingine.

Tena ikiwa uko mahali ambapo kanisa halipo, hatari nyingine ni kwamba unaweza kuacha imani kabisa. Unaweza kusingizia kwamba kwa kuwa kanisa halipo, na huwezi kuabudu pamoja na makundi

mengine ya kidini, kwa nini ujisumbue nayo hata hivyo? Lakini hilo si suluhisho la tatizo lako. Badala yake, lazima utambue kwamba kuna kitu unachoweza kufanya ili kutatua tatizo.

Huenda umeishi nyumbani kwako maisha yako yote, ukisoma kozi ya Biblia au kusikia ijnili ikihubiriwa redioni na kisha ukamtii Bwana na kugundua kwamba wewe ni Mkristo pekee mahali ulipo. Au labda umehamia kwa sasa huko nyumbani uko mahali fulani ambapo kanisa lilikuwepo. Lakini bila kujali kwa jinsi ilivyotokea ukawa hapo mshukuru Mungu, hapo tafadhali acha hii iwe fursa kwako kuanzisha kanisa hapo ulipo. Lakini unaweza kusema, "mimi ni nani niweze kuanzisha kanisa la Bwana? "Bila shaka unaweza kupata visingizio vingi, lakini ukweli ni kwamba unaweza kufanya chochote kinachohitajika kufanywa ikiwa wewe utaamua kufanya hivyo.

Kanisa linahitajika kuwa katika eneo lako kwa sababu wewe upo na kwa sababu ya wengine wote huko wanaohitaji wokovu. Wewe na kanisa mnamwakilisha Kristo. Unawakilisha ukweli wa Mungu, kuwapa watu fursa ya kuchagua kati ya ukweli na uwongo. Kama kanisa halipo kwa ajili ya kusimamia ukweli, huenda watu wa eneo hilo hata hawajui mapenzi ya Mungu. Kanisa linawakilisha nuru na njia ya kwenda kwa Bwana. Bila hivyo kuna giza tu.

Kanisa linahitajika kuwa hapo si tu kumwabudu Mungu bali pia kuwa na bidii katika kuhubiri na kufundisha injili ya Kristo. Hili linaweza kufanywa katika ibada lakini pia linaweza kufanywa kupitia mikutano, kazi binafsi, fasihi (uandishi) n.k. Kuna njia nyingi sana za kutangaza mapenzi ya Mungu, lakini ni juu ya kanisa kuongoza.

Ni lazima kanisa liwe na ukubwa gani ili kufanya kazi hii? Maandiko yanasema wazi katika maneno ya Yesu, *"Kwa kuwa walipo wawili watatu wamekusanyika kwa jina langu, nami nipo papo hapo katikati yao."* (Mathayo 18:20). Hiyo inamaanisha kwamba unaweza kuanzisha kusanyiko na wewe mwenyewe na mshirika mwingine, na kisha unaweza kuendelea kukua maadam mnaongezeka idadi.

Kumbuka kwamba kanisa la Bwana linaundwa na waliookolewa, na watu wanapomtii Bwana, yeye huwaokoa, huwaongeza kwa wengine wote ambao wameokolewa katika kusanyiko la mahali hapo, huanza pamoja na washirika wawili au zaidi wanaokubaliana kwamba

watakutana kuabudu na kufanya kazi pamoja kwa ajili ya Bwana, na linakua kuanzia hapo.

Kanisa au kusanyiko la mahali pamoja, si nyumba ya kukutania au jengo la kanisa. Kwa kweli haijalishi mahali ambapo kanisa hukutana. Linaweza kuwa na jengo lake au linaweza likaanza kukutana nyumbani, katika nyumba ya kukodi, katika jengo la shule au mahali pengine popote. Jambo muhimu kuhusu kanisa la Bwana si mahali linapopatikana, bali ni nani wanaokutana.

Kanisa litajulikana kama kanisa la Kristo, au kwa maneno mengine litavaa jina la kimaandiko kama lilivyowekwa katika maandiko. Katika ibada yake, katika mafundisho yake, kazi yake na katika yote linayofanya, linatawaliwa na mambo yanayofundishwa katika neno la Mungu. Dhamira yake itakuwa kueneza kazi ya Kristo na kumheshimu Bwana.

Inafurahisha sana kuwa Mkristo na mshirika wa kanisa la Bwana ikiwa wewe ni mshirika wa kusanyiko kubwa lililo karibu nawe au unaishi mahali ambapo kanisa halijakuwepo, ukweli ni kwamba unaweza kuchukua nafasi muhimu katika kusaidia kanisa kukua au kuwa muhimu katika kuanzisha kusanyiko mahali ulipo.

## Somo la 8

# JINSI YA KUANZA KANISA LA BWANA

Mfululizo wetu wa masomo unazingatia mada ya jinsi ya kuanzisha kanisa la Kristo mahali ulipo, tukisisitiza juu la hitaji la kanisa kuwepo katika mji wako, kijiji au popote ulipo. Pia tunasisitiza ukweli kwamba ikiwa wewe ni Mkristo unaweza kushiriki katika kuanzisha kusanyiko la kanisa mahali ulipo, kama halipo mahali hapo.

Katika somo hili tunataka kuzungumza kuhusu jinsi ya kuanza kanisa la Bwana. Katika masomo yaliyopita tulijadili juu ya hitaji la wokovu,jinsi ya kumtii Bwana, jinsi ya kutambua kwa nini kanisa linahitajika mahali ulipo n.k. sasa tunataka kuonyesha jinsi unavyoweza kuanzisha kanisa mahali unapoishi.

Kabla hujaendelea mbele niseme tena kwamba tunazungumza kuhusu kuanzisha kanisa mahali ulipo, kwa msingi wa kwamba mahali ambapo halijaanza bado. Ikiwa lipo, unahitaji kushirikiana na kusanyika la mahali ulipo, si kusababisha mgawanyiko wa kujitenga. Lakini uwe na hakika kwamba kundi linalojiita kanisa la Kristo ni la kweli na si kanisa la kimadhehebu lililojificha,lichunguze sana. Tembelea na uangalie ibada yake. Inavaa jina gani? Katika masomo haya tunajaribu kulichunguza kanisa ili tutambue ikiwa ni mwili wa Bwana au sio. Mtu anaweza kuuliza, “lakini kuna tofauti gani?” kuna tofauti kati ya kuwa sahihi na kutokuwa sahihi. Bwana anajua anachotaka, na jambo atakalolipanga daima huwa sahihi. Kwa hiyo, kanisa lake ni sahihi na mengine yote si sahihi.

Katika baadhi ya miji tuna makusanyiko mengi sana,kwa maana ya kwamba kuna kuna wale wanaomtii Bwana, badala ya kuabudu pamoja na kusanyiko lililo karibu nao, wanaanza kazi katika nyumba zao au katika nyumba za kupanga. Wakati Fulani makusanyiko mawili au matatu huwa kwenye mtaa mmoja. Hivyo ni vibaya kwa sababu wakati mwingine husababisha mgawanyiko miongoni mwa ndugu na pia vibaya wakati kuna kuna makusanyiko mengi madogo yanayojitahidi kudumu, ambapo yangeweza kuungana na kusaidiana yakatiana moyo na kufanya kazi nzuri zaidi.

Kwa hivyo, hatuzungumzii juu ya kuanzisha kusanyiko mahali ambapo tayari kuna kusanyiko moja au zaidi karibu, bali tunahimiza kuanzisha kanisa la Bwana katika mji au eneo ambalo halipo. Labda unafikiria namna inavyowezekana kuanzisha kanisa la Kristo. Bila shaka hatuzunguumzii juu ya kuvumbua kanisa jipya, yaani kuanzisha kanisa jipya kwa mamlaka yetu n.k. Tunajua kwamba tayari Bwana analo kanisa lake alilolianzisha (Mathayo 16:18). Lilianzishwa zamani huko Yerusalemu injili ilipohubiriwa na mwanzoni watu elfu tatu walitii, wakaokolewa na Bwana akawa anawaongeza watu wanaozidi kuokolewa katika kanisa lake (Matendo 2). Baada ya hapo, mahali popote ambapo injili ilihubiriuwa na watu wengine wakatii, kusanyiko la kanisa la Bwana lilianzishwa. Tangu wakati huo,mahali popote lilipohubiriwa neno la Mungu na watu wakatii, kanisa lilianza mahali hapo. Ndivyo ilivyo hata leo na ndicho tunachomaanisha tunapozungumzia juu ya kuanza kanisa mahali unapoishi. Kanisa la Bwana linaweza kuwepo mahali maadam wewe na wengine mnamtii Bwana, ni rahisi tu.

Kwa hiyo hali yako ni hii: wewe ni Mkristo na unataka kumwabudu Bwana. Unataka kuwa mshirika wa kusanyiko la mahali ulipo lakini hakuna kanisa la Kristo katika mji wako, utafanyaje? Kwanza kabisa, mimi ningekushari kwamba, ingawa uko peke yako, utenge muda fulani kila siku ya Bwana (kila siku ya kwanza ya juma), ambayo ni Jumapili, wa kumwabudu Mungu; kusoma maandiko,kuomba na kuimba nyimbo za kiroho. Kwa kuwa Bwana anapenda watu wake wamkumbuke kila siku ya kwanza ya juma kwa kushiriki meza ya Bwana, unapaswa kuandaa mkate usiotiwa chachu na kupata maji ya zabibu na unapaswa kufuata muundo wa kimaandiko katika 1 Wakorintho 11:23-29 wa kushiriki mkate kwa ukumbusho wa mwili wa Kristo na mzao wa mzabibu kwa ukumbusho wa damu ya Kristo. Kisha unapaswa kuweka akiba sehemu ya kipato chako ili itumike katika kazi ya Bwana labda kununua Biblia ili kujifunza na wengine, kununua vifaa kwa ajili ya meza ya Bwana, kuwa na fedha za kusaidia wahitaji n.k. Hata ingawa upo wewe pekee, bado itakutia moyo na nguvu ya kuendelea hadi pale wengine watakapoongezeka.

Baada ya hapo kama ningekuwa wewe ningejaribu kuwashawishi wanafamilia wangu na marafiki kukusanyika pamoja nami katika ibada. Wakati huo huo ningekuwa nawaza juu ya watu binafsi, wanaume au wanawake au vijana ambao ningeweza kuzungumza na kujifunza nao maandiko kwa kusudi la kuwaongoa na kuwaleta kwenye ukweli. Ningekuwa mpole kwao, ningechukua muda pamoja nao, lakini ningejaribu kuwaonesha kile ambacho mtu lazima akifanye ili aokolewe na kisha ningewaonesha kile ambacho Biblia inafundisha kuhusu kanisa la Bwana. Labda kwa muda huo mtu mmoja au zaidi angeamua kumtii Mungu. Ungewaeleza juu ya kumwamini Bwana na kutubu dhambi zao, jambo wanalopaswa kufanya ni kumkiri Kristo kwamba ni Mwana wa Mungu. Unaweza kwenda kwenye Matendo 8:26-39 na kusoma hadithi ya kuongoka kwa mtu kutoka Kushi kama mtu aliye mtii Kristo. Kisha unaweza kuwauliza wale wanaotaka kumtii Bwana. “Je, unaamini kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu?” baada ya kukiri kwao unaweza kuwapeleka ziwani au katika kijito cha maji, au mahali popote yanapopatikana  maji ya kutosha kuwazamisha na kuwabatiza. Kabla ya ubatizo waeleze kwamba unawabatiza kwa mamlaka ya Yesu Kristo kwa jina la Baba na Mwana na  Roho Mtakatifu kwa ondoleo la dhambi zao (Mathayo 28:18-20). Unaweza kumchukua mtu mmoja na kumzamisha ndani ya maji. Hakikisha anafunikwa kabisa na maji kwa sababu ubatizo ni mazishi ambayo mfano wake ni kuzikwa kwa Kristo (Warumi 6:3,6 na Wakolosai 2:12). Unapokuwa na mtu mmoja au zaidi aliyemtii Bwana, una mwanzo wa kusanyiko la kanisa la Bwana katiak mji wako.

Mnaweza kukutana nyumbani kwako kwa ajili ya ibada katika siku ya Bwana au mnaweza kupanga kukutana katika ukumbi fulani wa umma. Unaweza kualika familia yako na marafiki kuja. Unaweza kuwa na nafasi ya kutangaza mahali pako pa kukutania na kuhimiza umma kuja. Utakuwa na uamuzi wako na washirika wengine kupanga nani atahudumia nini linapokuja suala la mafundisho, uongozi wa maombi huduma ya meza ya Bwana kuongoza uimbaji n.k kwa kweli wanawake hawawezi kupangwa kuhudumia hadharani mbele ya wanaume, wanaweza kusaidia kuandaa mkate na mzao wa mzabibu kwa ajili ya

meza ya Bwana. Pia wanaweza kufundisha watoto au kukutana na wanawake wengine kwa ajili ya kujifunza Biblia.

Kuhusu mahubiri au madarasa ya Biblia, tunaishi katika nyakati za ajabu. Ikiwa hakuna mtu aliye tayari kuhubiri katika hatua hii, maandiko fulani yanaweza kusomwa, na pia kipeperushi cha injili au makala inaweza kusomwa kwa waliopo. Zaidi ya hayo, [unaweza kumwomba mhubiri mzoefu…] kama utatuandikia mahubiri yaliyorekodiwa, labda tunaweza kutuma baadhi mara kwa mara. Kwa mkanda kanisa litaweza kusikia mahubiri hayo wiki baada ya wiki.

Pia ikiwa utatuandikia sisi au Wakristo wengine ili uweze kujua, labda mpangilio fulani unaweza kufanywa kwa ajili ya mahubiri kuja kwako kwa madhumuni ya kuendesha baadhi ya mikutano ya injili.

Ikiwa wewe ni Mkristo mchanga au mwanamke, unaweza kuona ni vigumu kuanzisha kusanyiko lakini ikiwa utalifanyia kazi, jaribu kufanya hivyo wasiliana na mtu anayeweza kukusaidia, na uendelee kufundisha familia yako washirika na marafiki, basi utakuwa na uwezo wa kufanya kitu. Inaweza kuchukua muda kidogo, lakini hakika utafaulu.

Kwa kweli, hii haisumbui wala siyo ngumu kama inavyodhaniwa kinachohitajika ni kwa Mkristo mmoja au zaidi aliyeazimia kwenda kufanya kazi kwa ajili ya Bwana, kuanza kwa kanisa na ukuaji wake vitafuata bila shaka.

## Somo la 9

# JINSI YA KUBATIZA

Mfululizo wetu wa masomo juu ya mada ya J**insi ya Kuanzisha Kanisa la Kristo Mahali Ulipo**, linaendelea. Kama wewe uko mahali ambapo kanisa halipo tunataka kukuhimiza ili uanzishe kanisa liwepo hapo ulipo. Bila shaka kama wewe si mshirika jambo la kwanza unachohitaji kufanya ni kumtii Bwana na kuwa mshirika. Kisha utakuwa katika nafasi ya kuanzisha kusanyiko.

Tunapozingatia mambo yote yanayohusika katika kitu kama hiki, tunakuja kwenye suala la ubatizo na hasa jinsi ya kubatiza.

Kwanza tunataka kusisitiza tena maana ya kimaandiko juu ya ubatizo na madhumuni yake. Biblia inatuambia kwamba ubatizo ni maziko, au kuzamishwa na kwamba unafanyika ndani ya maji. Paulo alisema, *"Mkazikwa pamoja naye katika ubatizo; na katika huo mkafufuliwa pamoja naye, kwa kuziamini nguvu za Mungu aliyemfufua katika wafu."* (Wakolosai 2:12). Wakati mwingine alisema, *"Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima."* (Warumi 6:3,4). Tunaambiwa kwanza wakati Yohana anambatiza Kristo *"alipanda mara kutoka majini"*

Katika Matendo 8 tunasoma kuhusu Filipo alivyomfundisha mtu kutoka Kushi. Walipofika kwenye maji, mkushi huyo alitaka kujua kama angeweza kubatizwa. Filipo alimwambia kwamba angeweza, kama tu aliamini kwa moyo wake wote kuwa Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu. Kisha akamkiri Kristo na wote wawili wakushuka wakaingia kwenye maji, Filipo alimbatiza yule towashi, kisha wote wawili wakapanda kutoka katika maji.

Kwa nini wote wawili walishuka majini? Ili Filipo aweze kumzamisha mtu huyu, na baada ya kumzamisha, Filipo na yule mkushi wakapanda kutoka majini. Hivyo Biblia kwa uwazi inafundisha kwamba ubatizo ni kuzikwa katika maji.

Kisha tunataka kusema kwamba ubatizo ni kwa ajili ya ondoleo la dhambi. Hatusemi kwamba ubatizo pekee ndio unaokoa, bali ubatizo huokoa (huondoa dhambi) kwa msingi wa kwamba mtu **anasikia** ukweli, **anamwamini** Mungu na kisha **kubatizwa**. Kristo aliwatuma mitume kwenda ulimwenguni pote na kuhubiri injili kwa kila kiumbe (mtu) kwa kufanmya hivyo walipaswa kuhubiri kwamba, *"Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini, atahukumiwa."* (Marko 16:16). Petro na mitume wengine walihubiri katika umati mkubwa katika mji wa Yerusalemu na wakati watu hao walipouliza wafanye nini *"Petro akawaambia, Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu."* (Matendo 2:38). Ubatizo humweka mtu ndani ya Kristo na ndani ya kanisa. Kauli kama hiyo inapatikana katika Wagalatia 3:26,27 wakati Paulo alisema *" Kwa kuwa ninyi nyote mmekuwa wana wa Mungu kwa njia ya imani katika Kristo Yesu. Maana ninyi nyote mliobatizwa katika Kristo mmemvaa Kristo."*

Hatimaye, katika ubatizo mtu anafanikisha **kufa**, **kuzikwa** na **kufufuka** kwa Kristo. Kristo alikufa msalabani, katika kumtii Bwana mtu hufa kwa ajili ya dhambi zake au huziacha dhambi zake. Kristo alikuwa amezikwa kaburini. Anayemtii Bwana anazikwa ndani ya maji ya ubatizo, kisha Kristo alifufuka kutoka kaburini. Vile vile, yule anayemtii Baba aliye mbinghuni anainuliwa kutoka katika kaburi la maji na kutembea katika upya wa uzima. Yote haya yapo katika Warumi 6. Mtu anapobatizwa anaonesha kufa kwa Bwana, kuzikwa na kufufuka katika utii wake katika kweli, hilo ni tendo zuri!

Ikiwa umebatizwa na wewe ni mshirika wa kanisa, basi uko tayari kufundisha ukweli huu kwa wale walio karibu nawe. Lakini utafanya nini ikiwa mtu anataka kubatizwa? Labda hakuna wa kubatiza ila wewe. Lakini unawezaje kulifanya jambo hilo? Kwa kweli, yote ni rahisi sana. Kwanza tafuta maji ambayo yana kina cha kutosha kwa mtu kuzamishwa. Inaweza kuwa mto, kijito kidogo, ziwa au kisima cha maji mahali fulani. Ikiwa unaishi kando ya bahari unaweza kubatiza hapo kila wakati. Kinachofuata, panga muda kwa ajili ya ubatizo. Mwelekeze mtu huyo aje kwenye maji, awe na nguo za kubatiziwa na nguo za kubadilisha pamoja na taulo. Huenda anayebatiza akataka kuleta taulo

na nguo za kubadilisha. Pengine wanafamilia na marafiki watakuja pamoja na kushuhudia ubatizo.

Unaweza kutaka kuwa na wimbo mmoja au miwli. Bila shaka utataka kusoma baadhi ya maandiko, labda Matendo8:26-39 ili kuonesha jinsi Filipo alivyomtaka mtu kutoka kushi kukiri imani yake katika Kristo kabla ya kuendelea na ubatizo. Baada ya kusoma maandiko unaweza kumgeukia yule anayebatizwa na kumwuliza swali hili **"Je, Unaamini kuwa Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu?"** ikiwa mtu huyo atakubari kufanya hivyo, atasema tu, "Ndiyo, ninaamini kuwa **Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu**".

Maadam ukiri umefanyika basi umwongoze mtu huyo kwenye maji mahali pana kina cha kutosha kwa kumzamisha, lakini kabla ya ubatizo utataka kutoa neneo hili **"kulingana na shauku yako ya kumtii Bwana, na kukiri kwako kwamba unaamini kuwa Yesu kristo ni Mwana wa Mungu, kwa mamlaka ya Yesu Kristo, ninakubatiza kwa jina la Baba na Mwana, na Roho Mtakatifu kwa ondoleo la dhambi zako. Amina"** Kauli hii ya mamlaka inapatikana katika Mathayo 28:18-20.

Kisha utachukua mikono ya mtu huyo, weka mkono mmoja juu ya mwingine, kisha utamweleza utumie mkono wako mmoja kubana pua na hakuna kitu cha kuogopa. Ikiwa kina cha maji sio kirefu, mwombe akae kitako ili aweze kuzama katika maji kirahisi. Kisha weka mkono wako mwingine nyuma ya mgongo wake [usawa wa mabega na shingo] na kumlaza taratibu kwa nyuma ili azikwe kabisa ndani ya maji. Halafu mpandishe mara moja kutoka majini. Hivyo ndivyo inavyofanyika. Ni rahisi sana kufanya, na ni nyepesi. Hakuna kitu cha kuogopa juu ya maji kwa sababu hutaenda zaidi ya kina kinachoweza kudhibitiwa na ubatizo unachukua sekunde chache tu.

Njia nyingine ya ubatizo ni kumfanya mtu apige magoti ndani ya maji, kichwa tu kibaki nje ya maji na kisha kuzamisha kichwa chini ya maji. Kwa njia hiyo huna haja ya kushughulika na uzito wa mtu huyo ukimuegemeza nyuma na kisha kumvuta juu. Jambo kuu ni kumzamisha muumini aliyetubu. Hilo likifanyika, basi inaonesha ametii aliyoyaamuru Bwana. Amebatizwa kimaandiko.

Ikiwa vitabu vya nyimbo vimeletwa, wimbo mmoja au miwili zinazoweza kuimbwa baada ya ubatizo. Ikiwa mtu anaebatizwa ni mwanaume, unaweza kumwomba aongoze sala kama anaweza, kwa kuwa sasa yeye ni Mkristo mpya Ndugu mpya katika Kristo. Hii itakuwa sala yake ya kwanza kama Mkristo na jinsi gani itapendeza kumsikia akimshukuru Bwana kwamba sasa yeye ni mtoto wa Mungu. Nimesikia baadhi ya sala nzuri za wale ambao wamemtii Bwana.

Sasa kwa kuwa mtu huyu amebatizwa, Bwana amemuongoza katika kanisa lake. Katika hali ya kusanyiko la mahali pamoja ni Mkristo, hapo sasa kuna mawili au zaidi wanaounda kanisa mahali ulipo. Katika kuwafundisha wengine, huduma hii ya ubatizo hakika itarudiwa mara nyingi.

Bila shaka unaelewa kwamba kunyunyiza na kumwaga maji kichwani sio ubatizo wa kimaandiko.

Je, wewe mwenyewe, umemtii Bwana katika ubatizo? Ikiwa sivyo, sisi tunaomba kwamba uweze kufanya hivyo.

### Somo la 10

## JINSI YA KUABUDU

Masomo yetu yanaendelea juu ya somo la jumla la **Jinsi ya Kuanzisha Kanisa la Kristo Mahali Ulipo.** Kama wewe si Mkristo na mshirika wa kanisa, tunataka kuhimiza kuwa mmoja wapo, lakini ikiwa wewe ni mshirika, na kama hakuna kanisa mahali ulipo, tunataka kukuhimiza uanzishe kusanyiko huko. Unaweza kuanza kwa kuanzisha makusanyiko ya Biblia ndani ya nyumba yako na wanafamilia wako, na marafiki wengine wanapofahamu vya kutosha watataka kumtii Bwana, hivyo utaweza kuanzisha kanisa mahali hapo ulipo.

Katika somo hili tunataka kujadili jinsi ya kuabudu. Sisi sote tunahitaji kujua jinsi ya kumwabudu Mungu, ikiwa tunataka kuanzisha kusanyiko jipya.

Biblia ina mengi ya kusema kuhusu ibaada. Shetani alipomjaribu Yesu ili asujudu mbele yake katika kuabudu, Kristo alijibu *"Ndipo Yesu alipomwambia, Nenda zako, Shetani; kwa maana imeandikwa, Msujudie Bwana Mungu wako, umwabudu yeye peke yake."* (Mathayo 4:10). Tena Yesu alisema, *"Mungu ni Roho, nao wamwabuduo yeye imewapasa kumwabudu katika roho na kweli."* (Yohana 4:24), kwa hiyo haitoshi kuabudu bali tunapaswa kumwabudu Mungu pekee na lazima tumwabudu kwa uaminifu na kwa kadri ya mapenzi yake, kama alivyoeleza katika neno lake.

Watu wengi huabudu katika hali ya ujinga, bila hata kuelekeza ibada zao kwa Mungu wa mbinguni. Mtume Paulo alikutana na kundi la watu kama hawa katika mji wa Athene (Matendo 17:23). Kristo alisema kwamba wengi walimwabudu Mungu lakini walimwabudu bure kwa sababu walabudu kulingana na mafundisho na amri za wanadamu (Mk 7:7). Kwa hiyo tunahitaji kufikiria aina ya ibada ambayo Mungu anaitaka. Katika kuanzisha kusanyiko jipya, Mungu ataabudiwa namna gani? Hebu twende kwenye Biblia yenyewe tuone kile ambacho kinahitajika.

Watu wa Bwana wanaweza kukutana wakati wowote au mahali popote ili kumsifu Muumba wao kwa **kusoma na kujifunza** maandiko, **kusali** kwa Baba na **kuimba** sifa zake. Lakini Bwana haswa alilieleza

kanisa kukutana kila siku ya kwnza ya juma ili kufanya mambo fulani yanayohitajika katika ibaada yake. Katika Matendo 20:7 kumbukumbu inatuambia kuhusu kukusanyika kwa kanisa siku ya kwanza ya juma kwa ajili ya kuabudu. Paulo aliwaamru Wakristo wa Korintho kuweka akiba, kama Mungu alivyowafanikisha, siku ya kwanza ya juma (1 Wakorintho 16:2)

Chini ya sheria ya Agano la Kale siku ya kuabudu ilikuwa siku ya sabato, au jumamosi lakini ujio wa Kristo, katika kifo chake msalabani, Bwana aliondoa sheria ya zamani na kuleta mpya ambayo ni bora zaidi (Waebrania 8:13;15-17). Katika sheria mpya aliyoitoa siku mpya ya ibada ni, siku ya kwanza ya juma, siku ya Bwana, siku tunayoiita Jumapili.

Kwa hiyo Wakristo wanapaswa kukusanyika katika siku hiyo kwa ajili ya ushirika na ibaada. Bwana ameahidi kuwa pamoja na watu wake, ingawa wanaweza kuwa wawili au watatu tu wamekusanyika pamoja (Mathayo 18:20). Anaposema nasi kupitia neno lake. Sisi pia tunamatendo kadhaa ya ibaada tunayapitia ili kumheshim na kulitukuza jina lake.

Njia moja wapo ya kumkaribia Mungu ni kupitia kusoma na kujifunza neno lake. Kwa njia hii Mungu anazungumza nasi, akituambia kuhusu mambo ambayo yeye anataka tufanye. Kristo alisema sisi tunapaswa kuchunguza maandiko (Yohana 5:39). Paulo aliandika *"Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali neno la kweli."* (2 Timotheo 2:15). Mungu hasemi nasi kwa sauti ya kusikika, bali huzungumza kupitia neno lake. Kwa hiyo, tunapaswa kusikiliza katika tabia ya uchaji na unyenyekevu, kisha tuendelee kumtii. Yakobo anasema *"Lakini iweni watendaji wa neno, wala si wasikiaji tu, hali mkijidanganya nafsi zenu."* (Yakobo 1:22). Katika Yakobo 1:21 anasema neno hili laweza kuokoa roho zetu. Yakobo 1:25, inatukumbusha, *"Lakini aliyeitazama sheria kamilifu iliyo ya uhuru, na kukaa humo, asiwe msikiaji msahaulifu, bali mtendaji wa kazi, huyo atakuwa heri katika kutenda kwake."* Tunaweza kuona umuhimu na thamani ya kujifunza au kusikia neno la Mungu tunapokutana kwenye ibada.

Tendo lingine la ibaada ni **maombi**. Bwana anataka kusema nasi kupitia neno lake, lakini anataka tuombe kwake. Tunapaswa kuomba katika maisha yetu binafsi, lakini yeye pia anataka tuombe pamoja kama kusanyiko la watu wake. Baada ya kanisa kuanzishwa tunasoma juu ya wanafunzi *"Wakawa wakidumu katika fundisho la mitume, na katika ushirika, na katika kuumega mkate, na katika kusali."* (Matendo 2:42). Kristo alisema sisi imetupasa kusali siku zote wala tusikate tamaa (Luka 18:1). Paulo alisema tunapaswa kuomba bila kukoma, au kuwa na roho ya maombi au ya tabia ya maombi daima (1 Wathesalonike 5:17) katika tukio lingine alisema, *"Msijisumbue kwa neno lo lote; bali katika kila neno kwa kusali na kuomba, pamoja na kushukuru, haja zenu na zijulikane na Mungu."* (Wafilipi 4:6). Tunaweza kuendelea kwa kuzingatia aya zote za maandiko zinazozungumzia maombi, lakini katika sala zetu za faragha na za hadharani, tunapaswa kuweka akilini maelezo ya Yohana *"Na huu ndio ujasiri tulio nao kwake, ya kuwa, tukiomba kitu sawasawa na mapenzi yake, atusikia. Na kama tukijua kwamba atusikia, tuombacho chote, twajua kwamba tunazo zile haja tulizomwomba."* (1 Yohana 5:14,15). Maneno muhimu hapo ni kwamba tunapaswa kuomba sawasawa na mapenzi yake. Tunapofanya hivyo, Bwana atasikia na kujibu maombi yetu. Ni lazima tutambue kwamba yeye anajua kilicho bora kwetu.

Kisha fikiria **kuimba** kama tendo la ibada. Paulo anasema, *"Neno la Kristo na likae kwa wingi ndani yenu katika hekima yote, mkifundishana na kuonyana kwa zaburi, na nyimbo, na tenzi za rohoni; huku mkimwimbia Mungu kwa neema mioyoni mwenu."* (Wakolosai 3:16). Utaona kwamba katika maelezo haya inasisitiza ukweli kwamba tunaweza kuimba na kumshangilia Bwana mioyoni mwetu. Katika Waebrania 13:15 tunaambiwa kwamba tunapaswa kumsifu *"Basi, kwa njia yake yeye, na tumpe Mungu dhabihu ya sifa daima, yaani, tunda la midomo iliungamayo jina lake."* Yote haya ni kusema kwamba Mungu anataka tumsifu, badala ya kutumia vyombo vya muziki kama njia ya kumwabudu.

Tunapaswa pia kushiriki katika **karamu ya ukumbusho** kila siku ya kwanza ya juma (Matendo 20;7). Paulo anasema katika 1 Wakorintho 11 kwamba tunapaswa kushiriki mkate (mkate usiotiwa

chachu) kwa ukumbusho wa mwili wa Kristo na mateso yote aliyovumilia kwa niaba yetu. Na kushiriki kikombe (mzao wa mzabibu au maji ya zabibu) kwa kumbukumbu ya damu ya Kristo, damu iliyomwagika ili sisi tupate ondoleo la dhambi zetu. Anasema kwamba tunapaswa kushiriki mkate na kikombe tu baada ya kujichunguza wenyewe ili kuwa na uhakika kwamba tunafanya hivi kutoka moyoni na kwa ukumbusho wake.

Na hatimaye, tunapaswa **kutoa** pesa zetu siku ya kwanza ya juma (1 Wakorintho 16:2). Tunapaswa kutoa kwa kadri ya kufanikiwa , kama tulivyokusudia mioyoni mwetu, si kwa huzuni au kwa lazima bali kwa furaha (2 Wakorintho 9:7). Hili lifanyike kwa hiari na fedha zinazotolewa zitumike katika kazi ya Bwana.

Katika kusanyiko jipya wanaume wanapaswa kupanga nani atasoma maandiko au kutoa somo, nani ataongoza maombi, nani ataongoza uimbaji, ni nani atakae hudumia katika meza ya Bwana. Hii inapaswa kuwapanga mapema kiasi cha kutosha ili kwamba maandalizi katika kundi yawepo mapema.

### Somo la 11

## JINSI YA KUHUDUMIA MEZA YA BWANA

Tunaendelea na mfululizo wetu kuhusu **jinsi unavyoweza kuanzisha kanisa la Kristo mahali ulipo.** Hata hivyo lazima utambue kwamba ili kufanya hivyo, lazima kwanza uwe mshirika wa kanisa wewe mwenyewe. Ikiwa wewe si mshirika tungependa kukutia moyo uwe mmoja wa washirika. Unaweza kufanya hivyo kwa kumwamini Mungu, kutubu dhambi zako, kukiri kwa kinywa chako kuwa Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu na kubatizwa au kuzikwa katika maji kwa ajili ya ondoleo la dhambi zako. Kwa utiifu wako, Bwana atakuokoa na atakuongeza katika kanisa lake (Marko 16:16; Mdo 2:47).

Katika somo hili tutajadili jinsi ya kuhudumu katika meza ya Bwana ili kukuongoza katika juhudi zako za kuanzisha kanisa mahali ulipo.

Meza ya Bwana ilianzishwa na Kristo pale aliposhiriki chakula cha jioni cha mwisho na mitume wake wakati wa sikukuu ya mikate isiyotiwa chachu, au sikukuu ya Pasaka. Kristo aliishi na kufa chini ya sheria ya Musa, lakini sheria hiyo iliondolewa na kifo chake na Agano Jipya likachukua nafasi yake. Agano hilo mwanzilishi wake ni Kristo. Kristo na mitume walikusanyika kwa ajili ya sikukuu ya pasaka, na alitumia nafasi hii kuanzisha Meza ya Bwana. Kumbukumbu inasema, *" Nao walipokuwa wakila Yesu alitwaa mkate, akabariki, akaumega, akawapa wanafunzi wake, akasema, Twaeni, mle; huu ndio mwili wangu Akakitwaa kikombe, akashukuru, akawapa, akisema, Nyweni nyote katika hiki; kwa maana hii ndiyo damu yangu ya agano, imwagikayo kwa ajili ya wengi kwa ondoleo la dhambi. Lakini nawaambieni, Sitakunywa kabisa tangu sasa uzao huu wa mzabibu, hata siku ile nitakapokunywa mpya pamoja nanyi katika ufalme wa Baba yangu."* (Mathayo 26:26 - 29). Aya ya mwisho ya kifungu hiki katika maneno ya Kristo, inaonyesha kwamba yeye asingeshiriki meza ya Bwana tena hadi baada ya kifo, mazishi, na ufufuo wake, na pia baada ya kuanzishwa kwa kanisa. Tena yeye angekuwa Pamoja na watu wake katika Roho wanaposhiriki chakula cha Bwana kwa ajili ya

ukumbusho wake. Uasisi wa chakula cha Bwana umeelezwa katika Marko 14:22 – 25 na katika Luka 22:14 – 20.

Paulo aliwaandikia Wakristo wa Korintho kuhusu chakula cha Bwana akasema, *"Kwa maana mimi nalipokea kwa Bwana niliyowapa nanyi, ya kuwa Bwana Yesu usiku ule aliotolewa alitwaa mkate, naye akiisha kushukuru akaumega, akasema, Huu ndio mwili wangu ulio kwa ajili yenu; fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu. Na vivi hivi baada ya kula akakitwaa kikombe, akisema, Kikombe hiki ni agano jipya katika damu yangu; fanyeni hivi kila mnywapo, kwa ukumbusho wangu. Maana kila mwulapo mkate huu na kukinywea kikombe hiki, mwaitangaza mauti ya Bwana hata ajapo. Basi kila aulaye mkate huo, au kukinywea kikombe hicho cha Bwana isivyostahili, atakuwa amejipatia hatia ya mwili na damu ya Bwana. Lakini mtu ajihoji mwenyewe, na hivyo aule mkate, na kukinywea kikombe. Maana alaye na kunywa, hula na kunywa hukumu ya nafsi yake, kwa kutokuupambanua ule mwili."* (1 Wakorintho 11:23 - 29).

Kutokana na maandiko yaliyotangulia nadhani ni Dhahiri kuwa Bwana anataka watu wake washiriki ukumbusho huu wa chakula cha Bwana. Inapaswa pia kuwa wazi kwamba mkate unaotumika ni ukumbusho wa mwili wa kristo na kikombe au mzao swa mzabibu ni ukumbusho wa damu ya Kristo. Lakini kwa nini Bwana anataka tufanye hivyo? Ili tuweze kumkumbnuka yeye na dhabihu aliyoitoa ili sisi tupate kuokolewa. Tunaposhiriki tusema nafsini mwetu, kwa Bwana na kwa ulimwengu kwamba tunaamini kwamba Yesu Kristo yu hai na kwamba atakuja tena siku moja.

Paulo alisema kwamba kabla ya kula chakula cha Bwana tunapaswa kujichunguza. Kwa maneno mengine ikiwa tunachunguza mioyoi yetu na Maisha na kugundua kwamba tuna dhambi ndani yetu ambayo haijatubiwa na kusamehewa, tunapaswa kujirekebisha pasipo kufanya hivyo tunaweza kuifanya mioyo yetu kuwa migumu dhidi ya Mungu na hatimaye kupotea.

Ni nani anayeweza kushiriki Meza ya Bwana? Kwa kweli imekusudiwa tu kwa ajili ya watu wa Bwana, lakini tunaipitisha kwa wale wote walioko ndani ya mkusanyiko. Kisha ni juu ya kila mtu kuamua kwamba atakula au la. Hatuwezi kumkataza mtu yeyote

kushiriki kwa sababu rahisi kwamba mtu anaweza kututembelea ambaye hatujakutana naye na kumfundisha. Kama tutaruhusu wale tu tunaowajua kuwa ni wakristo kushiriki Meza ya Bwana, tunaweza kuwazuia baadhi ya wakristo wanaozuru (wanaotembelea) kushiriki. Kwa hivyo huu ni uamuzi wa kila mtu binafsi nafsini mwake mwenyewe

Jambo linalofuata, ni lini tunsapaswa kushiriki Meza ya Bwana na tufanye kila baada ya muda gani? Katika Matendo 20:7 tuna mfano wa watu wa Bwana waliokusanyika kwa ajili ya ibada siku ya kwanza ya juma na wakati wa mkutano huo walishiriki Meza ya ya Bwana. Tunasoma, *"Hata siku ya kwanza ya juma, tulipokuwa tumekutana ili kumega mkate, Paulo akawahutubu, akiazimu kusafiri siku ya pili yake, naye akafuliza maneno yake hata usiku wa manane."*.

Kama katika Matendo 2:42, mstari huu unazungumza juu ya watu wake Bwana "Kuumega mkate". Katika matukio yote mawili kinachorejelewa ni kushiriki meza ya Bwana. Lakini ni mara ngapi Wakristo hukusanyika ili kuimba, kuomba, kujifunza neno la Mungu, na kutoa kwa kadri ya uwezo vwao? Kila siku ya kwanza ya juma au kila Jumapili (japo matendo ya kuimba, kuomba na kujifunza neno yanaweza kufanyika hata siku nyingine). Sasa je, ni mara ngapi wakristo wanapaswa kushiriki chakula cha Bwana? Kama unakumbuka, Paulo alisema, *"Maana kila mwulapo mkate huu na kukinywea kikombe hiki, mwaitangaza mauti ya Bwana hata ajapo."* (1 Wakorintho 11:26). Hiyo ni mara ngapi? Kila siku ya kwanza ya juma.

Tunajua kwamba wengi wa marafiki zetu, watu wa dini wanakuwa na chakula cha Bwana mara moja tu kila baada ya miezi mitatu, au robo mwaka. Wengine wanashiriki katika matukio maalum, labda mara moja kwa mwaka. Lakini inatupasa tuombe kutofautiana na watu hawa. Hatukubaliani nao kwa msingi wa jinsi maandiko yanafundisha. Ikiwa hatutafuata amri na mifano iliyowekwa katika neno la Mungu, kwa nini tujisumbue na mambo ya dini?

Ikiwa utaanzisha kusanyiko mahali ulipo, wewe lazima ukumbuke kwamba ibada ya kimaandiko katika siku ya kwanza ya juma itajumuisha meza ya Bwana. Kama kuna washirika wawili au kumi na wawili au zaidi ni wanaume, basi wanapaswa kumchagua wa

kufundisha maandiko, wa kuongoza katika maombi na wa kuongoza nyimbo. Kisha mtu mmoja anapaswa kuteuliwa kuhudumu kwenye meza ya Bwana. Kabla ya kushiriki meza ni vizuri kutoa maelezo fulani japo kwa kifupi kuhusu jambo hilo, pamoja na kusoma baadhi ya maandiko kama vile yanayopatikana katika 1 Wakorintho 11:23 – 29 au Mathayo 26:26 – 29. Maandiko mengine yakiambatanishwa na kifo cha Kristo pia yanaweza kutumika. Mtu anayehudumu kwenye Meza ya Bwana baada ya kutoa shukrani kwa ajili ya mkate, atamke kwamba kila mmoja na ashiriki kwa ajili ya ukumbusho wa mwili wa Kristo juu ya mateso yake na kifo chake msalabani. Yeye au wengine wanaosaidia, basi wapitishe mkate huo pande zote ili waliopo wapate nafasi ya kuishiriki, ikiwa wana shauku hiyo. Baada ya kushiriki mkate, shukrani zinaweza kutolewa kwa ajili ya kikombe, au mzao wa mzabibu, Pamoja na maelezo ya ukweli kwamba inawakilisha kumwagika kwa damu ya kristo. Mzao wa mzabibu, kawaida huwa katika vikombe vidogo, basi unaweza kupitishwa kote.

Mara nyingi wanawake hufanya maandalizi ya chakula cha Bwana, kwa kawaida ni katika hali ya kujitolea. Mkate usiotiwa chachu unaokwa na kisha maji ya zabibu yanaweza kununuliwa, ikiwa inapatikana, au matunda ya zabibu, au zabibu kavu zinaweza kununuliwa, na zabibu hizo zinaweza kukamuliwa ili kupata juisi, au zabibu kavu zinaweza kuchemshwa na juisi yake ikatumika. Maandalizi ya mwisho yanaweza kufanywa Jumamosi jioni au Jumapili asubuhi. Mkate unaweza kuwekwa kwenye sahani na mzao wa mzabibu unaweza ukatiwa kwenye vikombe vidogo au bilauli.halafu vitu hivi hupangwa kwenye meza na labda hufunikwa na kitambaa safi. Wote wanaoshiriki katika kumbukumbu hii wanapaswa fikiria kuwa ni heshima kufanya hivyo.

## Vichanganyio vya mkate wa ushirika

½ kikombe cha unga.
Vijiko 2 vya chakula vya mafuta ya kula.
Kiasi kidogo cha chumvi.
Maji(kama vijiko 2 vya chakula).

Weka Mafuta kwenye unga. Ongeza takriban vijiko 2 vya maji baridi, Changanya vizuri kisha tandaza (kama chapati) katika sehemu iliyopakwa unga. Weka alama za miraba midogo midogo kwa kutumia kisu au kitu chochote, oka katika joto la kadri mpaka utakapoona mkate umekuwa na rangi ya kahawia. Kiasi kinaweza kuongezeka au kupunguzwa kulingana na mahitaji. Mkate unapaswa kutayarishwa usiku mmoja kabla ili uwe tayari unapohitajika.

**Betty Burton Choate.**
**Maelekezo juu ya mzao wa mzabibu.**

Kwa upande wa mzao wa mzabibu, unaweza kuwa na uwezo wa kununua chupa ya juisi ya zabibu. Kama haipatikani unaweza kununua zabibu kavu, zichemshe, kisha uchukue maji yake na kuyaweka kwenye vikombe vidogo au glasi (bilauli). Au unaweza kununua kiasi fulani cha zabibu na kukamua maji yake na kuweka kwenye vikombe.

## Somo la 12

# JINSI YA KUOMBA

Tunaendelea na mfululizo wa masomo yetu **Jinsi ya Kuanzisha Kanisa la Kristo Mahali Ulipo.** Kama wewe ni Mkristo na uko mahali ambapo kanisa halipo, tunataka kukusaidia kuanzisha kanisa mahali ulipo. Unachohitaji ni maarifa ya namna ya kuanzisha na bidii ya kuendesha na ubunifu katika kufanikisha. Kwa kweli ikiwa umekaa hapo unangojea mtu mwingine kuanza kazi inaweza isifanyike kamwe. Fikiria mwenyewe kama ungekuwa ni yule ambaye Bwana anaweza kumtumia katika hali kama hii. Ingekuwa furaha na fursa iliyoje ya kufanya kazi na Mungu kwa njia hiyo! Kufikia sasa tumeshughulikia masomo kadhaa muhimu yanayohusiana na mada hii na sasa tunataka kujadili jinsi ya kuomba.

Ikiwa una nia ya kuanzisha kusanyiko na kuwa na huduma ya ibada ya hadhara, utahitaji kujua kitu kuhusu maombi, sala ya hadharani, umuhimu wake na jinsi ya kuifanya.

Kwanza nieleze maombi ni nini. Ni njia ya kupitia ili tuzungumze na Baba yetu aliye mbinguni. Kwa maneno mengine, maombi ni mojamoja ya baraka na upendeleo uliotolewa kwa watu wa Mungu. Lakini watu wa Mungu ni nani? Wale ambao wamemtii yeye, waliookolewa yaani Wakristo, Watoto wa Mungu,washirika wa kanisa la Bwana, ambalo ni familia yake ya Kiroho. Ikiwa utasoma katika maandiko utaona kwamba sala imehifadhiwa kwa ajili ya wana na binti walio na uhusiano na Baba yao. Mwenye dhambi, mmoja ambaye hajaokoka, ambaye si mtoto wa Mungu, hawezi kustahili kumwomba Mungu kwa matarajio ya kujibiwa maombi yake. Yule kipofu ambaye Yesu alimponya alikuwa na haya ya kusema, *"Twajua ya kuwa Mungu hawasikii wenye dhambi; bali mtu akiwa ni mcha Mungu, na kuyafanya mapenzi yake, humsikia huyo."* (Yohana 9:31). Mtu huyu alikuwa anaelezea kanuni ya ukweli. Alisema kwamba Mungu hamsikii mwenye dhambi, katika maana ya kujibu maombi yake, yeye huwasikia hao wanaomwabudu na kutii mafundisho yake na bila shaka hili linamrejelea yule aliyefanyika kuwa mtoto wa Mungu, Paulo alisema, *"Kwa kuwa macho ya Bwana huwaelekea wenye haki, Na masikio yake*

*husikiliza maombi yao; Bali uso wa Bwana ni juu ya watenda mabaya.”* (1 Petro 3:12). Isaya aliandika hapo zamani za kale, *“Tazama, mkono wa Bwana haukupunguka, hata usiweze kuokoa wala sikio lake si zito, hata lisiweze kusikia; lakini maovu yenu yamewafarikisha ninyi na Mungu wenu, na dhambi zenu zimeuficha uso wake msiuone, hata hataki kusikia.”* (Isaya 59:1,2).

Ili kutusaidia kuona kwamba ni lazima tuwe Watoto wa Mungu ili yeye atusikie, fikiria kuhusu mgeni anayeitaka serikali ya mtaa impe upendeleo na haki ambazo zimewekwa kwa ajili ya wazawa. Bila shaka tunajua hilo halifanyika. Wala Mungu hawapi wale ambao si Watoto wake baraka, bali huwapa walio wake. Ikiwa alisikia na kujibu maombi ya mwenye dhambi, kama vile afanyavyo kwa Watoto wake wenyewe, Je! Watoto wake wangekuwa na nafasi gani dhidi ya wale wasio wake? Hakika unaweza kuona tofauti. Suala ni kwamba ikiwa mtu anataka upendeleo wa maombi, lazima awe mtoto wa Mungu.

Mengi yanasemwa kuhusu maombi katika maandiko. Wakristo wa awali, *“Wakawa wakidumu katika fundisho la mitume, na katika ushirika, na katika kuumega mkate, na katika kusali.”* (Matendo 2:42). Pauli alisema, *“Msijisumbue kwa neno lo lote; bali katika kila neno kwa kusali na kuomba, pamoja na kushukuru, haja zenu na zijulikane na Mungu.”* (Wafilipi 4:6). Yohana alitangaza, *“Na huu ndio ujasiri tulio nao kwake, ya kuwa, tukiomba kitu sawasawa na mapenzi yake, atusikia. Na kama tukijua kwamba atusikia, tuombacho chote, twajua kwamba tunazo zile haja tulizomwomba.”* (1 Yohana 5:14,15).

Tunaweza kuendelea kunukuu mistari ya maandiko ambayo inatia moyo maombi ya Mkristo binafsi na katika mpangilio wa kusanyiko. Kuna miongozo fulani, hata hivyo ambayo imewekwa kwamba tuweze kuzingatia. Kristo aliwaambia wanafunzi wake, *“Nanyi mkiomba lo lote kwa jina langu, hilo nitalifanya, ili Baba atukuzwe ndani ya Mwana. Mkiniomba neno lo lote kwa jina langu, nitalifanya.”* (Yohana 14:13,14). Katika (Yohana 15:16) aliahidi, *“Si ninyi mlionichagua mimi, bali ni mimi niliyewachagua ninyi; nami nikawaweka mwende mkazae matunda; na matunda yenu yapate kukaa; ili kwamba lo lote mmwombalo Baba kwa jina langu awapeni.”.* Tunaweza kuona hayo mambo yanakuwa wazi kabisa kuhusu wale wanaoweza kuomba na

masharti yaliyowekwa kwa ajili ya kujibu maombi hayo. Bwana anaelekeza neno lake kwa wanafunzi wake, kwa wale ambao wanamtii yeye. Anasema na hao wakaao ndani yake, wale walio ndani ya Kristo na kanisa lake. Anasema kwamba maombi kwa Baba lazima yapelekwe kwa jina lake kwa kuwa yeye ndiye mtetezi wetu (1 Yohana 2:1). Pia kama tulivyoona katika 1 Yohana 5:14,15, maombi yetu lazima yafanyike kulingana na mapenzi yake.

Kuna mambo mengine Bwana alisema kuhusu maombi. Yeye aliwafundisha wanafunzi wake, *"Tena msalipo, msiwe kama wanafiki; kwa maana wao wapenda kusali hali wamesimama katika masinagogi na katika pembe za njia, ili waonekane na watu. Amin, nawaambia, Wamekwisha kupata thawabu yao. Bali wewe usalipo, ingia katika chumba chako cha ndani, na ukiisha kufunga mlango wako, usali mbele za Baba yako aliye sirini; na Baba yako aonaye sirini atakujazi. Nanyi mkiwa katika kusali, msipayuke-payuke, kama watu wa mataifa; maana wao hudhani ya kuwa watasikiwa kwa sababu ya maneno yao kuwa mengi. Basi msifanane na hao; maana Baba yenu anajua mnayohitaji kabla ninyi hamjamwomba."* (Mathayo 6:5 - 8). Baada ya kuwaambia wanafunzi kwamba hawapaswi kuomba kwa kujionesha au kuonekana na watu, Bwana aliendelea kuwapa mfano wa jinsi ya kuomba. Hii inarejelewa na watu wengi wa kidini kama "Sala ya Bwana" na mara nyingi hurudiwa katika mikusanyiko ya ibada lakini kiukweli si sala ya Bwana. Ni kielelezo tu cha maombi na haikukusudiwa kutumika kama maombi kwa ajili ya Wakristo kusema binafsi. Ikiwa ilitumiwa hivyo, watu wa Bwana wangekuwa wanafanya jambo lile lile ambalo yeye alisema wasifanye, kufanya ili waonekane na kusikiwa na wanadamu na kupayuka-payuka. Kristo hata hivyo alikuwa akitumia sala hiyo kama mfano wa jinsi ya kuomba.

Inatakiwa kuwe na maombi wakati wa ibada ya kusanyiko. Washirika wanaweza kuomba binafsi na kwa pamoja, yaani kama ndugu wengine katika Kristo wanavyoongoza katika maombi. Mambo yote yafanyike kwa heshima na kwa utaratibu, hivyo wanaume wanapaswa kukusanyika kabla ya ibada na kuamua ni sala ngapi zitakuwepo, na wateue baadhi ya ndugu kuongoza katika maombi. Au ikiwa washirika wa kusanyiko wamekubaliana, anayesimamia huduma

anaweza tu kutangaza kwamba ndugu fulani ataliongoza kundi katika sala. Idadi yoyote ya maombi inaweza kuwepo wakati wa ibada.

Anayeongoza katika sala anapaswa kutoa shukrani kwa ajili ya Baraka za Bwana, kuomba mwongozo na msaada katika maisha ya watu, awakumbuke wagonjwa na wengine wenye mahitaji maalum, na aombe msamaha kwa ajili ya dhambi. Sala hii na nyingine zote zinapaswa kuelekezwa kwa Baba aliye mbinguni kwa kupitia jina la Kristo.

Anayeongoza katika sala atamke maneno vizuri na kwa sauti kubwa ya kutosha ili wote wasikie na kuweza kusema “Amina”, yaani ionekane hata wao wameshiriki katika kuomba.

Washirika wanaweza kuketi, kusimama, kupiga magoti, au kuwa katika mkao wowote wakati wa maombi, itakuwa vizuri zaidi kwao wakionesha unyenyekevu na uchaji wao kwa Mungu. Katika maandiko hali hii ya mikao wakati wa kuomba imewekwa wazi sana.

Maombi pia yanahusika wakati wa Meza ya Bwana, na kwa kawaida neno la shukrani hutolewa katika kanisa kwa kubarikiwa kuwa na kitu cha kutoa kabla mchango haujatolewa.

Bila shaka wanawake hawaruhusiwi kuongoza katika mkusanyiko, wa hadhara kama tutakavyoona katika somo lijalo.

## Somo la 13

# JINSI YA KUIMBA

Sasa katika mafunzo yetu juu ya ibada tunakuja kwenye somo la jinsi ya kuimba. Tumekuwa tukizungumza kuhusu sehemu mbalimbali za ibada. Pia tumekuwa tukijadili umuhimu wa ibada na jinsi ya kufanya hivyo kimaandiko.

Biblia inafundisha kwa hakika kwamba sisi kama Wakristo tunapaswa kushiriki katika kuimba tunapomwabudu Mungu. Kuna maandiko kadhaa ambayo tunataka kuyachunguza tunapofikiria kuhusu kuimba sifa kwa Mungu. Paulo aliwaandikia Wakristo wa Efeso, *"mkisemezana kwa zaburi na tenzi na nyimbo za rohoni, huku mkiimba na kumshangilia Bwana mioyoni mwenu;"* (Waefeso 5:19). Pia aliwaambia Wakolosai, *"Neno la Kristo na likae kwa wingi ndani yenu katika hekima yote, mkifundishana na kuonyana kwa zaburi, na nyimbo, na tenzi za rohoni; huku mkimwimbia Mungu kwa neema mioyoni mwenu."* (Wakolosai 3:16). Utaona katika marejeo haya mawili kwamba Paulo anasema walipaswa kuimba zaburi, nyimbo,na tenzi za rohoni, na kwamba walipaswa kushangilia mioyoni mwao. Hii inaonesha kwamba Bwana alitaka watu wake waimbe kwa sauti za midomo au muziki wa akapela tu. Kwa maneno mengine hapakupaswa kuwepo na vyombo vya muziki katika kuimba. Hili linaweza kusikika kama geni katika zama zetu, hasa wakati  vikundi vingi vya kidini hutumia ala za muziki katika huduma zao, lakini maandiko hayatetei popote,au hata kuhimiza jambo hilo.

Unaona, kuna aina mbili za muziki ulimwenguni. Moja ni ya zamani kuliko nyingine, na huo ni muziki wa sauti. Muziki huu umetengenezwa kwa msaada wa sauti zilizoundwa na Mungu, na inasemekana kuwa huu ni muziki mzuri zaidi ulimwenguni, uliotengenezwa na mchanganyiko  wa sauti za binadamu. Aina nyingine za muziki ni ya ala, inayozalishwa kwenye vyombo vilivyotengenezwa na binadamu. Binadamu anapiga ngoma, zeze au gitaa. Wanapiga vinanda, na aina nyingine nyingi za vyombo vya muziki. Lakini hivi vyote havina uhai, havina moyo, na sababu inayofanya vitoe sauti ni kwa sababu mtu hupiga juu yao.

Sasa ni ipi kati ya aina hizi za muziki Bwana anaitaka? Kama tulivyokwisha kuona, Paulo anasema kwamba tunapaswa kuimba na kushangilia katika mioyo yetu. Mwandishi wa Waebrania aliagiza, *“Basi, kwa njia yake yeye, na tumpe Mungu dhabihu ya sifa daima, yaani, tunda la midomo iliungamayo jina lake.”* (Waebrania 13:15). Huyu mtu wa Mungu aliyevuviwa anasema kwamba tunapaswa kumsifu Bwana kwa matunda ya midomo yetu. Hii ina maana kwamba sisi tunapaswa kutumia sauti zetu tunapomwimbia Bwana sifa. Yeye anataka viumbe vyake vimsifu na si viumbe vyetu. Anataka hivyo ambayo ni hai na mahiri kumsifu Yeye, si vitu visivyokuwa na uhai.

Watu wengine wangejiuliza ni tofauti gani inayoonesha aina ya muziki tunapaswa kuutumia tunapomwabudu Mungu? Hoja ni Bwana anajua anachotaka katika ibada na tunapaswa kufuata anayoyataka. Si suala la kujifurahisha wenyewe au watu kwa ujumla. Badala yake Bwana ndiye anayepaswa kupendezwa. Paulo alisema, *“Imekuwaje, basi? Nitaomba kwa roho, tena nitaomba kwa akili pia; mtaimba kwa roho, tena nitaimba kwa akili pia.*” (1 Wakorintho 14:15).

Kulingana na historia ya kiulimwengu muziki wa sauti ulitumiwa tu na kanisa la karne ya kwanza katika ibada yake kwa Mungu, lakini mamia ya miaka ya baadae viongozi wa dini wa siku hizo walianzisha muziki wa ala katika ibada. Imekubaliwa na kutumiwa na wengi tangu wakati huo, lakini ikiwa tunataka kumwabudu Bwana kwa nini tusimwabudu kama alivyobainisha yaani katika roho na katika kweli? (Yohana 4:24).

Kuna sababu nyingi zinazotolewa kwa nini muziki wa vyombo unapaswa kutumika katika ibada, lakini hakuna hata moja kati ya hizo inayoegemezwa kwenye neno la Mungu ila ni mantiki tu na akili ya kawaida.

Ukristo ni dini ya pekee katika hilo, kwa kuwa ni dini ya uimbaji. Kuimba kunaweza kutumiwa kumsifu Bwana, kuimba ni mojawapo ya mambo yanayofanyika kiushirika. Ikiwa uko katika harakati za kuanzisha kusanyiko la kanisa la Bwana, wanaume wanapaswa kuchagua mmoja kutoka miongoni mwao wale ambao wanaweza kuliongoza kundi katika nyimbo za kiroho na kimaandiko.

Wakati wa kuchagua nyimbo, kiongozi anatakiwa kuchagua zile ambazo zinafahamika, na kwa vyovyote vile zinapaswa kuwa za kimaandiko. Na hivyo ujumbe ndani yao unapaswa kupatana na mafundisho ya neno la Mungu. Inawezekana kuimba kimakosa pamoja na kuhubiri au kufundisha kimakosa. Kwa kweli unapoimba kimakosa unafundisha makosa, mtu anapoimba anapaswa kuutafakari ujumbe wa wimbo, na anapaswa kushiriki katika uimbaji akitambua kwamba anawafundisha wale walio karibu naye.

Kuhusu idadi ya nyimbo zilizotumiwa, hakuna idadi iliyowekwa. Jukumu hilo ameachiwa kiongozi w nyimbo, na inaweza kutegemea muda uliopo. Kawaida kiongozi anasimama mbele ya kundi. Katika upande wa magharibi wa ulimwengu, ndugu kawaida wanatumia vitabu vya nyimbo vilivyo na nota na ikiwa mtu anajua nota anaweza kusoma muziki na unaweza kuongoza ipasavyo na kwa usahihi. Wakati mwingine anaweza kutumia ishara za mikono ili kuelekeza uimbaji. Katika sehemu nyingine za dunia mifumo tofauti inaweza kutumika, na kiongozi wa nyimbo anaweza kuwa na maneno ya nyimbo tu, ili apate kutumia nyimbo alizojifunza hapo awali.

Kusanyiko zima linapaswa kushiriki katika uimbaji. Huenda usiwe muimbaji bora zaidi ulimwenguni, lakini ikiwa ni kutoka moyoni, lazima uwe mzuri kwa Bwana. Hatupaswi kuimba kwa kujiburudisha, ingawa tunaweza kupenda kuimba, na tunaweza kujengwa nao. Hatupo ili kuwa na solo, kwaya, na vikundi maalum, lakini badala yake tunapaswa kuwa na uimbaji wa kusanyiko, kwa sababu kanisa linapaswa kuungana pamoja katika kumsifu Mungu. Wakati fulani ikiwa uimbaji wetu si mzuri kama inavyopaswa kuwa, tunaweza kupanga kukutana na kuwa na vipindi maalum vya mafunzo. Huenda tukahitaji kujifunza baadhi ya nyimbo, na hilo linaweza kufanywa kurudia tena na tena. Hatujaribu kuuvaa utendaji, bali tunataka kufanya kazi nzuri kwa kuwa uimbaji wetu unaelekezwa kwa Bwana, nasi hatutaki kuweka tu chochote tofauti na maagizo yake.

Kulingana na Biblia wanawake wanaweza kushiriki kuimba katika kusanyiko, lakini hakuna amri au mfano unaowaruhusu kuongoza uimbaji hadharani. Tutajadili nafasi ya mwanamke katika kanisa baadaye kidogo.

Tunatakiwa kuwatia moyo vijana wetu wajifunze kuongoza kuimba. Hili linaweza kufanyika kwa kuwapa nafasi ya kuongoza katika ibada za jioni au jumatano jioni au siku nyingine yoyote kuwa na darasa maalum ambalo wanaweza kufanya mazoezi kwa maelekezo ya ndugu kadhaa wenye umri mkubwa (Wazee).

## Somo la 14

# JINSI YA KUTOA

Sasa tunaendelea na mada yetu ya jumla ya **Jinsi ya Kuanza Kanisa la KristoMahali Ulipo.** Pamoja na hayo mawazo katika akili, tungependa kuzungumza na wewe kuhusu jinsi ya kutoa.

Ikiwa una nia ya kuanzisha kusanyiko la kanisa la Bwana mahali ulipo, lazima uwe na mikutano siku ya kwanza ya wiki kwa kusudi la kumwabudu Mungu. Mbali na maombi, kujifunza Biblia, na meza ya Bwana, pia unatakiwa kuwapa fursa ya kutoa mali zao ndugu waliopo, au kutoa mchango ili kusaidia kazi ya Bwana. Kabla hatujaenda katika mchakato wa jinsi ya kufanya hivyo, kwanza tunatakiwa kutambua baadhi ya mistari ya maandiko inayoonesha umuhimu wa kutoa.

Tunajua kwamba Biblia imejaa mafundisho na mifano ya kutoa. Hata Mungu alimtoa Mwanawe kufa msalabani kwa ajili ya dhambi ya ulimwengu (Yohana 3:16), na Kristo alitoa uhai wake ili mwanadamu apate nguvu ya kuokolewa (1 Yohana 4:14). Tunaweza kuwa na mifano gani mkuu zaidi kuliko huo? Lakini tunaweza kumpa nini Bwana? Kiasi gani tunaweza kutoa?

Katika tukio fulani Yesu alipojua kwamba kijana mmoja alikuwa akitilia mkazo sana juu ya mali, alimwambia kwamba kama angeokoka angeenda akauze alicho nacho na kuwapa maskini (Mathayo 20:21). Luka aliandika kwamba sisi tunapaswa kukumbuka maneno ya Yesu aliposema, *"Katika mambo yote nimewaonyesha ya kuwa kwa kushika kazi hivi imewapasa kuwasaidia wanyonge, na kuyakumbuka maneno ya Bwana Yesu, jinsi alivyosema mwenyewe, Ni heri kutoa kuliko kupokea."* (Matendo 20:35). Mtume Paulo aliwaandikia Wakristo wa Korintho, *"Kwa habari ya ile changizo kwa ajili ya watakatifu, kama vile nilivyoamuru makanisa ya Galatia, nanyi fanyeni vivyo. Siku ya kwanza ya juma kila mtu kwenu na aweke akiba kwake, kwa kadiri ya kufanikiwa kwake; ili kwamba michango isifanyike hapo nitakapokuja;"* (1 Wakorintho 16:1,2).

Ukweli kadhaa umeoneshwa katika taarifa ya Paulo. Kwanza inabainisha siku ambayo utoaji utafanyika, na hiyo ni siku ya kwanza ya juma. Tunasoma katika Matendo 20:7 ambapo wanafunzi

walikusanyika kwa ajili ya ibada, na kwa kufanya hivyo walishiriki katika ibada ya meza ya Bwana, kuwa pamoja siku ya kwanza ya juma kwa ajili ya kuabudu, kwa kawaida huu ungekuwa wakati mzuri kwa watu wa Bwana kutoa mali zao.

Pili, alisema kila mtu ashiriki, yaani ikiwa walikuwa wanefanikiwa wiki moja kabla. Ikiwa mtu hajapata, kwa kawaida hana chochote anachoweza kutoa. Katika jambo hili mtu haipasi kuona aibu kwa kutokutoa kwa kuwa Bwana hamtazamii kutoa. Ikiwa umepata unapaswa kutoa. Kutokutoa itakuwa ni namna ya kumnyang'anya Bwana kile ambacho ni mali yake.

Tatu, anasema kwamba wanapaswa kuweka akiba. Leo sisi kwa kawaida tunafikiria katika suala la kutoa mchango wa kifedha, lakini kulikuwa na nyakati ambazo watu wa Bwana hawakuwa na pesa ambayo wangeweza kutoa, lakini waliweza kutoa wanyama, mboga, matunda, n.k, na ambavyo viliweza kutumika kusaidia kazi ya Bwana. Hata leo, katika baadhi ya sehemu za dunia Wakristo wengine wanaweza wasiwe na pesa, lakini wanaweza kuwa na vitu vingine vya kutoa. Kwa mfano wanaweza kumsaidia mhubiri kwa kutoa kuku, mayai, au vitu vingine. Hiyo bila shaka itahesabiwa kama mchango.

Nne, alisema kwamba walipaswa kutoa kama walivyofanikiwa. Yaani watoe sehemu ya walichokuwa wamepata haijalishi ni kiasi gani kitawekwa akiba kwa kila mtu, lakini kila mmoja anajua ni kiasi gani kinachopaswa kuwa. Wayahudi walitoa sehemu ya kumi ya mapato yao na kwa kutilia maanani mapato yao yote ya dhabihu za ziada, walitoa zaidi ya sehemu ya kumi. Sisi tuna tumaini la uzima wa milele. Hakika tusingetoa chini ya wale walioishi chini ya sheria ya zamani (Agano la Kale).

Tano, utoaji katika tukio hili ulipaswa kutumiwa kusaidia kushughulikia baadhi ya mahitaji ya watakatifu, na Paulo alisema kuwa walipaswa kutoa mapema ili kila kitu kiwe tayari atakapofika. Ikiwa watu wa Mungu watatoa inavyopaswa, mahitaji ya kazi yake yanaweza kushughulikiwa bila tatizo lolote. Hakika Bwana hatarajii watu wa ulimwengu kusaidia kazi yake. Mchango kutoka kwa mtu ambaye sio Mkristo hautakataliwa lakini hata hivyo wasiombwe.

Baadaye Paulo aliwaandikia tena Wakristo wa Korintho, na kusema, *"Lakini nasema neno hili, Apandaye haba atavuna haba; apandaye kwa ukarimu atavuna kwa ukarimu. Kila mtu na atende kama alivyokusudia moyoni mwake, si kwa huzuni, wala si kwa lazima; maana Mungu humpenda yeye atoaye kwa moyo wa ukunjufu."* (2 wakorintho 9:6,7).

Tafadhali zingatia kwamba Paulo anafundisha dhana ya kutoa kwa kutumia kielekezo cha kupanda na kuvuna. Watu wengi wa siku hizo wangefahamu sana kanuni hiyo ilivyo. Wazo ni kwamba kadiri unavyopanda ndivyo unavyovuna; ukipanda kidogo utavuna kidogo. Kanuni hii ni kweli si tu katika kilimo, lakini katika kila eneo lingine la Maisha. Kwa mfano ukimtolea Bwana zaidi, ndipo na yeye atakubariki zaidi. Ikiwa unatoa kidogo unaweza kutarajia malipo kidogo. Bila shaka ikiwa mtu anatoa zaidi kwa madhumuni ya kupokea zaidi, nia yake ni mbaya, na haitamsaidia kitu katika jambo hilo. Lakini ikiwa ni mtu mwaminifu na mnyofu, anampenda Bwana, na anajaribu kweli kufanya mapenzi ya Mungu basi kadiri atoavyo sana, ndivyo atakavyobarikiwa sana.

Wengi hawajabarikiwa kwa sababu wanamdanganya Mungu. Wao ni wabinafsi na hutanguliza mahitaji yao mbele za Bwana. Wanashangaa kwa nini Baba yao hawabariki sana. Mtu lazima akumbuke kumtanguliza Kristo na ufalme wake ndipo mambo mengine yatakuwa yanazidishwa (Mathayo 6:33). Jaribu na uone ikiwa haifanyi kazi.

Paulo alisema tunapaswa kutoa kama tulivyokusudia mioyoni mwetu. Tunajua tulichokichuma, hivyo tunapaswa kuwa tayari tumejiandaa kwa kiasi cha pesa utakachotoa kabla ya wakati wa kutoa; chombo cha mchango kinapopitishwa, tunaweza kutoa. Tukingoja hadi dakika ya mwisho tunaweza kuishia kuweka zaidi ya tulivyokusudia. Kama Paulo alivyosema, tunapaswa kuamua tutatoa nini na kisha tuwe tayari kutoa inavyotupasa kwa wakati ufaao.

Kisha anaseama kwamba utoaji wetu haupaswi kufanywa kwa kinyongo au kwa lazima, bali tunapaswa kutoa kwa furaha. Sisi hatupaswi kuhisi kwamba tunawekwa mahali, au kwamba tumelazimishwa kutoa mchango, bali tunapaswa kutoa kwa shauku na

tunapaswa kuwa na furaha kwamba tunaweza kutoa. Mwandishi anasema kwamba Mungu anampenda mtoaji wa aina hii.

Katika siku ya Bwana lazima mtu mmoja ateuliwe kupitisha chombo cha mchango kwa wale waliohudhuria ibada. Ni vema tendo hili likitanguliwa au kuhitimishwa na maombi ya shukrani kwa baraka zetu za kimwili. Wote wanatakiwa kupewa nafasi ya kutoa, na kisha baada ya ibada wachaguliwe watu wawili katika wanaume wahesabu makusanyo, waweke kumbukumbu yake na labda waziweke katika akaunti ya benki kwa jina la kusanyiko la mahali husika. Mmoja wa washirika wa kiume anapaswa ateuliwe kuwa mweka hazina ili aweze kutunza fedha na kutoa taarifa ya salio kwa kanisa. Fedha zinaweza kutumika kuhubiri injili, kununua vifaa kwa ajili ya kanisa, kuwasaidia maskini, wahitaj, n.k.

Kumbuka kwamba utoaji wetu ni sehemu muhimu sana ya huduma yetu kwa Mungu.

**Somo la 15**

# MADARASA YA BIBLIA

Tumezungumza kuhusu kuwafundisha wengine injili, kuwabatiza ili wawe ndani ya Kristo na namna ya kuabudu. Tutaendelea na mafundisho yetu tukizungumzia madarasa ya Biblia na jinsi ya kuyaendesha.

Tunajua kwamba Bwana ametupa neno lake katika Biblia. Ili kukijua kitabu hicho na kujua mapenzi ya Mungu ni lazima tujifunze binafsi au tusikie kikifundishwa. Kristo aliwaambia mitume kwamba waende na kuhubiri Injili *"Akawaambia enendeni ulimwenguni mwote Mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe"* (Marko 16:15). Paulo alisema (2 Timotheo 2:15) Akasema tena "*Basi imani chanzo chake ni kusikia, na kusikia huja kwa neno la aKristo*" (Warumi 10:17). Mungu alizungumza kutoka mbinguni kuhusu Yesu, *" Alipokuwa katika kusema, tazama, wingu jeupe likawatia uvuli; na tazama, sauti ikatoka katika lile wingu, ikasema, Huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, ninayependezwa naye; msikieni yeye."* (Mathayo 17:5). Katika haya na mengine mengi tunaweza kuona umuhimu wa kusikia na kujifunza neno la Mungu. Na kwa maarifa hayo tunapata kumwamini na kumtii Bwana ili tupate kuokolewa na kuongezwa katika Kanisa Lake.

Bila shaka kuhubiri, kufundisha, na kujifunza binafsi Neno la Mungu ni sawa kwa watu wazima, lakini vipi kuhusu wengine? Vipi kuhusu watoto wa rika tofauti tofauti? Katika elimu ya watu wazima, hotuba hutumika mara nyingi. Hata huko madarasa yao yanakuwa na masomo tofautitofauti na viwango tofautitofauti vya kujifunza. Lakini linapokuja suala la elimu ya watoto wa umri tofauti tofauti madarasani daima hugawanywa katika makundi ya umri tofauti tofauti. Kamwe hakuwezi kuwepo na shule yenye watoto mia kadhaa pamoja katika

viwango vyote vya umri, na wawe na mwalimu atoe maelekezo sawa kwa wote. Ni aina gani ya elimu ingepatikana kwa njia hiyo?

Tunaweza kuona hekima ya madarasa katika shule zetu za kidunia, hivyo kwa nini hatuoni hekima ya kuwa na madarasa ya Biblia? Nimeona katika sehemu nyingi ni vigumu sana katika makusanyiko madogo kukubali wazo la kuwa na madarasa ya Biblia. Wamekutana kwa muda mrefu katika nyumba au vyumba vidogo, wamekuwa na huduma  ya kuimba, sala, na somo la Biblia litolewalo kwa wote waliopo na kwa sababu fulani wengine wanataka kuendelea kufanya hivyo. Lakini hawafikirii juu ya watoto ambao hawawezi kuelewa mhubiri anasema nini! Ikiwa darasa litaweza kupangwa kwa watoto wote kulingana na umri wao, wakati huo pia darasa la watu wazima likiendelea, hiyo itakuwa na manufaa makubwa kwa kila mtu. Masomo yanaweza kutayarishwa kwa wototo na kutolewa kwa kiwango chao hapo watajifunza sana zaidi ya kusikiliza somo ambalo hutolewa kwa watu wazima na wazazi, uhuru wa kulea watoto wadogo pasipo usumbufu, ungeleta umakini wa usikivu katika somo.

Kuhubiri na kufundisha hakutakiwi kuwa aina ya burudani au fursa kwa mtu kuonesha uwezo wake wa kuzungumza. Badala yake kusudi lao ni kuwasaidia wale waliopo wajifunze mapenzi ya Mungu ili waweze kumtii. Kwa kuzingatia hili sisi tunaweza kuona kwa urahisi zaidi thamani ya madarasa kwa watoto na kwa wazazi wao. Imegundulika kuwa katika makusanyiko ambayo kuna idadi fulani ya madarasa ya Biblia, ukweli unaeleweka zaidi katika mazingira ya darasani kuliko katika mahubiri.

Ikiwa kusanyiko litaanzishwa mahali ulipo, kumbuka kuwa na mpango wa darasa la Biblia. Hata kama kundi ni dogo njia bora ya kufanya kazi ni kuwa na saa iliyotengwa kwa ajili ya darasa la Biblia na wakati huowanaume wawe na darasa, wanawake nao wawe na darasa na wapange darasa kwa ajili ya watoto pia. Au wanaume na wanawake wanaweza kuwa na darasa lao pamoja na kama kuna umri tofauti tofauti

wa watoto, wanaweza kugawanywa katika madarasa mawili au zaidi. Kwa kawaida kuwa na madarasa mengi yatategemea mahali ambapo mtakutania. Hata katika ukumbi, madarasa yanaweza kufanyika katika pembe tofauti tofauti za jengo. Nyumbani, madarasa yanaweza kufanyika katika vyumba tofauti.

Jambo jingine ambalo litalazimika kufanyiwa kazi ni walimu wa madarasa tofauti tofauti. Ikiwa hawana uzoefu, wale ambao watajaribu wanaweza kukuza uwezo wao wa kufundisha polepole. Jambo kuu ni kujaribu. Mtu anaweza kuandaa somo katikati ya juma, na kuendelea kujitolea ili mradi awe tayari kufundisha darasa. Maandalizi kiwango cha juu lazima yafanyike katikati ya juma ili walimu wawe tayari kwa darasa siku ya Jumapili na siku zingine zitakazopangwa.

Baada ya masomo, kusanyiko linaweza kukusanyika kwa ajili ya ibada. Labda mmoja wa washirika wa ndani anaweza kufundisha somo, au inaweza kuwa mhubiri wa ndani. Ikiwa hakuna aliyepo kati ya hawa wanaume wanaweza kupeana zamu za kusoma maandiko au kipeperushi cha injili. Mambo yote yanawezekana mahali ambapo kuna hamu na nia ya kumtii Bwana.

Kila aina ya mambo yanaweza kuendelezwa kupitia mpangilio wa madarasa ya biblia, hasa kadiri kusanyiko likuavyo ndivyo haja ya madarasa inavyoongezeka zaidi.

Kuna aina mbalimbali za mada za kutumia. Darasa wanaweza kujifunza Agano la Kale, Agano Jipya, hasa vitabu vya Biblia, mifano ya Kristo, maisha ya Kristo, na injili ya Kristo, uinjilisti, n.k, au mafundisho yanaweza kupangwa katika madarasa kupitia Biblia au kupitia Agano Jipya katika muda wa kipindi fulani.

Madarasa maalum yanaweza kupangwa. Ikiwa una waongofu wapya wanaweza kutaka kuwa na darasa la “Mwongofu Mpya”. Katika hilo darasa unaweza kufundisha juu ya injili, kanisa, maisha ya Kikristo, na mambo mengine ambayo Wakristo wapya wanahitaji kujua ili kuwasaidia wakue kiroho.

Wakati mwingine kuna madarasa ya mafunzo ya kuwapa wanaume, na hasa vijana, nafasi ya kujifunza jinsi ya kuhutubu, kuongoza uimbaji, kuongoza maombi, n.k, kusudi la madarasa kama haya ni kuwatayarisha wanaume hawa kushiriki katika huduma za kawaida katika kanisa. Wazo sio kwamba tunajaribu kuwa wataalam, bali tunataka kujaribu kufanya kazi nzuri, kwani ndivyo inavyofanyika kwa ajili ya Bwana, na kwa sababu anayeshiriki anamwakilisha Bwana na kanisa lake.

Wakati fulani ndugu wanapenda kuwa na darasa kwa watoto wadogo, na kuwauliza ni vitabu vingapi vilivyomo kwenye Biblia, ili kukariri vitabu kusudi waweze kuvitaja kwa majina, kuorodhesha mitume, na kutoa mambo mengine ya Biblia, haya ni mafunzo mazuri kwa ajili yao, nyimbo fulani za watoto hutumiwa mara nyingi katika darasa la aina hii.

Kwa kawaida, katika madarasa yote ya Biblia au Agano Jipya ndicho kitabu cha msingi cha kufundishia. Lakini inaweza kuwa baadhi ya walimu wangetaka kutayalisha muhtasari wa masomo yao na kisha kutoa nakala kwa washiriki wa darasa. Wakati mwingine makusanyiko mengine yanaweza kutumia nyenzo fulani iliyoandaliwa tayari, . ambayo imeundwa ili kusaidia kufafanua baadhi ya mafundisho ya Biblia, lakini katika hali zote mwalimu anapaswa kupitia nyenzo hiyo/hizo kwa uangalifu mkubwa ili kuwa na uhakika kwamba ni kweli ya Mungu pekee ndiyo inayofundishwa.

**Somo la 16**

# JINSI YA KUFANYA UINJILISTI

Kwa kuzingatia mada hii, sasa tutajadili jinsi ya kufanya uinjilisti. Kuanzisha kusanyiko jipya kunahusisha uinjilisti ambao unaeneza kazi ya Kristo. Sisi ni waamini wakuu katika hili, na tunataka wewe pia ulifurahie jambo hilo.

Moja wapo ya njia bora za kuona hitaji la uinjilisti ni kuanza na agizo kuu. baada ya kifo cha Bwana, mazishI na ufufuo wake, muda mfupi tu kabla ya kurudi kwa Baba Mbingun, Yesu alizungumza na mitume wake *"Akawaambia, Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini, atahukumiwa."* (Marko 16:15,16) *"Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari."* (Mathayo 28:19,20) Luka aliandika *" Akawaambia, Ndivyo ilivyoandikwa, kwamba Kristo atateswa na kufufuka siku ya tatu; na kwamba mataifa yote watahubiriwa kwa jina lake habari ya toba na ondoleo la dhambi, kuanza tangu Yerusalemu. Nanyi ndinyi mashahidi wa mambo haya. Na tazama, nawaletea juu yenu ahadi ya Baba yangu; lakini kaeni humu mjini, hata mvikwe uwezo utokao juu."* (Luka 24:46-49) *"Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi."* (Matendo 1:8).

Kutokana na maandiko yaliyotangulia, Bwana alikuwa akisema kuwa injili yake inapaswa kupelekwa ulimwenguni kote, kwa kila taifa la ulimwengu, na kwa kila kiumbe cha kila taifa la ulimwengu wote. Alisema kwamba injili ilipaswa kuhubiriwa kwanza Yerusalemu na

kisha katika Yudea, na hadi Samalia na hatimaye duniani pote. Zaidi ya hayo alisema kwamba atawapa mitume nguvu ya Roho Mtakatifu ili kuwaongoza katika kufanya kazi hii, unaona, waliishi kabla Agano Jipya kutolewa kwa ukamilifu, kwa hiyo Bwana alimtuma Roho Mtakatifu awaongoze katika kweli yote. Hatimaye alitoa Agano Jipya kama tulilo nalo leo na kufanya kusiwepo tena hitaji la mwongozo wa kimiujiza wa Roho Mtakatifu.

Tunaposoma Matendo 2, tunaona kwamba mitume walikusanyika katika mji wa Yerusalemu. Injili ilikuwa haijahubiriwa bado, na kanisa halikuwepo wakati huo. Lakini Roho Mtakatifu alimiminwa juu ya mitume ili kuwaongoza, na kuwawezesha kunena kwa lugha za watu wengine waliokuwepo katika eneo hilo, na kuweza kufanya miujiza. Nguvu hii walipewa ili kuwashawishi watu wajue kwamba hawakuwa walimu wa uwongo bali walikuwa walimu wa kweli kutoka kwa Mungu. Hii ilikuwa siku ya Pentekoste, siku ya kwanza baada ya kufufuka kwa Yesu Kristo, Wayahudi walipokuwa wamekusanyika kutoka duniani kote ili kusherehekea sikukuu. Bwana alichagua wakati huu ili injili ipate kuhubiriwa na matokeo yake watu wapatao elfu tatu walitaka kujua nini wanapaswa kufanya *"Petro akawaambia, Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu…Akawashuhudia kwa maneno mengine mengi sana na kuwaonya, akisema, Jiokoeni na kizazi hiki chenye ukaidi…wakimsifu Mungu, na kuwapendeza watu wote. Bwana akalizidisha kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa."* (Matendo 2:38,40,47). Pamoja na kanisa la Bwana wetu kuanzishwaa huko Yerusalemu, injili ilihubiriwa tena na watu wengi zaidi wakamsifu Mungu.

Badaye tunamwona Filipo akishuka njia kwenda Samaria kuhubiri huo ujumbe wa ajabu wa injili. Wengi waliamini na kubatizwa. Pia, katika Matendo 8 tunasoma kwamba Filipo aliongozwa na malaika wa Bwana kwenda kumhubiria mtu wa kushi. Alifanya hivyo na mtu huyo

alimtii Bwana, na bila shaka alirudi zake nchini kwake kwenda kupanda mbegu ya Kristo katika sehemu hiyo ya ulimwengu (Ethiopia barani Afrika). Kwa hiyo injili ilikuwa ikihubiriwa na kanisa lilianzishwa katika maeneo mengi.

Katika Matendo 9 tunasoma juu ya kuongoka kwa Sauli na tunajua kile alichokifanya katika safari zake mbalimbali za kimisionari. Alipeleka injili kote. Asia na hata Ulaya. Katika Wakolosai 1:23 alisema *"mkidumu tu katika ile imani, hali mmewekwa juu ya msingi, mkawa imara; msipogeuzwa na kuliacha tumaini la Injili mliyosikia habari zake, iliyohubiriwa katika viumbe vyote vilivyo chini ya mbingu; ambayo mimi Paulo nalikuwa mhudumu wake."*. Pia katika Warumi 10:18 *"Lakini nasema, Je! Wao hawakusikia? Naam, wamesikia, Sauti yao imeenea duniani mwote, Na maneno yao hata miisho ya ulimwengu."*. Hebu fikiria hilo! Kipindi cha miaka thelathini baada ya Injili kuhubiriwa kwanza, inasemekana kwamba ujumbe ulikuwa umefikishwa duniani kote! Ndio, kanisa lilikuwa imara katika Yerusalemu, katika Antiokia, Korintho, Efeso, Filipi, Thesalonike, Beroya, Kolosai, na hata Rumi na pia katika maelfu ya maeneo mengi duniani kote kwa wakati huo.

Je hili lilifikaje? Mitume walianza kazi huko Yerusalemu na katika kipindi kilichosalia cha maisha yao walihubiri na walieneza kanisa la Bwana popote walipokwenda. Lakini hawakuweza kufanya yote yaliyohitajika kufanywa. Kwa hiyo waongofu wao waliwasaidia kufundisha. Kulikuwa na Filipo, Stefano, na mamia ya maelfu ya wengine. Wakati wowote mitume, au waongofu wao, walipoingia kwenye sehemu mpya walipohubiri Injili miongoni mwa wale waliosikia huko, wengine waliamini, wakatubu dhambi zao, wakamkiri Kristo kama Mwana wa Mungu, na kubatizwa kwa ondoleo la dhambi zao. Kisha Bwana akawaokoa na kuwaongeza katika kanisa lake na kusanyiko jipya la eneo lilipoanzishwa! Huku Injili ikiendelea kuhubiriwa katika mji na eneo hilo, watu zaidi walimtii Bwana na

kusanyiko liliendele kukua. Baada ya muda Wakristo hao wachanga waliendelea kuhubiri Injili katika majiji, miji na vijiji vinavyowazuzunguka, na makusanyiko zaidi yakaanzishwa huko. Na hivyo hali hiyo iliendelea mpaka kazi ya Kristo ilipoifunika dunia.

Bwana bado anatuamuru, hata leo hii kupeleka Injili ulimwenguni kote. Ikiwa umemtii Bwana basi umeokolewa na wewe ni mshirika wa kanisa lake. Bado huenda kusiwe na kusanyiko la mahali ulipo. Ikiwa sivyo, vipi linaweza kuanzishwa hapo? Kwa mahubiri yako mwenyewe ya Injili kwa watu wanaokuzunguka. Unaweza kuanza na wanafamilia yako na marafiki. Hiyo inaweza kuwa rahisi kwa mwanaume, lakini vipi kuhusu mwanamke au kijana? Katika swala hilo itabidi ufanye mafundisho yako kwa kiwango cha kuongea na mtu mmoja mmoja, na mtu mwingine mzoefu anaweza kuja na kukusaidia kufanya mikutano kadhaa. Ikiwa unataka kweli kanisa la Bwana kuwepo hapo, nina hakika kwamba kitu kinaweza kufanyika ili kusaidia kuwezesha kuwepo hapo, nina hakika kwamba kitu kinaweza kufanyika ili kusaidia kuwezesha kuwepo vipeperushi vya Injili, magazeti na fasihi nyinginezo zaweza kutumiwa kufundishia Injili. Masomo ya aina kadhaa yanaweza kuhusika, na pia madarasa ya Biblia yanaweza kupangwa. Kwa vielelezo na kwa neno la mdomo, tunapaswa kumfundisha kila mwongofu, na watoto wetu wenyewe na vijana wetu, wa wajibu wao binafsi wa kuwa wainjilisti.

Ikiwa neno la Mungu limefundishwa vya kutosha, basi hakika hii itazaa baadhi ya waongofu, na pamoja na waongofu kusanyiko linaweza kuwa imara. Hivyo Wakristo huko wanaweza kuanza kukutana nyumbani, shuleni, ukumbini au hata nje chini ya mti, jambo la msingi waweze kukutana, kuabudu na kuendelea kufundisha neno la Mungu kuwa wainjilisti. Daima tafuta fursa za kufanya hivyo ili uwafundishe wengine. Pamoja na kazi kukua, labda baada ya muda juhudi fulani zinaweza kuwekwa ili kuhubiri Injili katika majiji, miji na vijiji katika eneo hilo.

Kumbuka kwamba Bwana hataki tutosheke na tulicho nacho, bali anataka tuendelee, tukihubiri, tukiongea na kueneza Jambo Lake. Hii ndiyo kazi anayotaka tuifanye. Tunapotii, atakuwa pamoja nasi na kubariki juhudi zetu.

## Somo la 17

# JINSI YA KUPANGILIA

Moja ya mambo muhimu sana, kukumbuka wakati kuanzisha kusanyiko la kanisa ni **jinsi ya kulipangilia**. Kwa hiyo, tunataka kutoa mawazo ya hilo kwa wakati huu.

Kama sisi sote tunavyojua, katika kila kitu ambacho kinaonekana kinaundwa. Fikiria kuhusu shule, biashara, serikali na jeshi. Hivi vyote vinakitu kinachofanana, vimeundwa na kufanya kazi kwa ufanisi kama shirika. Kama pasingekuwa na mpangilio mzuri, wangefanya mambo kwa kuchanganyikiwa, pasingekuwa na tija, na wangeweza kuishi katika kushindwa.

Vivyo hivyo katika dini, lazima kuwe na muundo. Kristo aliahidi kujenga kanisa lake (Mathayo 16:18), na alitimiza ahadi yake kulingana na Matendo 2. Katika kundi kama hili la watu kulikuwa na hitaji la kufanya kazi kwa utaratibu na kwa mpangilio.

Maandiko yanatuambia kwamba Kristo ni kichwa chake (kanisa) (Wakolosai 1:18; Waefeso 1:22,23) na mwili, au kanisa linaundwa na wale wote ambao wamemtii. Ingawa kanisa lipo duniani kote, lakini pia lipo katika namna ya makusanyiko ya mahali-mahali. Kristo bado ni kichwa chake na kusanyiko linaundwa na waliookolewa. Wakati kanisa halina muundo wowote wa kibinadamu, katika kusanyiko mojamoja kuna muundo.

Katika mwanzo wa kusanyiko wanaume ndio wanaoangalia mahitaji na kuhusika na shughuli yoyote ambayo inaweza kujitokeza. Kutoka miongoni mwa washirika, kunaweza pia kuwa na wahubiri, walimu, viongozi wa nyimbo, n.k, kusanyiko linapokua katika hali ya kiroho na idadi, linahitaji kupangiliwa vizuri zaidi. Sasa linaweza kuwa na wanaume wanaoweza kuchaguliwa kuwa wazee na mashemasi, viongozi waliowekwa rasmi.

Kuhusu mambo haya, Paulo alimwandikia Timotheo, *"Ni neno la kuaminiwa; mtu akitaka kazi ya askofu, atamani kazi njema. Basi imempasa askofu awe mtu asiyelaumika, mume wa mke mmoja, mwenye kiasi na busara, mtu wa utaratibu, mkaribishaji, ajuaye kufundisha; si mtu wa kuzoelea ulevi, si mpiga watu; bali awe mpole; si mtu wa kujadiliana, wala asiwe mwenye kupenda fedha; mwenye kuisimamia nyumba yake vema, ajuaye kutiisha watoto katika ustahivu; (yaani, mtu asiyejua kuisimamia nyumba yake mwenyewe, atalitunzaje Kanisa la Mungu?) Wala asiwe mtu aliyeongoka karibu, asije akajivuna akaanguka katika hukumu ya Ibilisi. Tena imempasa kushuhudiwa mema na watu walio nje; ili asianguke katika lawama na mtego wa Ibilisi. Vivyo hivyo mashemasi na wawe wastahivu; si wenye kauli mbili, si watu wa kutumia mvinyo sana,si watu wanaotamani fedha ya aibu. wakiishika siri ya imani katika dhamiri safi. Hawa pia na wajaribiwe kwanza; baadaye waitende kazi ya shemasi, wakiisha kuonekana kuwa hawana hatia. Vivyo hivyo wake zao na wawe wastahivu; si wasingiziaji; watu wa kiasi, waaminifu katika mambo yote. Mashemasi na wawe waume wa mke mmoja, wakiwasimamia watoto wao vizuri, na nyumba zao. Kwa maana watendao vema kazi ya shemasi hujipatia daraja nzuri, na ujasiri mwingi katika imani iliyo katika Kristo Yesu."* (1 Timotheo 3:1-13) Paulo alimwambia Tito *"Kwa sababu hii nalikuacha Krete, ili uyatengeneze yaliyopunguka, na kuweka wazee katika kila mji kama vile nilivyokuamuru; ikiwa mtu hakushitakiwa neno, naye ni mume wa mke mmoja, ana watoto waaminio, wasioshitakiwa kuwa ni wafisadi wala wasiotii. Maana imempasa askofu awe mtu asiyeshitakiwa neno ,kwa kuwa ni wakili wa MUNGU;asiwe mtu wa kujipendeza nafsi yake,asiwe mwepesi wa hasira,asiwe mlevi wala mgomvi,asiwe mpenda mapato ya aibu. bali awe mkaribishaji, mpenda wema, mwenye kiasi, mwenye haki, mtakatifu, mwenye kudhibiti nafsi yake; akilishika lile neno la imani vile vile kama alivyofundishwa, apate kuweza kuwaonya watu kwa*

*mafundisho yenye uzima, na kuwashinda wenye kupinga. Kwa maana kuna wengi wasiotii, wenye maneno yasiyo na maana, wadanganyaji, na hasa wale wa tohara, ambao yapasa wazibwe vinywa vyao. Hao wanapindua watu wa nyumba nzima, wakifundisha yasiyowapasa kwa ajili ya mapato ya aibu."* (tito 1:5-11). Pia ifahamike kuwa wale waliochaguliwa kama wazee wa kanisa wako katika maandiko yanayowaelezea kama maaskofu na wachungaji, (Tito 1:7; 1 Petro 5:1-5; 1 Timotheo 4:14; Waefeso 4:11). Zaidi ya hayo, kwa wazee kuchaguliwa, angalau wanaume wawili lazima watimize sifa hizi, na ndipo kusanyiko liweze kuwaweka ili wahudumu. Katika nafasi hiyo watakuwa chini ya Kristo, wakitawaliwa katika yote wayasemayo na kuyatenda kwa neno la Mungu, watakuwa wana wajibu wa "kulisha kundi" yaani kuhakikisha kwamba washirika wanafundishwa ipasavyo mapenzi ya Mungu, na kwamba wana uongozi wa kiroho ulikomaa.

Kuhusu sifa zinazohitajika kulingana na maandiko ambayo tayari yanaeleweka, isipokuwa mambo matatu, washirika wote wa kanisa wanapaswa kuwa nayo. Mambo matatu ambayo Wakristo wanaweza wasitimize. Mtu hawezi kuchaguliwa kuwa mzee ikiwa ni Mkristo mchanga. Wazee lazima pia wawe na mke mmoja tu, na kuwa na watoto ambao ni Wakristo, hali hiyo inaonesha uwezo wa kutoa uongozi wa kiroho kwa kanisa. Zaidi ya hayo, Wakristo wote wanapaswa kushuhudiwa mema, si wabinafsi si wepesi wa hasira, si walevi, si wapiga watu, watakatifu, wapenda haki.

Wazee wa kusanyiko wanaweza kuhudumu kwenye kundi moja la Wakristo. Hawana mamlaka juu ya makusanyiko mengine. Wala wazee wa kusanyiko linguine lolote hawawezi kuwatawala.

Kwa habari ya mashemasi vivyohivyo wawe wawili au zaidi, wanaume ambao watahudumu chini ya wazee wakiwa wasaidizi au watumishi. Kuna sifa pia, wanazopaswa kuwa nazo. Pia wake zao lazima wawe wanakidhi vigezo fulani.

Kwa ujumla tunafikiri wazee kuwa wanaume wanaotoa mwongozo wa kiroho kwa kusanyiko huku mashemasi wakiangalia mahitaji ya kimwili katika kusanyiko. Katika hatua zake za awali, au katika miaka michavhe ya mwanzo, unaweza kuwepo bila wazee na mashemasi. Kwa kawaida, ingawa litakuwa linaendelea kukua mpango wa Mungu kwa ajili ya ustawi ni kwamba liwe na wazee na mashemasi. Washirika wote wanapaswa kuwapenda na kuwaheshimu viongozi, na wanapaswa kufuata mwongozo wao kama wanavyomfata Kristo.

Kisha kuna wainjilisti au wahubiri. Mhubiri, hata hivyo, si mchungaji wa kanisa wala si yeye anayetawala kanisa. Badala yake, ikiwa kuna wazee, yeye hutumika chini yao. Kama hakuna wazee, basi anafanya kazi pamoja na wanaume wa kusanyiko, inampasa kuwa mnyoofu kimaadili, na lazima ahubiri mafundisho yenye uzima. Kama vile Paulo alivyomwambia mhubiri kijana, Timetheo, *"Basi Roho anena waziwazi ya kwamba nyakati za mwisho wengine watajitenga na imani, wakisikiliza roho zidanganyazo, na mafundisho ya mashetani; kwa unafiki wa watu wasemao uongo, wakichomwa moto dhamiri zao wenyewe;"* (1 Timotheo 4:1,2). Kauli nyingi katika maandiko zinaelekezewa kwa wahubiri ili kuwakumbusha wajiubu na majukumu yao kwa Bwana na wanadamu wenzao katika kutangaza ujumbe wa Mungu. Pia kuna walimu, au walimu wa darasa la Biblia. Hawa wanaweza kuwa wanaume na wanawake. Bila shaka wanawake watafundisha wanawake wenzao na watoto.

Katika kusanyiko, liwe dogo au kubwa, kazi fulani zinapaswa kufanyika. Mtu atatakiwa kuongoza uimbaji, kutakuwa na haja ya mweka hazina, wengine wangepaswa kujaiandaa kwa ajili ya meza ya Bwana, pamoja na kushughulikia mahitaji mengine.

Hivyo kuwa na ufanisi zaidi, na kufanya mambo katika amani na mpangilio mzuri, wanaume wa kanisa lazima wajipange kwa utaratibu katika kusimamia majukumu haya. Katika hali ya ukuaji, na baada ya muda, kila kusanyiko linaweza kuweka wazee na mashemasi. Kanisa

linapaswa kuheshimiwa na kuwatii viongozi wake, mradi tu kama wao ni waaminifu katika neno la Mungu.

## Somo la 18

# MAHALI PA KUKUTANA

Katika somo letu kwa wakati huu tunataka kujadili **mahali pa kukutania.** Kawaida ikiwa kundi la watu linakutana kila juma kumwabudu Bwana, lazima wawe na mahali maalum pa kukutana. Kuna uwezekano wa namna tofauti katika hili, lakini kwanza tuangalie kanisa la kwanza na tuone ni nini wao walifanya kuhusu mahali pa kukutania.

Tunajua kwamba pindi kanisa lilipoanza siku ya Pentekoste katika mji wa Yerusalemu, mitume walihubiri idadi kubwa ya watu, na elfu tatu walimtii Bwana (Matendo 2:41). Hakuna kinachosemwa kuhusu mahali ambapo hili lilifanyika kwamba ni katika eneo la wazi, au katika uwanja, kwenye viwanja vya hekelu, au mahali pengine. Andiko la Matendo 2:42 linasema kwamba waongofu hao *"Na siku zote kwa moyo mmoja walidumu ndani ya hekalu, wakimega mkate nyumba kwa nyumba, na kushiriki chakula chao kwa furaha na kwa moyo mweupe, wakimsifu Mungu, na kuwapendeza watu wote. Bwana akalizidisha kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa."* (Matendo 2:46,47). Katika Matendo tatu tunaona Petro na Yohana wakimponya kiwete aliyekuwa katika Mlango mzuri wa hekalu na hii ilisababisha fursa kwa Petro kuwahubiria watu wengi. Walikusanyika katika ukumbi wa Sulemani katika hekalu, baada ya Petro kuwambia walichopaswa kufanya, tunasoma, *"Lakini wengi katika hao waliosikia lile neno waliamini; na hesabu ya watu waume ikawa kama elfu tano."* (Matendo 4:4). Kwa hiyo kanisa lilikuwa likiongezeka kwa idadi, lakini je ni wapi wafu wote hawa walikutana kwa ajili ya ibada? Labda waliendelea kukusanyika hekaluni, lakini bila shaka hilo lingekuwa na matatizo baadaye, kwa vile walikuwa wakiabudu kulingana na sheria ya Musa bali kwa mafundisho ya Kristo.

Hatufikirii sana hapa kuhusu mahali pa kukutania ili uinjilisti ufanyike. Hilo linaweza kufanyika mahali popote. Kwa mfano, tuna Filipo aliyekutana na mtu kutoka Kushi mahali pa jangwa, alipopata furusa ya kuungana naye katika gari lake, akamfundisha walipokuwa wakiendelea na safari (Mdo 8:26-39). Katika Matendo 9 tunasoma kwamba Anania alikutana na Sauli katika njia iliyoitwa nyoofu, akamwambia kile alichopaswa kufanya ili kumtii Bwana, na kisha akamsaidia katika utiifu wake. Paulo na Sila walimfundisha injili Mlinzi wa gereza wa Filipi na nyumba yake wakiwa gerezani (Matendo 16).

Tunaweza kutaja sehemu nyingine nyingi ambazo Injili ilihubiriwa, kama vile katika masinagogi mbalimbali ambako Paulo mara nyingi alienda kuwafundisha Wayahudi. Tunasoma kwamba Paulo alipokuwa Efeso, *"Akaingia ndani ya sinagogi, akanena kwa ushujaa kwa muda wa miezi mitatu, akihojiana na watu, na kuwavuta katika mambo ya ufalme wa Mungu. Lakini wengine walikaidi, wakakataa kuamini, wakiitukana ile Njia mbele ya mkutano; basi, akaondoka akawaacha, akawatenga wanafunzi, akahojiana na watu kila siku katika darasa ya mtu mmoja, jina lake Tirano. Mambo haya yakaendelea kwa muda wa miaka miwili, hata wote waliokaa Asia wakalisikia neno la Bwana, Wayahudi kwa Wayunani."* (Matendo 19:8-10)

Sasa tunajua kwamba shule lazima ilikuwa na jengo la kukutania, na Paulo alifundisha pale, lakini ukweli unabaki pale pale kwamba hii isingekuwa sehemu ambayo Wakristo wangeabudu, kama vile ambavyo pengine hawakuabudu katika sinagogi, ingawa Paulo alikwenda huko kufundisha mapenzi ya Mungu. Hivyo tunauliza swali tena: watu wa Bwana walikutana wapi kwa ajili ya ibada siku hizo?

Ingawa hatusomi katika Agano Jipya juu ya majengo ya kanisa, Wakristo walikuwa na nyumba zao binafsi katika hizo siku. Paulo alizungumza kuhusu kufundisha hadharani na nyumba kwa nyumba (Matendo 20:20) pia tunasoma kuhusu kufungwa kwa Paulo huku

Rumi, *“Akakaa muda wa miaka miwili mizima katika nyumba yake aliyokuwa ameipanga, akawakaribisha watu wote waliokuwa wakimwendea, akihubiri habari za ufalme wa Mungu, na kuyafundisha mambo ya Bwana Yesu Kristo, kwa ujasiri mwingi, asikatazwe na mtu.”* (Mdo 28:30,31). Kwa ukweli uleule kwamba Paulo alikuwa katika nyumba yake mwenyewe, na alikuwa amefungwa huko kwa miaka miwili, unatuambia kwamba aliweza kuabudu. Paulo pia alizungumza kuhusu kanisa lililokutana katika nyumba ya Prisila na Akila (Warumi 16:5; 1 Wakorintho 16:19), na bila shaka kulikuwa na makusanyiko mengine mengi yaliyokutana nyumbani, kama tunavyosoma katika Filemoni 1:2, Wakolosai 4:15 na Warumi 6:23.

Lakini kanisa la Korintho lilikutana wapi? Vipi kuhusu kanisa la Filipi? Tunajua kwamba Paulo alipoingia katika mji huo. Alimkuta Lidia na watu wa nyumbani mwake nje kando ya mto ambako aliwafundisha na kuwaongoa. Baadaye alimwaongoa mlinzi wa gereza na watu wa nyumbani mwake. Tunajua kwamba kanisa lilikuwa huko, hata kufikia kuwa na wanaume wanaostahili kuwa wazee na mashemasi, kwa sababu Paulo alipoliandikia kanisa la Filipi wakati fulani aliandika barua yake kwa watakatifu wa Filipi, pamoja na wale maaskofu (wazee) na mashemasi. Lakini tena, walikutana wapi kwa ajili ya ibada?

Wakati hakuna tamko katika maandiko ambalo linaonesha kwamba Bwana alikuwa kinyume na kanisa kumiliki majengo kwa ajili ya ibada, wala maandiko hayaelezi juu ya jambo hili. Tunajua kwamba nyakati za Agano la Kale Mungu aliwaagiza watu wake wajenge maskani ambapo angekutana nao. Kisha Sulemani akajenga hekalu huko Yerusalemu, mahali ambako Bwana alikutana na watu wake, lakini Yesu alimweleza Msamalia mwanamke kwamba wakati utafika ambapo Mungu, hatoabudiwa tu katika mlima kule Samaria, au katika Yeruisalemu, bali watu wake wangeweza kuabudu katika roho na kweli popote pale walipo (Yohana 4: 1-30).

Kwa hiyo ni dhahiri kwamba Bwana hakutaka kutilia mkazo juu ya jengo, lisije likageuzwa kuwa hekalu au “mahali patakatifu”. Yeye alijua kwamba Wakristo wangeweza kupanga mahali pa kukutania wenyewe. Ni wazi, maelezo hayakuwa muhimu vyakutosha kwamba Mungu atuwekee sharia hata juu ya jambo hili!

Vipi leo? Kanisa linaweza kukutana wapi? Linaweza kukutana katika nyumba, katika jengo la shule, au katika nyumba ya kukodi. Tena, Bwana anawaachia hilo watu wake. Tunaweza kukutana popote tunapotaka kukutana. Bila shaka, kusanyiko kubwa, hitaji lake la sehemu ya kukutania ni kubwa. Pia kusanyiko kubwa zaidi, linahitaji uwezo mkubwa zaidi wa kifedha kwa ajili ya jengo lake. Linaweza hata kununua mali na nyumba yake ya kukutania.

Lakini kumbuka, daima, nyumba ya kanisa au jengo sio kanisa. Wala si mahali patakatifu. Ni mahali tu ambapo watu wa Bwana wanaweza kukusanyika kwa ajili ya ibada, kuendesha madarasa ya Biblia, n.k. Jengo au mahali pa kukutania si muhimu sana. Watu wanaoabudu humo ndio muhimu. Hakika kanisa likianzia hapo ulipo, mipango inaweza kufanywa kwa ajili ya kuwa na mahali pa kukutana.

## Somo la 19

# MAHALI PA MWANAMKE

Kwa wakati huu tunataka kujifunza swali la nafasi ya mwanamke kanisani. Katika kuzungumza juu ya kuanza kanisa mahali ulipo, naweza kuwa nazungumza na mwanamke au binti. Katika hali hiyo, unaweza kufanya nini? Kama tutakavyoona, wewe unaweza kufanya mengi, lakini kwanza kabisa, hebu tuende kwenye maandiko tuone yanasema nini kuhusu nafasi ya mwanamke katika kanisa.

Katika nyakati hizi za Vuguvugu la ukombozi wa wanawake, kusema chochote kuhusu mwanamke kuwa na mipaka katika kile anachoweza kufanya kunaleta majibu ya chuki. Kuna walio tayari kupinga na kumuona mtu mwenye msimamo huo kuwa ni mtu anayewachukia wanawake, anayewapendelea wanaume, na hii ni kweli katika baadhi ya dini na nyanja nyingine. Baadhi ya marafiki zetu wakidini n.k katika makanisa yao wametoa nafasi kwa wakawake kuwa wachungaji, wahubiri n.k. Lakini sio swali la kile tunachotaka, au tusichotaka, au jinsi ulimwengu unavyoweza kutuchukulia, au majibu yetu katika kusimama kwenye ukweli yanaweza kusababisha nini, bali jambo muhimu zaidi ni nini Biblia inafundisha kuhusu jambo hili. Ni lazima tuwe tayari kukubaliana na maandiko jinsi yanavyosema kuhusu nafasi ya mwanamke katika kanisa.

Tafadhali elewa kwamba Mungu aliunba mwanamume na mwanamke; aliwaumba tofauti, aliwafanya mmoja wakiume na mwingine wa kike; mmoja awe baba na mwingine awe mama. Sasa sisi tunakubali ukweli na majukumu hayo, sivyo? Itakuwa ajabu sana mwanamke kutaka kuchukua nafasi ya mwanaume (kuzalisha) na mwanaume kutaka kuchukua nafasi ya mwanamke (kuzaa) wakitaka kupata mtoto. Mungu alimpa kila mmoja jukumu na hawezi kubadilika, bila kujali wangependa madiliko kiasi gani. Ukweli ni kwamba sisi tunapaswa kufurahia majukumu ambayo Mungu ametupa. Kazi ya mwanaume ni muhimu, lakini pia kazi ya mwanamke ni muhimu. Mmoja hawezi kufanya bila mwingine.

Litakuwa jambo la ajabu kumtaja Mungu kama “Mke” wakati maandiko yanamtaja kuwa ni Baba. Nani angependa kubadilisha

Jukumu la Mariamu la kumzaa yesu? Kwa kweli, haya ni mambo ya kijinga na shetani anafurahi zaidi kuyatumia kama njia ya kuwageuza mwanaume na mwanamke dhidi ya kila mmoja, na wote wawili kupata matokeo ya kuumizwa.

Bila shaka, kuna maeneo mengi ambayo, wanaume na wanawake inapaswa kuzingatiwa sawa sawa,bila tofauti yoyote. Hatuwezi kupingana na ukweli huo, wala hatupingi ukweli kwamba katika sehemu nyingi za dunia, hata miongoni mwa dini kubwa wanawake wananyaswa wanawekwa nyuma na wanachukuliwa zaidi kama watumishi au vitu vya kuchezewa na wanaume kuliko kitu kingine chochote. Katika namna nyingi sana mwanamke hatazamwi hana haki, na hata haruhusiwi kwenda mahali pa ibada pamoja na mume wake na watoto wake. Ni huzuni iliyoje kwa wanadamu kuwavunjia heshima wanadamu wengine kiasi hicho.

Tunapoenda kwenye Biblia na kuwafikiria mwanaume na mwanamke katika mazingira ya Kiroho, tunaona kwamba Mungu amempa kila mmoja majukumu kamili, na kwamba majukumu hayo yana umuhimu sawa. Lakini Mungu hakumweka mwanaume na mwanamke mmoja dhidi ya mwingine. Hajawaweka washindane katika uongozi, uwajibikaji n.k.

Kwa mfano, Yesu alipotoa agizo kuu alilolitoa mwanzoni aliwapa mitume (wote wanaume) kazi ya kwenda hadharani kutangaza injili yake ulimwenguni (Marko 16:15,16), ingawa kulikuwa na wanawake wengi waliojitolea miongoni mwa wafuasi wake. Ilikuwa mitume walioahidiwa uongozi wa Roho Mtakatifu katika kuanzisha na kutoa mwongozo kwa kanisa la kwanza (Mdo 2). Baadaye, Paulo alitoa sifa za watu wanaotakiwa kuwa wazee na mashemasi katika makusanyiko ya mahali pamoja ya kanisa (1 Timotheo 3; Tito 1). Tena, wanaume tu ndio walipaswa kuhudumu katika nafasi hizi.

Sasa je, hii ina maana kwamba Mungu aliwashusha hadhi wanawake katika kanisa, au wanawake kwa ujumla? Sivyo . Kwa kweli kazi ya mwanamke ni muhimu sana, pengine muhimu zaidi kuliko wengi wanavyotambua. Mtu anapodai kuwa mwanamke lazima afanye kila kitu ambacho mwanaume hufanya ili awe muhimu kuna vizazi vinaonekana kinyume na mawazo hayo. Kuwaza hivyo kunapungua

thamani ya mwanamke machoni pa wengi, kwa sababu wanapuuza kabisa kazi muhimu za usawa ambao Mungu amezitenga kwa ajili ya wanawake.

Kuna msemo kwamba "mkono unotingisha kitanda cha mtoto unatawala dunia" yaani mwanamke anapokuwa amezaa watoto wake, anaushawishi mkubwa zaidi kwao katika kuwafunza, na hivyo kupitia watoto wake anaweza kutawala ulimwengu. Kila Waziri Mkuu, Rais, au Kiongozi, alikuwa na mama ambaye alimshawishi sana wakati kumlea. Zaidi zaidi, mama anayelea watoto wake kulingana na Mapenzi ya Mungu yanaweza kuwashawishi wawe wakristo, viongozi na watenda kazi kanisani. Wanaweza kubadilisha ulimengu kuwa bora na wanaweza kubadilisha roho milele. Hakuna kazi kubwa zaidi.

Kweli, mwanamke hawezi kuwa mhubiri, mzee au shemasi katika kanisa. Pia anapaswa akae kimya katika ibada, yaani hapaswi kutwaa mamlaka na kuongoza utumishi hadharani (1 Wakorintho 14:28; 1 Timotheo 2:11,12). Hata hivyo, haimaanishi kwamba yeye hawezi kushiriki katika uimbaji wa kusanyiko au kwamba hawezi kuuliza swali au kuonyesha jambo lolote katika kujifunza Biblia. Lakini ina maana kwamba lazima aheshimu wale wanaosisimia ibada au mkutano.

Paulo aliandika kwa uvuvio wa Mungu akisema, *"Basi napenda wajane, ambao si wazee, waolewe, wazae watoto, wawe na madaraka ya nyumbani; ili wasimpe adui nafasi ya kulaumu."* (1 Timotheo 5:14). Alisema tena *"Vivyo hivyo na wazee wa kike wawe na mwenendo wa utakatifu; wasiwe wasingiziaji, wasiwe wenye kutumia mvinyo nyingi, bali wafundishao mema; ili wawatie wanawake vijana akili, wawapende waume zao, na kuwapenda watoto wao; na kuwa wenye kiasi, kuwa safi, kufanya kazi nyumbani mwao, kuwa wema, kuwatii waume zao wenyewe; ili neno la Mungu lisitukanwe."* (Tito 2:3-5)

Petro alihimiza hivi, *"Kadhalika ninyi wake, watiini waume zenu; kusudi, ikiwa wako wasioliamini Neno, wavutwe kwa mwenendo wa wake zao, pasipo lile Neno; wakiutazama mwenendo wenu safi, na wa hofu. Kujipamba kwenu, kusiwe kujipamba kwa nje, yaani, kusuka nywele; na kujitia dhahabu, na kuvalia mavazi; bali kuwe utu wa moyoni usioonekana, katika mapambo yasiyoharibika; yaani, roho ya upole na utulivu, iliyo ya thamani kuu mbele za Mungu. Maana hivyo*

*ndivyo walivyojipamba wanawake watakatifu wa zamani, waliomtumaini Mungu, na kuwatii waume zao. Kama vile Sara alivyomtii Ibrahimu, akamwita Bwana; nanyi ni watoto wake, mfanyapo mema, wala hamkutishwa kwa hofu yo yote. Kadhalika ninyi waume, kaeni na wake zenu kwa akili; na kumpa mke heshima, kama chombo kisicho na nguvu; na kama warithi pamoja wa neema ya uzima, kusudi kuomba kwenu kusizuiliwe. Neno la mwisho ni hili; mwe na nia moja, wenye kuhurumiana, wenye kupendana kama ndugu, wasikitikivu, wanyenyekevu; watu wasiolipa baya kwa baya, au laumu kwa laumu; bali wenye kubariki; kwa sababu hayo ndiyo mliyoitiwa ili mrithi baraka."* (1 Petro 3:1-9).

Paulo alimlinganisha Kristo na kanisa lake na mume na mke aliposema, *"Enyi wake, watiini waume zenu kama kumtii Bwana wetu. Kwa maana mume ni kichwa cha mkewe, kama Kristo naye ni kichwa cha Kanisa; naye ni mwokozi wa mwili. Lakini kama vile Kanisa limtiivyo Kristo vivyo hivyo wake nao wawatii waume zao katika kila jambo. Enyi waume, wapendeni wake zenu, kama Kristo naye alivyolipenda Kanisa, akajitoa kwa ajili yake;"* (Waefeso 5:22-25).

Sasa kuhusiana na mahali ulipo, mwanamke ana jukumu gani la kufanya? Tuseme wewe ni mwanamke na unataka kuanza kanisani hapo ulipo. Ungependa kujifunza na watu mbalimbali, ukitumaini kwamba mmoja au zaidi watamtii Mungu. Kama mwanamke, umeweza kuwaongoa wanawake wengine, basi mnaweza kukutana na kuabudu pamoja. Mwanaume mmoja au zaidi wakiongoka, itakuwa wajibu wao kuchukua uongozi katika ibada. Mwanamke Mkristo ameruhusiwa na Bwana kufundisha wanawake na watoto, hadharani au faraghani (Matendo 18:26). Anaweza bila shaka kuwafundisha wanaume na wanawake faraghani, na kupitia juhudi zake kusanyiko la kanisa la Bwana linaweza kuanzishwa.

### Somo la 20

## JINSI YA KUSAIDIA WAHUBIRI

Katika somo hili tutajadili jinsi ya kusaidia wahubiri. Ukianzisha kusanyiko mahali ulipo, punde tu au baadaye ninyi ndugu mtakabaliwa na swala la namna ya kumsaidia mhubiri wa kusanyiko, utafanya nini juu ya jambo hilo? Paulo aliwaandikia Wakristo wa Korintho, *"Je! Mimi si huru? Mimi si mtume? Mimi sikumwona Yesu Bwana wetu? Ninyi si kazi yangu katika Bwana? Kwa maana ikiwa mimi si mtume kwa wengine, lakini ni mtume kwenu ninyi; kwa maana ninyi ndinyi muhuri ya utume wangu katika Bwana. Hilo ndilo jawabu langu kwa wale wanaoniuliza. Je! Hatuna uwezo wa kula na kunywa? Hatuna uwezo kuchukua pamoja nasi mke aliye ndugu, kama wao mitume wengine, na ndugu wa Bwana, na Kefa? Au je! Ni mimi peke yangu na Barnaba tusio na uwezo wa kutokufanya kazi?*

*Ni askari gani aendaye vitani wakati wo wote kwa gharama zake mwenyewe? Ni nani apandaye mizabibu asiyekula katika matunda yake? Au ni nani achungaye kundi, asiyekunywa katika maziwa ya kundi?*

*Je! Ninanena hayo kwa kibinadamu? Au torati nayo haisemi yayo hayo? Kwa maana katika torati ya Musa imeandikwa, Usimfunge kinywa ng'ombe apurapo nafaka. Je! Hapo Mungu aangalia mambo ya ng'ombe? Au yamkini anena hayo kwa ajili yetu? Naam, yaliandikwa kwa ajili yetu; kwa kuwa alimaye nafaka ni haki yake kulima kwa matumaini, naye apuraye nafaka ni haki yake kutumaini kupata sehemu yake. Ikiwa sisi tuliwapandia ninyi vitu vya rohoni, je! Ni neno kubwa tukivuna vitu vyenu vya mwilini? Ikiwa wengine wanashiriki uwezo huu juu yenu, sisi si zaidi?*

*Lakini hatukuutumia uwezo huo; bali twayavumilia mambo yote tusije tukaizuia Habari Njema ya Kristo. Hamjui ya kuwa wale wazifanyao kazi za hekaluni hula katika vitu vya hekalu, na wale waihudumiao madhabahu huwa na fungu lao katika vitu vya madhabahu? Na Bwana vivyo hivyo ameamuru kwamba wale waihubirio Injili wapate riziki kwa hiyo Injili. Lakini mimi sikutumia mambo hayo hata moja. Wala siyaandiki hayo ili iwe hivyo kwangu*

*mimi; maana ni heri nife kuliko mtu awaye yote abatilishe huku kujisifu kwangu. Maana, ijapokuwa naihubiri Injili, sina la kujisifia; maana nimewekewa sharti; tena ole wangu nisipoihubiri Injili! Maana nikiitenda kazi hii kwa hiari yangu nina thawabu; ila ikiwa si kwa hiari yangu, nimeaminiwa uwakili. Basi thawabu yangu ni nini? Ni hii, ya kuwa nihubiripo, nitaitoa Injili bila gharama, bila kutumia kwa utimilifu uwezo wangu nilio nao katika Injili."* (1 Wakorintho 9: 1-18) katika jambo hila, Paulo anaonyesha uhuru aliokuwa nao kama mhubiri, mtume na kama mtumishi wa Bwana kuwa angeweza kupokea msaada kutoka kwa ndugu kwa ajili ya kazi yake ya kuhubiri, lakini hii hakufanya hivyo. Kutokana na hali iliyokuwepo alihisi kuwa isingekuwa vema. Hata hivyo kulikuwa na matukio mengi ambayo yalimfanya akubali kusaidiwa na kanisa. Akiwaandikia wakristo wa kanisa la Filipi, alisema, *"Nanyi pia, ninyi wenyewe mnajua, enyi Wafilipi, ya kuwa katika mwanzo wa Injili, nilipotoka Makedonia, hakuna kanisa lingine lililoshirikiana nami katika habari hii ya kutoa na kupokea, ila ninyi peke yenu. Kwa kuwa hata huko Thesalonike mliniletea msaada kwa mahitaji yangu, wala si mara moja. Si kwamba nakitamani kile kipawa, bali nayatamani mazao yanayozidi kuwa mengi, katika hesabu yenu. Lakini ninavyo vitu vyote na kuzidi, tena nimejaa tele; nimepokea kwa mkono wa Epafrodito vitu vile vilivyotoka kwenu, harufu ya manukato, sadaka yenye kibali, impendezayo Mungu."* (Wafilipi 4:15-18).

Paulo anayonyesha kwamba ni haki kwa mtenda kazi kulipwa ujira wake. Anatoa kielelezo kwa kusema kwamba mkulima, mtunza shamba la mizabibu, na mchungaji wa mifugo wanaishi kutokana na wanavyozalisha katika utendaji wao. Pia anawakumbusha wasomaji jinsi makuhani walivyoshiriki dhabibu zilizoletwa madhabahuni. Anahitimisha kwa kusema kwamba wale wahubirio injili waishi kwa injili. kwa maneno mengine ni kwamba, mhubiri anapaswa kusaidiwa katika kazi yake.

Katika tukio linguine, Paulo aliandika, *"Kwa maana andiko lasema, Usimfunge kinywa ng'ombe apurapo nafaka. Na tena, Mtenda kazi astahili ujira wake."* (1 Timotheo 5:18). Katika jambo hili alikuwa anaonyesha kwamba mzee aliyetumia muda wake wote katika kazi ya

Bwana alistahili hesima mara dufu. Ni kweli kwamba huduma inaweza kuwa inatolewa bila malipo kwa kuwa wakati mwingine anayefanya kazi anaweza kuwa na msaada kutoka chanzo kingine, lakini hakika hakuna ubaya kwa kanisa kutoa ujira kwa mtu anayetumia muda wake wote kwa kazi ya Bwana. Hata kama mtu anafanya kazi ya muda fulani tu kanisani, anaweza kupata msaada kwa ajili ya juhudi zake.

Ni ukweli usiopingika kwamba kuna waajiriwa leo, kama walivyokuwepo daima. Hawa ni wale wanaofanya kazi kwa ajili ya mshahara tu, sio kwa sababu wanaamini wanachokifanya au kwa sababu ya shauku ya kumtumikia Bwana. Hao ndiyo watakaohubiri chochote kile kilichoombwa kihubiriwe ili tu wapate msaada. Yesu aliwaelezea hivi, *"Mtu wa mshahara, wala si mchungaji, ambaye kondoo si mali yake, humwona mbwa-mwitu anakuja, akawaacha kondoo na kukimbia; na mbwa-mwitu huwakamata na kuwatawanya. Yule hukimbia kwa kuwa ni mtu wa mshahara; wala mambo ya kondoo si kitu kwake."* (Yohana 10:12,13)kwa maneno menginge, mwajiriwa si mwaminifu wala mkweli, haaminiki kabisa katika kile anachokifanya. Anafanya kazi kwa ajili ya pesa tu na sio kwa ajili ya kuendeleza kazi ya Bwana. Ni juu ya kanisa la mahali pamoja kuwa na tahadhari na aina hii ya wahubiri kwa sababu wanaweza kuleta madhara makubwa kanisani na katika jumuiya.

Sasa, tuchukulie unafikiri kumsaidia mhubiri. Unafanyaje kuhusu kumchagua huyo mtu? Anaweza kuwa ndani ya kusanyiko au anaweza kutoka sehemu nyingine ya nchi. Je, utamsaidia mtu huyo kwa muda mfupi au kwa muda wote? Maana yake ni kwamba, utampa msaada kwa sehemu au msaada kamili? Kama hamna kiasi cha kutosha katika kusanyiko lenu, mnaweza kuomba msaada kutoka katika kusanyiko au makusanyiko mengine angalau mwanzoni.

Je unataka mhubiri kijana au mhubiri mzee? Je, unataka mtu ambaye hajaoa au aliyeoa na mwenye familia? Unataka mtu mwenye uzoefu? Uzoefu kiasi gani? Ingekuwa vizuri kumchunguza ameishi wapi, amefanya kazi gani, n.k Je, ni Mkristo mwaminifu? Analipa madeni yake? Ni mwadilifu? Na mambo kama hayo.

Pia itakuwa vizuri kumsikia akihubiri kabla ya kufanya chaguo la mwisho. Yeye ni mhubiri wa aina gani? Je, anaweza kuendana na watu

katika kusanyiko? Je, ni mtu anaepokea ushauri? Je, ana uwezo wa kuwaongoa watu kuwaleta kwa Kristo? Vipi kuhusu mafundisho yake, amesimama katika kweli? Unahitaji kujua anasimama wapi kwenye masuala mbalimbali ya kimafundisho.

Pia inatakiwa kujua atahitaji msaada kiasi gani kwa ajii yake na familia yake? Ikiwa mnaweza kumsaidia na mnaiona kazi yake inaendana na matarajio yenu kulingana na kile ambacho Biblia inafundisha, basi mnaweza kuendelea.

Inatakiwa kuonyeshwa kuwa msaada kwa ajili ya mhubiri unakuwa wa maridhiano kutokana na busara za kusanyiko. Hapaswi kuwa na hali ya kuegemea upande mmoja. Asife njaa mhubiri, lakini pia hapaswi kulipwa zaidi ya wakristo wenyeji katika vipato vya zao.

## Somo la 21

# JINSI YA KUWASAIDIA WENYE UHITAJI

Tunapoendelea na mafundisho yetu tufikiri juu ya jambo linguine linalohusisha kusanyiko la mahali pamoja ambalo ni **jinsi ya kuwasaidia wenye uhitaji.**

Tunajua kwamba watu wote wanamhitaji Bwana kwa maana ya kwamba wanahitaji kuokolewa katika dhambi zao. Lakini mara kusanyiko linapoanzishwa na huanza kukua, wakati mwingine kunakuwa na washirika ambao wanakuwa na mahitaji ya kimwili. kunaweza pia kuwa na watu katika mji ambao wanakabiliwa haswa na mambo magumu katika maisha yao, halafu yakasababisha mahitaji ya dharura. wakati kanisa lina kazi ya msingi ya kuhubiri injili, bado linaundwa na wanadamu na linashughulika na wanadamu nje ya kanisa. Kwa hiyo, haliwezi kufumba macho yake kwa kutojali matatizo ya kimwili ambayo linaweza kusaidia.

Yesu alisema, *"Hapo atakapokuja Mwana wa Adamu katika utukufu wake, na malaika watakatifu wote pamoja naye, ndipo atakapoketi katika kiti cha utukufu wake; na mataifa yote watakusanyika mbele zake; naye atawabagua kama vile mchungaji abaguavyo kondoo na mbuzi; atawaweka kondoo mkono wake wa kuume, na mbuzi mkono wake wa kushoto.*

*Kisha Mfalme atawaambia wale walioko mkono wake wa kuume, Njoni, mliobarikiwa na Baba yangu, urithini ufalme mliowekewa tayari tangu kuumbwa ulimwengu; kwa maana nalikuwa na njaa, mkanipa chakula; nalikuwa na kiu, mkaninywesha; nalikuwa mgeni, mkanikaribisha; nalikuwa uchi, mkanivika nalikuwa mgonjwa, mkaja kunitazama; nalikuwa kifungoni, mkanijia.*

*Ndipo wenye haki watakapomjibu, wakisema, Bwana, ni lini tulipokuona una njaa, tukakulisha, au una kiu tukakunywesha? Tena ni lini tulipokuona u mgeni, tukakukaribisha, au u uchi, tukakuvika? Ni lini tena tulipokuona u mgonjwa, au kifungoni, tukakujia? Na Mfalme atajibu, akiwaambia, Amin, nawaambia, kadiri mlivyomtendea mmojawapo wa hao ndugu zangu walio wadogo, mlinitendea mimi.*

*Kisha atawaambia na wale walioko mkono wake wa kushoto, Ondokeni kwangu, mliolaaniwa, mwende katika moto wa milele, aliowekewa tayari Ibilisi na malaika zake; kwa maana nalikuwa na njaa, msinipe chakula; nalikuwa na kiu, msininyweshe; nalikuwa mgeni, msinikaribishe; nalikuwa uchi, msinivike; nalikuwa mgonjwa, na kifungoni, msije kunitazama.*

*Ndipo hao pia watajibu, wakisema, Bwana, ni lini tulipokuona wewe una njaa, au una kiu, au u mgeni, au u uchi, au u mgonjwa, au u kifungoni, tusikuhudumie? Naye atawajibu, akisema, Amin, nawaambia, Kadiri msivyomtendea mmojawapo wa hao walio wadogo, hamkunitendea mimi. Na hao watakwenda zao kuingia katika adhabu ya milele; bali wenye haki watakwenda katika uzima wa milele."* (Mathayo 25:31-46).

Kama umesoma umesoma vitabu vya Mathayo, Marko, Luka Na Yohana, vitabu vya Agano Jipya, utajua kwamba Yesu alikuwa na huruma na alikuwa tayari kuwasaidia wale waliokuwa na magonjwa na matatizo mengine ya kimwili. Nadhani tunaweza kuona kutoka katika andiko ambalo tumesoma hivi punde kwamba Yesu alikuwa na watu wake pia wenye huruma na wenye kuwasikitikia wanaoumia. Anasema kwamba kwa kuwasaidia wale ambao wanauhitaji, pia tunamsaidia Yeye (Kristo). Kwa upande mwingine, ikiwa tutawapuuza wale wanaotegemea huruma na ukarimu wetu, tunamkataa Kristo mwenyewe. Kama tulivyoona kutoka katika usomaji wetu, hatima ya roho zetu itategemea jinsi sisi tunavyoguswa na wahitaji wanaotuzunguka.

Katika tukio la kuanzishwa kwa kanisa kumbukumbu inaonyesha kwamba wayahudi walikuwa wamekuja kutoka duniani kote ili kusherehekea sikukuu ya Pentekoste. Injili ilihubiriwa na siku hiyo yapata watu elfu tatu walimtii Bwana. Waongofu hawa wapya waliendelea kujifunza zaidi ujumbe wa Kristo, na kuwa na ushirika. Baadhi yao walianza kuhitaji msaada wa mahitaji ya kila siku. Ndugu wenyeji waliitikia. Kumbukumbu inasema, *"Na jamii ya watu walioamini walikuwa na moyo mmoja na roho moja; wala hapana mmoja aliyesema ya kuwa kitu cho chote alicho nacho ni mali yake mwenyewe; bali walikuwa na vitu vyote shirika. Na mitume wakatoa*

*ushuhuda wa kufufuka kwake Yesu kwa nguvu nyingi, na neema nyingi ikawa juu yao wote. Wala hapakuwa na mtu mmoja miongoni mwao mwenye mahitaji; kwa sababu watu wote waliokuwa na viwanja au nyumba waliviuza, wakaileta thamani ya vitu vile vilivyouzwa, wakaiweka miguuni pa mitume; kila mtu akagawiwa kwa kadiri ya alivyohitaji."* (Matendo 4:32-35) katika hali ya kawaida wakristo wasingeuza ardhi na nyumba zao na kugawana kwa hiari miongoni mwao , lakini hii ilikuwa hali maalum. Wale waliokuwa na ardhi wakauza nao wakagawana na wasiokuwa na kitu.

Tunasoma zaidi kuhusu mwongozo kwa Wakristo wahitaji wa wakati huo,*" Hata siku zile wanafunzi walipokuwa wakiongezeka hesabu yao, palikuwa na manung'uniko ya Wayahudi wa Kiyunani juu ya Waebrania kwa sababu wajane wao walisahauliwa katika huduma ya kila siku. Wale Thenashara wakawaita jamii ya wanafunzi, wakasema, Haipendezi sisi kuliacha neno la Mungu na kuhudumu mezani. Basi ndugu, chagueni watu saba miongoni mwenu, walioshuhudiwa kuwa wema, wenye kujawa na Roho, na hekima, ili tuwaweke juu ya jambo hili; na sisi tutadumu katika kuomba na kulihudumia lile Neno."* (Matendo 6:1-4). Kulikuwa na mitume kumi na wawili tu, wakati kulikuwa na wanafunzi wengi. Nguvu ya roho Mtakatifu ilikuwa imetolewa kwa mitume kufanya kazi fulani. Walipoonyesha kujali kuhusu mahitaji ya kimwili ya watu, kulikuwa na wengine ambao wangeweza kufanya kazi hiyo wakati mitume wanatumia muda wao katika kufundisha neno kwa wale waliokuwa na njaa ya **kweli.**

Katika 1 Wakorintho 16:1,2 tunamwoona Paulo akichukua makusanyo kutoka kwa Ndugu wa Galatia na korintho kwa ajili ya watakatifu walio maskini kuleYerusalemu. Baadaye aliandika kwamba mahali palipokuwa na wajane katika kusanyiko, watu wa familia zao wanapaswa kuwatunza. Lakini ikiwa mjane hakuwa na mtu wa kumsaidia, hawezi kujitafutia mahitaji yake mwenyewe, ikiwa alikuwa na umri wa miaka sitini au zaidi, na alikuwa mwaminifu, basi kanisa lilipaswa kumsaidia (1Timotheo 5). Lakini Paulo pia aliweka kanuni ambayo wote walipaswa kuizingatia kabla ya kuligeukia kanisa kwa ajili ya msaada wa kimwili *"Lakini mtu ye yote asiyewatunza walio*

*wake, yaani, wale wa nyumbani mwake hasa, ameikana Imani, tena ni mbaya kuliko mtu asiyeamini."* (1Timotheo 5:8). Katika tukio linguine Paulo alisema "ikiwa mtu hataki kufanya kazi, basi asile chakula (Wathesalonike 3:10).

Sasa katika kusanyiko la mahali Pamoja, vijana kwa wazee, wachache au wengi, kanisa linapaswa kujaribu kuwasaidia wale walio na uhitaji, na ambao wanastahili msaada,ikiwa ni mzee au kijana wachache au wengi. Hiyo ni Pamoja na yule ambaye hana kazi kwa muda, mtu ambaye alipata ajali, mkristo mwenye deni kubwa la matibabu, mtu ambaye nyumba yake imeungua, n.k. Lakini ndugu wenyeji wa kusanyiko wanaweza kutoa fedha pale wanapokuwa nazo. Washirika wasilitegemee kanisa kusaidia katika mahitaji yao isipokuwa kama kuna dharura. Linapokuja suala la kuita makusanyiko mengine kwa ajili ya msaada wa hitaji fulani, hilo linapaswa kufanywa tu ikiwa ni katika hali ya uzima na kifo, au maafa fulani yaliyojitokeza. Katika matukio ya kuwasaidia washirika, na wasio washirika wakati fulani misaada inatakiwa kuwa kutolwea kwa jina la kanisa, sambamba na maombi ambayo yatawafanya watu katika jamii husika watambue uwepo wa kujali na upendo wa kanisa. Watu binafsi, bila shaka, wanaweza pia kusaidia kibinafsi kwa kadri wawezavyo kufanya hivyo.

## Somo la 22

# JINSI YA KUFANYA KAZI PAMOJA

Kwa kuzingatia maudhui yetu, sasa tutajadili **jinsi ya kufanya kazi pamoja** kama washirika wa kanisa la Bwana.

Kwanza ni lazima tuelewe kwamba Biblia inafundisha umoja kwamba sote tunapaswa kuwa wamoja katika Kristo. Kristo alijenga kanisa, kanisa moja na anataka tuuendeleze mwili huo. Katika (Yohana 17:20 -23). Aliomba kwa ajili ya mitume kwa ajili ya wale ambao wangeongolewa nao, na pia kwa wale wote ambao wangemtii. Alisema *"Wala si hao tu ninaowaombea; lakini na wale watakaoniamini kwa sababu ya neno lao. Wote wawe na umoja; kama wewe, Baba, ulivyo ndani yangu, nami ndani yako; hao nao wawe ndani yetu; ili ulimwengu upate kusadiki ya kwamba wewe ndiwe uliyenituma. Nami utukufu ule ulionipa nimewapa wao; ili wawe na umoja kama sisi tulivyo umoja. Mimi ndani yao, nawe ndani yangu, ili wawe wamekamilika katika umoja; ili ulimwengu ujue ya kuwa ndiwe uliyenituma, ukawapenda wao kama ulivyonipenda mimi.".* Hakuna kitu kizuri zaidi kuliko watu wa Mungu waliounganishwa katika kumtii, yaani kuokolewa, kuwa washirika wa kanisa lake kuvaa jina lake, kuabudu na kufanya kazi pamoja na kuwa waaminifu kwake. Paulo aliwaambia Wakristo wa Korintho, *"Basi ndugu, nawasihi, kwa jina la Bwana wetu Yesu Kristo, kwamba nyote mnene mamoja; wala pasiwe kwenu faraka, bali mhitimu katika nia moja na shauri moja."* (1 Wakorintho 1:10). Daudi alisema zamani za kale *" Tazama, jinsi ilivyo vema, na kupendeza, Ndugu wakae pamoja, kwa umoja."* (Zaburi 133:1).

Kwa kuwa umoja ni mzuri utengano ni mbaya na unaharibu. Kristo alisema, *"Basi Yesu akijua mawazo yao, akawaambia, Kila ufalme ukifitinika juu ya nafsi yake, hufanyika ukiwa; tena mji au nyumba yo yote ikifitinika juu ya nafsi yake, haitasimama."* (Mathayo 12:25). Paulo alilaani mgawanyiko uliokuwapo katika kanisa la Korintho. Aliwauliza washirika *"Basi, maana yangu ni hii, ya kwamba kila mtu wa kwenu kusema, Mimi ni wa Paulo, na, Mimi ni wa Apolo, na, Mimi ni wa Kefa, na, Mimi ni wa Kristo. Je! Kristo amegawanyika? Je!*

*Paulo alisulibiwa kwa ajili yenu? Au je! Mlibatizwa kwa jina la Paulo?".* (1 Wakorintho 1:12-13). Walijua kuwa jibu lilikuwa hapana kwa kila moja ya maswali hayo. Hoja ilikuwa kwamba wanapaswa kumfuata Kristo na sio mwanadamu. Paulo aliwaambia Wakristo wa Rumi, *"Ndugu zangu, nawasihi, waangalieni wale wafanyao fitina na mambo ya kukwaza kinyume cha mafundisho mliyojifunza; mkajiepushe nao. Kwa sababu walio hivyo hawamtumikii Bwana wetu Kristo, bali matumbo yao wenyewe; na kwa maneno laini na ya kujipendekeza waidanganya mioyo ya watu wanyofu."* (Warumi 16:17,18).

Wakati mwingine ndugu hawapatani mtu na mtu katika kusanyiko la mahali pamoja. Hii inaweza kuhusiana na mambo ya mafundisho, lakini mara nyingi matatizo hutokea kwa ajili ya haiba, mambo madogo madogo, husuda, na wivu. Wakati mwingine kunakuwa na hasira juu ya nani atahubiri, nani husikilizwa zaidi, au jambo lingine lisilo muhimu. Hii inahuzunisha, na inadhuru kazi ndani ya kusanyiko. Pia inaumiza taswira ya kanisa kwani wasio washirika wanaona tofauti miongoni mwa Wakristo. Itakuwa vigumu kuwafikia watu pale ambapo washirika wamegawanyika. Bwana anataka tumpende na tupendane, tuthaminiane, tusaidiane,na tuwaombee washirika wote.

Lakini wakati Fulani makusanyiko katika eneo fulani hayapatani. Hawashirikiani na kufanya kazi pamoja, Hawasaidiani katika mikutano ya Injili na kazi nyingine nzuri. Wahubiri mara nyingi wana hatia ya mambo ya aina hii. Ni kana kwamba wanashindana wao kwa wao. Hivi ni vibaya na ni makosa. Kanisa linawezaje kukua ikiwa hisia hizi za ushindani zipo? Badala yake, Bwana anapenda makusanyiko haya na wahubiri kushirikiana, kusaidiana kila mmoja na mwenzake, kuhudhuria mikutano ya kila mmoja inapowezekana, na kushirikiana kwa kila njia inayowezekana. Ni kweli kwamba hakuna mtu katika kusanyiko hata moja linaloruhusiwa kutawala makusanyiko mengine, na kuwaambia nini wanaweza au hawawezi kufanya. Lakini ilimradi kila kusanyiko linaheshimu uhuru wa kusanyiko lingine basi kwa hiyo ni sahihi kabisa waweze kufanya kazi pamoja. Tunaona hili likifundishwa sehemu zote katika Agano Jipya.

Ikiwa tuna tofauti fulani na mshirika mwingine, au na kusanyiko linguine, tunapaswa kumwendea mtu huyo au kusanyiko hilo kwa nia

ya kuondoa tofauti hizo. Ikiwa mgawanyiko ni juu ya swali fulani la kimafundisho, tunapaswa kwenda kwenye Biblia ili tuone inafundisha nini. Tunapaswa kufanya hivi kwa maombi na kwa shauku ya kuwa na haki mbele za Mungu na kufanya yote tuwezayo ili kudumisha umoja kati ya watu wa Bwana. Hatupaswi kamwe kukasirikia jambo na kutafuta kumuumiza mtu au kupinga kwa makusudi kusanyiko lingine. Hatupaswi kuondoka na kumwacha Bwana na kanisa juu ya kila jambo dogo linalojitokeza. Jambo la msingi kwetu tunapaswa kusuluhisha tatizo lolote linapojitokeza na kuwa katika amani, kiroho.

Katika kusanyiko tunapaswa kuwatia moyo washirika kila wakati kwa kufanya kazi pamoja na kufanya kazi na ndugu wengine ndani ya eneo husika. Sisi ni ndugu waume na wake katika Kristo na sisi ni wachache kiidadi ukilinganisha na watu wengine duniani. Tunahitaji kuwa na umoja katika juhudi zetu kwa ajili ya Mungu. Tunapaswa kutambua pia, kwamba tuna kazi kubwa mbele yetu, yaani, kuishi kwa ajili ya Bwana na kupeleka Injili ulimwenguni. Tukiwa na umoja tutakuwa na nguvu za kufanya kazi hiyo. Zaidi ya hayo ni pale tu tunapoungana ndipo Bwana anaweza kuwa nasi tunapojitahidi kufanya mapenzi yake kwa dhati.

Kwa kuwa tunajadili somo hili, nichukue fursa hii kukuuliza ili nipime uelewa wako, ni kuhusiana na umoja. Je, unaamini kwamba watu wote wa dini wana haki ya kuamini kwa namna wanavyotaka, lakini kwa ujumla wao wanapaswa kuwa na umoja waungane kwa maana ya kwamba wote wanadai ni wafuasi wa Kristo? Je, wewe ni mshirika wa kanisa la kimadhehebu? Je, unaweza kusoma kuhusu kanisa lako katika Biblia? Lakini wengi wanaweza kusema “Hayo yote yana tofauti gani, mradi tu wewe ni mwamini wa Kristo?”. Hiyo ndio hoja, ikiwa wewe unamwamini Kristo, hakika utataka kufanya kile ambacho Kristo anataka wewe ukifanye. Katika somo letu tumejadili kuhusu ombi la Kristo, jinsi alivyoomba ili sisi sote tuwe kitu kimoja ndani yake. Pia tumeonesha kutoka katika maandiko kwamba Bwana analaani migawanyiko. Kwa hiyo tunawezaje kumwamini Kristo na kufanya mambo yale yale ambayo yeye aliyakataa? Tunawezaje kumwamini ikiwa sisi si washirika wa Kanisa Lake? Na tunawezaje kwenda mbinguni wakati tunatofautiana na Bwana na sisi wala si

sehemu ya familia yake duniani? Naomba ufikirie upya mambo haya. Sijaribu kusogeza kanisa langu, dini yangu, au kitu kingine chochote, lakini ninajaribu kuhimiza kwamba wote tumtii Bwana na kuwa tu kile anachotaka Bwana tuwe.

Na kwa wale ambao ni Wakristo na washirika wa kanisa la Bwana, ninawaambia pia kwamba hatuwezi kugawanywa katika kusanyiko la pamoja au vinginevyo, na kukubaliwa na Mungu. Anataka sisi sote tuongee kitu kimoja na kufanya kitu kile kile. Anataka tuwe na umoja kama kundi na kuwa mwili mmoja ndani yake, mwili wake wa Kiroho, familia yake.

Kumbuka kwamba Paulo alisema, *"Kwa hiyo nawasihi, mimi niliye mfungwa katika Bwana, mwenende kama inavyoustahili wito wenu mlioitiwa; kwa unyenyekevu wote na upole, kwa uvumilivu, mkichukuliana katika upendo; na kujitahidi kuuhifadhi umoja wa Roho katika kifungo cha amani. Mwili mmoja, na Roho mmoja, kama na mlivyoitwa katika tumaini moja la wito wenu. Bwana mmoja, imani moja, ubatizo mmoja. Mungu mmoja, naye ni Baba wa wote, aliye juu ya yote na katika yote na ndani ya yote."* (Waefeso 4:1 - 6).

Kumbuka kwamba katika kuhubiri na katika mahusiano yetu binafsi, tunapaswa kufanya kazi katika kazi iliyo kuu kuliko zote duniani.

## Somo la 23

# JINSI YA KUSAMEHE

Tutaendelea na mada yetu kuu ya mafunzo, juu ya **Jinsi ya Kuanzisha Kanisa la Kristo Mahali Ulipo**. Ni maombi yangu kwamba, masoomo haya yalete matokeo mazuri ya kusaidia kuanzishwa kwa makusanyiko mapya. Hakika ninakutegemea usaidie katika kazi hiyo. Kama nilivyosema katika matukio kadhaa hata hivyo, huwezi kusaidia mpaka uwe umemtii Bwana wewe mwenyewe. Hilo si gumu kulifanya. Unajua kwamba nimepitia mpango wa Injili wa wokovu mara idadi yoyote ya nyakati. Nimeonesha kwamba Bwana anapenda umwamini Mungu (Waebrania 11:6), utubu dhambi zako au jiepushe nazo (2 Petro 3:9), ukiri imani yako kwa Kristo kama Mwana wa Mungu (Mathayo 10:32), na kisha ubatizwe kwa ajili ya ondoleo la dhambi zako (Matendo 2:38). Ikiwa utafanya hivyo Bwana atakuokoa na kukuongeza kwenye kanisa lake (Matendo 2:47). Kama ni Mkristo na mshirika wa kanisa, unaweza kumwabudu Mungu kila siku ya kwanza ya juma, na usaidie kazi ya Bwana. Kama Mkristo unaweza kuchukua hatua ya kuanza kuanzisha kusanyiko la kanisa mahali ulipo ikiwa hakuna hata moja tayari. Sisi tunatumaini kwamba utafanya hivyo.

Sasa tutaendelea na mfululizo wa masomo yetu kwa kujadili somo muhimu la **jinsi ya kusamehe**.

Kwa kuwa tulikuwa wenye dhambi ilikuwa ni lazima kwa Bwana kusamehe ili tupate kuokolewa. Hata alijitoa mhanga juu ya msalaba ili kufanya wokovu wetu uwezekane. Tunamshukuru Mungu kwa hilo lakini ingawa Bwana ametuokoa kutoka katika dhambi zote zilizopita, sisi ni wanadamu tuko chini ya dhambi na kwa hiyo tunaendelea kuhitaji **msamaha**. Ni lazima pia tuwe tayari kuwasamehe wale wanaotukosea. Tusipojifunza jinsi ya kufanya hivyo na ikiwa hatuko tayari kusamehe, hatuwezi kusamehewa sisi nasi pia. Unaweza kuona jinsi gani somo hili ni la muhimu.

Yesu aliwafundisha wanafunzi wake kuomba *"Utusamehe deni zetu; kama sisi tunavyowasamehe wadeni wetu"* (Mathayo 6:12). Aliendelea kwa kusema, *"kwa maana mkiwasamehe watu makosa yao,*

*Baba yenu wa mbinguni pia atakusamehe. Bali usipowasamehe watu makosa yao wala Baba yenu hatawasamehe ninyi makosa yenu"* (Mathayo 6: 14, 15). Je si ajabu kwamba tunamtarajia Bwana utusamehe, na bado tusiwe tayari kuwasamehe wale wanaotukosea? Bwana anasema kwamba tunapaswa kufahamu ukweli kwamba haiwi hivyo. Tukikataa kusamehe, hatatusamehewa pia. Inabidi tuwe tayari kuwasamehe wale wanaotukosea. Ni rahisi tu, msamaha haupaswi kuwa jambo la upande mmoja, haipaswi kutarajia Bwana kufanya yote katika kusamehe. Paulo alisema *"tena iweni wafadhili ninyi kwa ninyi, wenye huruma, mkasameheane kama na Mungu katika Kristo alivyowasamehe ninyi."* (Waefeso 4:32). Tena aliasema *"Basi, kwa kuwa mmekuwa wateule wa Mungu, watakatifu wapendwao, jivikeni moyo wa rehema, utu wema, unyenyekevu, upole, uvumilivu, mkichukuliana, na kusameheana, mtu akiwa na sababu ya kumlaumu mwenzake; kama Bwana alivyowasamehe ninyi, vivyo na ninyi."* (Wakolosai 3:12,13).

Nadhani ni wazi kwamba ikiwa wengine wametenda dhambi dhidi yetu, na wanaomba msamaha wetu, lazima tuwasamehe: Hata kama hawaombi, lakini tunapaswa kuwa na nia ya kusamehe na tusiwe na kinyongo nao.

Vipi kama nimemtenda dhambi Mungu na mwanadamu mwenzangu? Tunawezaje kupata msamaha? Biblia inafundisha kwamba ikiwa tumefanya dhambi kibinafsi na kwa siri, yaani ikiwa sisi tu na Mungu ndio tunaijua hiyo dhambi, basi tunapaswa kutubu dhambi hiyo kwa Mungu pekee na kumwomba atusamehe. Katika hilo hakuna haja ya kwenda zaidi ya hapo.

Ikiwa tumemkosea mtu au tumemtendea vibaya, basi tunapaswa kumwendea na kumwomba atusamehe kwa kile tulichofanya, tumwombe msamaha pia tuombe msamaha kwa Mungu, na huo ndio uwe mwisho wake.

Lakini ikiwa tumefanya dhambi hadharani na kumletea aibu Bwana na kanisa lake, lazima twende mbele ya kanisa na kutubu dhambi zetu na kuungama hadharani makosa yetu. Katika Matendo 8 tunaye Simoni, aliyekuwa mchawi, akamtii Bwana ili apate kuokolewa na kuwa mshirika wa kanisa. Lakini alipomwona Petro na Yohana wakiwapa baadhi ya Wakristo Wasamaria uwezo wa Roho Mtakatifu, alijaribiwa

kuwatolea pesa kwa ajili ya nguvu hii Maandiko yanasema, *"Lakini Petro akamwambia, Fedha yako na ipotelee mbali pamoja nawe, kwa kuwa umedhania ya kuwa karama ya Mungu yapatikana kwa mali. Huna fungu wala huna sehemu katika jambo hili, kwa kuwa moyo wako si mnyofu mbele za Mungu. Basi, tubia uovu wako huu, ukamwombe Bwana, ili kama yamkini, usamehewe fikira hii ya moyo wako. Kwa maana nakuona u katika uchungu kama nyongo, na tena u katika kifungo cha uovu. Simoni akajibu, akasema, Niombeeni ninyi kwa Bwana, yasinifikilie mambo haya mliyosema hata moja."* (Matendo 8:20-24). Kwa hiyo Simoni alitubu na kurejeshwa, lakini hakuna ishara kwamba alipewa nguvu za Roho Mtakatifu, asije akapata kujaribiwa akatumia vibaya uwezo huo.

Yesu alisimulia hadithi ya kijana aliyekuwa pamoja na baba yake, alikuwa na kila kitu, lakini aliamua kuchukua urithi wake na kuondoka. Alifanya hivyo na alitumia urithi wake wote kwa maisha ya anasa. Alipojikuta hana kitu, na ili kujiokoa na njaa, ilimbidi afanye kazi ya kulisha nguruwe, ambayo ilikuwa ya kiwango cha chini, heri angerudi nyumbani. Basi rekodi inasema, *"Alipozingatia moyoni mwake, alisema, Ni watumishi wangapi wa baba yangu wanaokula chakula na kusaza, na mimi hapa ninakufa kwa njaa. Nitaondoka, nitakwenda kwa baba yangu na kumwambia, Baba, nimekosa juu ya mbingu na mbele yako; sistahili kuitwa mwana wako tena; nifanye kama mmoja wa watumishi wako. Akaondoka, akaenda kwa babaye. Alipokuwa angali mbali, baba yake alimwona, akamwonea huruma, akaenda mbio akamwangukia shingoni, akambusu sana. Yule mwana akamwambia, Baba, nimekosa juu ya mbingu na mbele yako; sistahili kuitwa mwana wako tena. Lakini baba aliwaambia watumwa wake, Lileteni upesi vazi lililo bora, mkamvike; mtieni na pete kidoleni, na viatu miguuni; mleteni ndama yule aliyenona mkamchinje; nasi tule na kufurahi; kwa kuwa huyu mwanangu alikuwa amekufa, naye amefufuka; alikuwa amepotea, naye ameonekana. Wakaanza kushangilia."* (Luka 15:17 - 24). Kisa hiki kinaonesha kwamba ikiwa tunapotelea mbali kutoka kwa Mungu, lakini tukitubu na kukiri makosa yetu, basi Baba yetu yuko tayari kutusamehe na kuturejesha kwake. Yakobo alisema, *"Ungameni dhambi zenu ninyi kwa ninyi, na*

*kuombeana, mpate kuponywa. Kuomba kwake mwenye haki kwafaa sana, akiomba kwa bidii.”* (Yakobo 5:16).

Sasa angalia upande mwingine. Je vipi ikiwa mtu amefanya dhambi dhidi yetu? Katika hali hiyo, Kristo alisema, *“Na ndugu yako akikukosa, enenda ukamwonye, wewe na yeye peke yenu; akikusikia, umempata nduguyo. La, kama hasikii, chukua pamoja nawe tena mtu mmoja au wawili, ili kwa vinywa vya mashahidi wawili au watatu kila neno lithibitike. Na asipowasikiliza wao, liambie kanisa; na asipolisikiliza kanisa pia, na awe kwako kama mtu wa mataifa na mtoza ushuru. Amin, nawaambieni, yo yote mtakayoyafunga duniani yatakuwa yamefungwa mbinguni; na yo yote mtakayoyafungua duniani yatakuwa yamefunguliwa mbinguni.”* (Mathayo 18:15 - 18).

Dhambi lazima itubiwe na kusamehewa na Bwana ikiwa mtu anataka kukubalika kwake. Unapaswa kukumbuka ukweli huu pindi utakapoanzisha kusanyiko la mahali pamoja ili kuweka kanisa kuwa safi kadri iwezekanavyo.

**Somo la 24**

# JINSI YA KUWA NA USAFI WA KIMAFUNDISHO

Kwa kutumia mada ya **Jinsi ya Kuanzisha Kanisa la Kristo Mahali Ulipo**, lengo letu ni kutoa habari itakayokusaidia kufanya hivyo.

Kama sehemu ya Habari hiyo, somo letu hapa linahusiana na **jinsi ya kuwa na usafi wa mafundisho**.

Tunamaanisha nini tunaposema **usafi wa mafundisho**, na kwa nini ni muhimu sana? Tunazungumzia juu ya mafundisho na kuhubiri mambo ya kweli yanayofanya iwezekane kwa mtu kuokolewa na kubaki mwokovu.

Tunajua kwamba Mungu amesema (Waebrania 1:1,2). Kristo ni "Neno" (Yohana 1:1,2). Kisha tunaambiwa kwamba Roho Mtakatifu aliwaongoza mitume na wengine katika kuandika ujumbe wa Bwana (2 Timotheo 3:16,17; 2 Petro 1:21). Kwa maneno mengine Mungu alitaka tujue mapenzi yake na ametoa hayo mapenzi kwetu katika kurasa za Biblia, na hasa katika kurasa za Agano Jipya, ambalo linatumika kwa watu wa siku zetu.

Baada ya kanisa kuanzishwa Yerusalemu tunasoma, *"ambaye Mungu alimfufua, akiufungua uchungu wa mauti, kwa sababu haikuwezekana ashikwe nao."* (Matendo 2:24). Nini lilikuwa fundisho la mitume? Ilikuwa ni ujumbe kutoka kwa Bwana. Lakini wanafunzi wakadumu humo. Yaani waliendelea kufanya mambo ambayo walikuwa wamefundishwa na Kristo na wakaendelea kuwa na ushirika, kuumega mkate, na katika kusali pamoja. Paulo alizungumza kuhusu mafundisho yenye uzima mara kadhaa. Alisema kwamba dhambi za ulimwengu ni kinyume cha mafundisho yenye uzima (1 Timotheo 1:10). Wakati mwingine alisema kwamba wakati utakuja ambapo watu hawatasikiliza mafundisho yenye uzima (2 Timotheo 4:3). Akizungumzia sifa za wazee maaskofu, Paulo alisema kwamba *"Maana imempasa askofu awe mtu asiyeshitakiwa neno ,kwa kuwa ni wakili wa MUNGU;asiwe mtu wa kujipendeza nafsi yake,asiwe mwepesi wa hasira,asiwe mlevi wala mgomvi,asiwe mpenda mapato ya aibu. bali awe mkaribishaji, mpenda wema, mwenye kiasi, mwenye*

*haki, mtakatifu, mwenye kudhibiti nafsi yake; akilishika lile neno la imani vile vile kama alivyofundishwa, apate kuweza kuwaonya watu kwa mafundisho yenye uzima, na kuwashinda wenye kupinga.".* (Tito 1:7-9).

Maelezo yanayohusika katika sifa za wazee ni hitaji la kuwa katika Imani ya kweli uzima katika kile unachoamini. lakini ili mtu awe mzima katika Imani atalazimika kusikia mafundisho yenye uzima (mapenzi ya Mungu ) kwa kuwa Imani huja kwa kusikia neno la Mungu (Warumi 10:17). Katika Tito 2:7,8 *" katika mambo yote ukijionyesha wewe mwenyewe kuwa kielelezo cha matendo mema, na katika mafundisho yako ukionyesha usahihi na ustahivu, na maneno yenye uzima yasiyoweza kuhukumiwa makosa, ili yule mwenye kupinga atahayarike, kwa kuwa hana neno baya la kunena juu yetu."*

Maandiko yote ambayo tumesoma yanasisitiza maneno kama hayo *"mafundisho yenye uzima", "neno la uaminifu", "uzima katika imani",* na *"hotuba yenye uzima".* Mkazo huu ulikuwa muhimu ili kutukumbusha kuweka mafundisho ya Bwana kama yalivyotolewa hapo awali na kuyalinda dhidi ya mafundisho ya uwongo. Paulo aliendelea kusema, *"Ndugu zangu, nawasihi, waangalieni wale wafanyao fitina na mambo ya kukwaza kinyume cha mafundisho mliyojifunza; mkajiepushe nao. Kwa sababu walio hivyo hawamtumikii Bwana wetu Kristo, bali matumbo yao wenyewe; na kwa maneno laini na ya kujipendekeza waidanganya mioyo ya watu wanyofu."* (Warumi 16:17,18).

Paulo alimsihi mhubiri kijana, Timotheo *"Basi wewe, mwanangu, uwe hodari katika neema iliyo katika Kristo Yesu. Na mambo yale uliyoyasikia kwangu mbele ya mashahidi wengi, hayo uwakabidhi watu waaminifu watakaofaa kuwafundisha na wengine."* (2 Timotheo 2:1,2). Akaendelea *"Nakuagiza mbele za Mungu, na mbele za Kristo Yesu, atakayewahukumu walio hai na waliokufa; kwa kufunuliwa kwake na kwa ufalme wake; lihubiri neno, uwe tayari, wakati ukufaao na wakati usiokufaa, karipia, kemea, na kuonya kwa uvumilivu wote na mafundisho. Maana utakuja wakati watakapoyakataa mafundisho yenye uzima; ila kwa kuzifuata nia zao wenyewe watajipatia waalimu makundi makundi, kwa kuwa wana masikio ya utafiti; nao watajiepusha*

*wasisikie yaliyo kweli, na kuzigeukia hadithi za uongo.”* (2 Timotheo 4:1-4) *“Mtu akisema, na aseme kama mausia ya Mungu; mtu akihudumu, na ahudumu kwa nguvu anazojaliwa na Mungu; ili Mungu atukuzwe katika mambo yote kwa Yesu Kristo. Utukufu na uweza una yeye hata milele na milele. Amina.”* (1 Petro 4:11).

Kwa maonyo haya kama taarifa rejea kuonesha umuhimu wa kweli kama mafundisho yenye uzima, na uaminifu, nataka nikwambie kwamba ikiwa utaanzisha kusanyiko mahali ulipo,basi lazima ifanyike kulingana na mafundisho ya neno la Mungu. Wakubali katika ushirika wako wale tu ambao wamefundishwa mapenzi ya Mungu na wameyatii. Wale wanaomwamini Mungu ambao wametubu dhambi zao, waliokiri Imani yao katika Kristo na wamebatizwa kwa ondoleo la dhambi zao (Marko 16:15,16; Warumi 10:10; Matendo 2:38).

Unaposoma kitabu cha Matendo ya mitume utapata visa vingi vya uongofu vilivyoorodheshwa. Wote walitii ukweli huu na matokeo yake, Bwana aliwaokoa na kuwaongeza katika kanisa lake (Matendo 2:47). Katika Yohana 3:3-5, uongofu umeoneshwa kama kuzaliwa upya. Katika Warumi 6:3,4 na 1 Wakorintho 12:13 wanaambiwa kwamba mtu anapozitii amri hizi anaingia kwa Kristo na kanisa.

Kusanyiko la mahali pamoja litafundisha mpango wa Injili wa wokovu na pia litafundisha kwamba kuna kanisa moja tu na kwamba Kristo alilijenga na ndiye kichwa chake, limejengwa juu yake; linavaa jina lake, kwamba Kristo alikufa kwa ajili yake, yeye ni Mwokozi wake, na kwamba siku moja atarudi kwa ajili yake (Mk 16:15,16; Waefeso 4:4-6; Mathayo 16:18 Wakolosai 1:18; 1 Wakorintho 3:11; Warumi 16:16; Matendo 20:28; Waefeso 5:23 - 27). Nimetoa maelezo hayo kwa mamlaka ya maandiko marejeleo ambayo nimeorodhesha.

Kusanyiko la mahali pamoja litafuata muundo wa kimaandiko katika kuabudu kwa kukutana siku ya kwanza ya juma kuimba, kuomba, kusoma, kushiriki meza ya Bwana na kutoa kwa kadri ya kufanikiwa (Matendo 20:7; Waefeso 5:19; Timotheo 2:15; 1 Wakorintho 11:23 – 29; 1 Wakorintho 16:2).

Kusanyiko la kwenu litawatia moyo washirika wake waishi maisha safi na ya kumcha Mungu. Paulo alisema *“Maana neema ya Mungu iwaokoayo wanadamu wote imefunuliwa; nayo yatufundisha kukataa*

*ubaya na tamaa za kidunia; tupate kuishi kwa kiasi, na haki, na utauwa, katika ulimwengu huu wa sasa; tukilitazamia tumaini lenye baraka na mafunuo ya utukufu wa Kristo Yesu, Mungu mkuu na Mwokozi wetu; ambaye alijitoa nafsi yake kwa ajili yetu, ili atukomboe na maasi yote, na kujisafishia watu wawe milki yake mwenyewe, wale walio na juhudi katika matendo mema. Nena maneno hayo, onya na kukaripia kwa mamlaka yote; asikudharau mtu awaye yote."* (Tito 2:11 - 15).

Kusanyiko la mahali pamoja litajitahidi kusema pale ambapo Biblia inasema na kunyamaza pale ambapo Biblia imenyamaza. Itatoa kila jitihada ya kutoongeza katika neno la Mungu au kupunguza kutoka katika Neno, au kulibadilisha (Ufunuo 22:18, 19; Wagalatia 1:6 - 9).

Moja ya njia bora za kuweka mafundisho ya Bwana safi ni kwa kila mshirika kusoma na kujifunza neno la Mungu (2 Timotheo 2:15). Kwa njia hiyo sio tu watajua kile ambacho Mungu anatarajia kutoka kwao, lakini pia wanaweza kuendelea kujilinda na mafundisho yote ya uwongo. Inapaswa kukumbukwa daima kwamba ukweli pekee ndio humfanya mtu kuwa huru (Yohana 8:23).

## Somo la 25

# JINSI YA KUISHI MAISHA YA KIKRISTO

Mada yetu ya jumla inaendelea kuwa **Jinsi ya Kuanzisha Kanisa la Kristo Mahali Ulipo**. Ni muhimu sana kujua kanisa ni nini na si nini. Kanisa linaundwa na kundi la watu waliookolewa wale ambao wamemtii Bwana kwa kumwamini, kutubu dhambi zao, kukiri Imani yao ndani yake Kristo kama Mwana wa Mungu, na kwa kubatizwa kwa ajili ya ondoleo la dhambi. Kanisa hili lilianzishwa na Kristo, Yeye ndiye kichwa chake, na yeye ndiye Mwokozi wake. Linavaa jina lake kama kanisa na washirika wake wanajulikana kama Wakristo. Kwa upande mwingine, kanisa si jengo la kimwili, au madhehebu yaliyoundwa na wanadamu.

Tunapoendelea na mfululizo huu, sasa tutajadili **jinsi ya kuishi maisha ya Kikristo**. Ikiwa tutakuwa washirika wa kanisa na kuwa na kanisa mahali tulipo basi sisi na wengine itatubidi kuishi maisha ya Kikristo ikiwa kuna mafanikio. Hakuna haja ya kuwa Mkristo kama hatuwezi kuishi maisha ya Kikristo, na kila mtu kuwa Mkristo mwaminifu kwa hilo.

Ili kuwa Mkristo lazima mtu akiri Imani yake katika Kristo kama Mwana wa Mungu. Katika Matendo 8 tunasoma juu ya uongofu wa mtu kutoka Kushi na kabla ya ubatizo wake alisema kwamba aliamini kuwa Kristo ni Mwana wa Mungu. Katika Warumi 10:10 Paulo anasema kwamba ukiri ufanyike hata kupata wokovu. Lakini mtu hatakiwi kukiri tu Imani yake katika Kristo ili kuokolewa,bali lazima aendelee kukiri jina la Kristo katika maisha yake yote ili kubaki mwokovu. Yaani hatakiwi kuwa tayari tu kumkiri Kristo kwa kinywa chake, lakini pia lazima amkiri Kristo kila siku kwa jinsi anavyoishi.

Kama matokeo ya utii wa mtu kwa Kristo anaokolewa na kuongezwa katika familia yake, kanisa. Sasa ni mtu aliyezaliwa mara ya pili (Yohana 3:3 - 5). Kwa hiyo yeye ni kiumbe kipya ndani ya Kristo. Paulo alisema *“ Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita tazama! Yamekuwa mapya.”* (2 Wakorintho 5:17).

Lakini hebu tuendelee kuchunguza jinsi ilivyo kuwa ndani ya Kristo na kuwa mali yake. Paulo aliwaandikia ndugu wa Kolosai, *"Basi mkiwa mmefufuliwa pamoja na Kristo, yatafuteni yaliyo juu Kristo aliko, ameketi mkono wa kuume wa Mungu. Yafikirini yaliyo juu, siyo yaliyo katika nchi. Kwa maana mlikufa, na uhai wenu umefichwa pamoja na Kristo katika Mungu. Kristo atakapofunuliwa, aliye uhai wetu, ndipo na ninyi mtafunuliwa pamoja naye katika utukufu. Basi, vifisheni viungo vyenu vilivyo katika nchi, uasherati, uchafu, tamaa mbaya, mawazo mabaya, na kutamani, ndiyo ibada ya sanamu; kwa ajili ya mambo hayo huja ghadhabu ya Mungu. Katika hayo ninyi nanyi mlitembea zamani, mlipoishi katika hayo. Lakini sasa yawekeni mbali nanyi haya yote, hasira, na ghadhabu, na uovu, na matukano, na matusi vinywani mwenu. Msiambiane uongo, kwa kuwa mmevua kabisa utu wa kale, pamoja na matendo yake; mkivaa utu mpya, unaofanywa upya upate ufahamu sawasawa na mfano wake yeye aliyeuumba. Hapo hapana Myunani wala Myahudi, kutahiriwa wala kutokutahiriwa, mgeni wala mshenzi, mtumwa wala mwungwana, bali Kristo ni yote, na katika yote. Basi, kwa kuwa mmekuwa wateule wa Mungu, watakatifu wapendwao, jivikeni moyo wa rehema, utu wema, unyenyekevu, upole, uvumilivu, mkichukuliana, na kusameheana, mtu akiwa na sababu ya kumlaumu mwenzake; kama Bwana alivyowasamehe ninyi, vivyo na ninyi. Zaidi ya hayo yote jivikeni upendo, ndio kifungo cha ukamilifu. Na amani ya Kristo iamue mioyoni mwenu; ndiyo mliyoitiwa katika mwili mmoja; tena iweni watu wa shukrani. Neno la Kristo na likae kwa wingi ndani yenu katika hekima yote, mkifundishana na kuonyana kwa zaburi, na nyimbo, na tenzi za rohoni; huku mkimwimbia Mungu kwa neema mioyoni mwenu. Na kila mfanyalo, kwa neno au kwa tendo, fanyeni yote katika jina la Bwana Yesu, mkimshukuru Mungu Baba kwa yeye."* (Wakolosai 3:1 - 17).

Tuendelee kusoma maneno ya mtume Paulo kama alivyozungumza kuhusu Wakristo wa siku hizo, na jinsi walivyotegemea nguvu za miujiza kusaidia kanisa kuanza na kukua katika ukomavu. Anasema Bwana *"Naye alitoa wengine kuwa mitume, na wengine kuwa manabii; na wengine kuwa wainjilisti na wengine kuwa wachungaji na waalimu; kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu, hata kazi ya*

*huduma itendeke, hata mwili wa Kristo ujengwe; hata na sisi sote tutakapoufikia umoja wa imani na kumfahamu sana Mwana wa Mungu, hata kuwa mtu mkamilifu, hata kufika kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo; ili tusiwe tena watoto wachanga, tukitupwa huku na huku, na kuchukuliwa na kila upepo wa elimu, kwa hila ya watu, kwa ujanja, tukizifuata njia za udanganyifu. Lakini tuishike kweli katika upendo na kukua hata tumfikie yeye katika yote, yeye aliye kichwa, Kristo. Katika yeye mwili wote ukiungamanishwa na kushikanishwa kwa msaada wa kila kiungo, kwa kadiri ya utendaji wa kila sehemu moja moja, huukuza mwili upate kujijenga wenyewe katika upendo. Basi nasema neno hili, tena nashuhudia katika Bwana, tangu sasa msienende kama Mataifa waenendavyo, katika ubatili wa nia zao; ambao; akili zao zimetiwa giza, nao wamefarikishwa na uzima wa Mungu, kwa sababu ya ujinga uliomo ndani yao, kwa sababu ya ugumu wa mioyo yao; ambao wakiisha kufa ganzi wanajitia katika mambo ya ufisadi wapate kufanyiza kila namna ya uchafu kwa kutamani. Bali ninyi, sivyo mlivyojifunza Kristo; ikiwa mlimsikia mkafundishwa katika yeye, kama kweli ilivyo katika Yesu, mvue kwa habari ya mwenendo wa kwanza utu wa zamani, unaoharibika kwa kuzifuata tamaa zenye kudanganya; na mfanywe wapya katika roho ya nia zenu; mkavae utu mpya, ulioumbwa kwa namna ya Mungu katika haki na utakatifu wa kweli. Basi uvueni uongo, mkaseme kweli kila mtu na jirani yake; kwa maana tu viungo, kila mmoja kiungo cha wenzake. Mwe na hasira, ila msitende dhambi; jua lisichwe na uchungu wenu bado haujawatoka; wala msimpe Ibilisi nafasi. Mwibaji asiibe tena; bali afadhali afanye juhudi, akitenda kazi iliyo nzuri kwa mikono yake mwenyewe, apate kuwa na kitu cha kumgawia mhitaji. Neno lo lote lililo ovu lisitoke vinywani mwenu, bali lililo jema la kumfaa mwenye kuhitaji, ili liwape neema wanaosikia. Wala msimhuzunishe yule Roho Mtakatifu wa Mungu; ambaye kwa yeye mlitiwa muhuri hata siku ya ukombozi. Uchungu wote na ghadhabu na hasira na kelele na matukano yaondoke kwenu, pamoja na kila namna ya ubaya; tena iweni wafadhili ninyi kwa ninyi, wenye huruma, mkasameheane kama na Mungu katika Kristo alivyowasamehe ninyi.."* (Waefeso 4:11 - 32).

Unaweza kuona katika mistari hiyo yote ya maandiko kwamba, kuwa Mkristo maana yake ni nini?. Ni ile hali ya kuishi maisha safi na ya kumcha Mungu; ni hali ya kumtumikia Mungu na kuwasaidia wanadamu wenzako.

Kupitia utiifu wetu kwa Bwana tunalichukua jina la Kristo (Matendo 11:26; 1 Petro 4:16). Kwa kufanya hivyo tunamheshimu na kumtangaza yeye kama Bwana na Mwokozi wetu. Tunasema kwamba tunaishi ndani yake na Yeye anaishi ndani yetu. Kwa hiyo hatupaswi kuchukua tu jina la Bwana, bali tunapaswa kumkiri Kristo kila siku kwa matendo yetu.

Iwe sisi ni washirika wa kusanyiko changa au wa kusanyiko la muda mrefu, liwe dogo au kubwa, bado tunapaswa kuzingatia kuwa sisi ni nani na tunawakilisha nini.

Wakati mwingine tunasikitika kwa sababu ya kuacha yote ili tuwe Wakristo na tunaweza hata kufikiri kwamba ni vigumu kuwa Mkristo. Lakini tunahitaji kupata vipaumbele vyetu sawa. Mungu hajatutaka tuache jambo lolote jema. Ametuomba tugeuke kutoka katika mambo mabaya na katika makosa ambayo yanaweza kutudhuru na kutuangamiza. Hiyo inatumika katika maisha yetu ya kimwili na kiroho. Tunaye Bwana ambaye ameahidi kuwa pamoja nasi na kutusaidia. Tuna maombi ambayo kwayo tunaweza kumwomba Baba yetu msaada. Tuna ndugu zetu wanaohitaji msaada na kutiwa moyo. Hakika Mkristo amebarikiwa kuliko wengine wote.

## Somo la 26

# JINSI YA KUSHUGHULIKA NA MATATIZO

Wewe ambaye umekuwa nasi katika mfululizo huu wote tunapaswa kulifahamu vyema kanisa la Bwana wetu kwa sasa; jinsi ya kuwa washirika wake, na hata **jinsi ya kuanzisha kusanyiko mahali ulipo**. Sijui ni wangapi wanachukulia kwa umakini jambo hili, lakini natumaini kupitia mfululizo wa masomo haya wengi watatilia mkazo na kuanzisha makusanyiko mapya mahali mlipo na duniani kote.

Sasa tunakuja kwenye somo ambalo litahusu **jinsi ya kukabaliana na matatizo**. Ndiyo kutakuwa na matatizo yatakayojitokeza. Maswali yataulizwa ambayo yatahitajika kuwa na majibu. Labda kwa kutafakari baadhi yao na kujaribu kutoa baadhi ya majibu, utakuwa msaada kwako wakati maswali yanapokujia.

Hapo zamani za kale Petro alisema, *"Mwe tayari siku zote kumjibu kila mtu awaulizaye habari za tumaini lililo ndani yenu; lakini kwa upole na kwa hofu."* (1 Petro 3:15).

**Je tuna haki ya kufasiri maandiko?** Msikilize Petro tena jinsi anavyosema, *"Mwe tayari siku zote kumjibu kila mtu awaulizaye habari za tumaini lililo ndani yenu; lakini kwa upole na kwa hofu."* (1 Petro 3:15).

**Je Biblia inafundisha kwamba wokovu ni kwa njia ya Imani pekee?** Tunaokolewa kwa Imani lakini si kwa Imani tu. Ikiwa mtu anaamini kweli au ana aina ya Imani inayookoa, atafanya yale ambayo Bwana amemwagiza afanye. Ikiwa hana aina hiyo ya Imani, basi yeye hawezi kuokolewa. Kristo alisema *"Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini, atahukumiwa."* (Marko 16:16). Kristo alisema lazima tufanye mapenzi ya Baba (Mathayo 7:12). Yakobo alisema kwamba tunapaswa kuwa watendaji wa neno (Yakobo 1:22). Pia alisema *"Vivyo hivyo na imani, isipokuwa ina matendo, imekufa nafsini mwake."* (Yakobo 2:17).

**Ubatizo unawezaje kuokoa?** Kama ilivyokuwa kwa upande wa Imani peke yake vilevile hauwezi. Ubatizo huja baada ya mtu kumwamini Bwana kiasi cha kutubu dhambi zake, kukiri Imani yake kwa Kristo kuwa ni Mwana wa Mungu, na kisha kwa kutii amri ya

kubatizwa, kwa kuzikwa katika maji ili kuosha dhambi zake (Waebrania 11:6; Luka 13:3; Mathayo 10:32; Warumi 6:3,4).

**Je kuna njia nyingi za kwenda mbinguni?** Kristo alisema *"Yesu akamwambia, Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima; mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya mimi."* (Yohana 14:6).Tena alisema *"Maneno hayo nimewaambia, msije mkachukizwa."* (Yohana 10:1). Baada ya Bwana kuweka hilo wazi kabisa unadhani kuna njia ngapi za kwenda mbinguni? Kwa nini Bwana ajisumbue kutoa njia kama kulikuwa na njia nyingine nyingi?

**Je, mtu hawezi kuokolewa na kwenda mbinguni bila kuwa mshirika wa kanisa lolote?** Ni kweli kwamba mtu anaweza kuokolewa na kwenda mbinguni bila kuwa mshirika wa madhehebu na makanisa yaliyoanzishwa na wanadamu, lakini mtu lazima awe mshirika wa kanisa la Bwana wetu ili kuokolewa katika ulimwengu huu nakatika ulimwengu ujao. "lakini hata kanisa la Kristo haliokoi, sivyo? Hapana , lakini Kristo ndiye Mwokozi wa kanisa (Waefeso 5:23). Kwa hiyo mtu lazima awe ndani ya kanisa ili aokolewe. Safina aliyoijenga Nuhu haikuwa mwokozi. Lakini Nuhu na familia yake walipaswa kuwa ndani ya Safina ili waokolewe. Paulo alisema kwamba mwishowe Kristo atakabidhi ufalme wa Mungu au kanisa kwa Baba yake (1 Wakorintho 15:24). Sasa kama atakwenda kulikabidhi kwa Mungu itakuwaje kwa wale ambao si washirika wake? Nadhani unajua.

**Je, sheria ya Musa inawafunga Wakristo leo? Ikiwa ndivyo kwa nini Kristo alikufa msalabani ili kutupa sheria iliyo bora zaidi na yenye ahadi bora?** Sheria (Torati) isingeondoka mpaka yote yatimie, na haikufanywa hivyo (Mathayo 5:18). Mwandishi wa wa kitabu cha Waebrania anasema hivi; *"ndipo aliposema, Tazama, nimekuja niyafanye mapenzi yako. Aondoa la kwanza, ili kusudi alisimamishe la pili."* Agano Jipya, kupitia kwa njia Yesu Kristo (Waebrania 10:9,10). Hapana hatujaachwa bila sheria zinazohusu kuua, kuiba, n,k. kwa vile zinapatikana katika Agano Jipya. Je, kuna ubaya gani kuwa na muziki wa ala katika ibada? Hapo hakuna ubaya juu ya muziki wa ala kwenye sehemu kwa mfano kama kwenye burudani, nyumbani, n.k, lakini linapokuja suala la ibada, hilo ni jambo lingine. Bwana amebainisha kwamba anatutaka tumsifu kwa sauti zetu

(Waefeso 5:19; Wakolosai 3:16). Angeagiza vitumike vyombo vya muziki basi ndivyo ingekuwa, lakini hakufanya hivyo. Hivyo ni suala la kufikiria kama tunataka tumpendeze Bwana au tujipendeze sisi wenyewe. Inashangaza jinsi wanadamu wanavyotaka kuwa na njia yao katika kila kitu, na namna ambavyo wanajaribu kuhalalisha.

**Ni mara ngapi Wakristo wanapaswa kushiriki meza ya Bwana?** Tuna mfano wa mahali walipokutana siku ya kwanza ya juma kumega mkate (Matendo 20:7). Wakristo wanapaswa kukutana mara ngapi kuabudu? Mara moja kwa wiki au kila jumapili, sivyo? Sawa. Hivyo ndivyo Wakristo wanavyopaswa kushiriki Meza ya Bwana.

**Je, kimaandiko kusanyiko la Bwana linaweza kufanya kazi bila ya kuwa na wazee na mashemasi?** Ndiyo, kwa sababu inachukua muda kwa wanaume kustahili kuwa wazee na mashemasi (1 Timotheo 3; Tito 1). Ni lazima liwepo kabla ya kuwa na wazee vile ambavyo litakuwepo baada ya kuwa na wazee. Kabla halijapata watu wenye sifa, wanaume wakusanyike watalazimika kuchukua mamlaka katika kusanyiko hilo. Ingekuwa bora kuwa na wazee na mashemasi na hii inatia moyo, lakini ikiwa hakuna wanaume wa kutosha waliotimiza sifa, basi itakuwa afadhali kusanyiko lisiwe nao. Kwa kusanyiko kuweka wanaume wawe wazee na mashemasi wakati hawastahili kutaleta madhara zaidi kuliko mema.

**Mtu mmoja anawezaje kuanzisha kusanyiko la Bwana?** Lazima pawepo mwanzilishi. Ikiwa wewe ni mshirika, ukamfundisha mtu mmoja au zaidi, na wanaamua kwamba wanataka kumtii Bwana, basi pamoja nao una kiini cha mwanzo wa kusanyiko. Ikiwa unataka tu bila kufanya chochote, huwezi kuanza chochote kwa njia hiyo. Lakini ikiwa unampenda Bwana nawe unataka kuona kusanyiko mahali ulipo, kama wewe utaamka na kuweka jitihada, basi unaweza kuanzisha kusanyiko.

Pengine tunaweza kuendelea na kujibu maswali, lakini kabla ya kufunga somo letu, wacha nikutie moyo kuwa ujilinde na mafundisho ya uwongo. Jambo linapokuja ,hata kama limetokea kwa ndugu, hakikisha unalichunguza kwa kuzingatia kile ambacho Biblia inafundisha kabla ya kulikubali. Hupaswi kuwa mkarimu, katika kuonesha msimamo wako linapokuja suala la kusimama kwenye

mambo mbalimbali. Kuna njia ambayo ni sawa, na wewe unatakiwa kufanya uwezavyo kuifuata njia hiyo, njia ya Bwana.

Hiyo inanipelekea nishauri kwamba wewe na washirika wengine wa kusanyiko mnapaswa kujitahidi sana kuwa wenye ujuzi wa maandiko. Lijue neno la Mungu. lizoee, soma na ujifunze. ukifanya hivyo hutadanganywa kirahisi.

Ninakuombea ufanikiwe katika juhudi zako za kuanzisha kusanyiko mahali ulipo. Usikate tamaa na kuacha, bali kaa nalo na endelea kulifanyia kazi. Uwe mwaminifu kwa Bwana na atakubariki kwa hilo.